
HARAKATI ZA WILLY GAMBA
HOFU
A. E. MUSIBA

# SURA YA KWANZA

## PORT ELIZABETH

Ilikuwa tarehe 24 Machi, baada ya mauaji ya kikatili ya waafrika 19, katika kitongoji cha Langa, karibu na Vitenhage; mji ulio karibu na ule mji wa viwanda wa Port Elizabeth, katika Jimbo la Cape Mashariki. Mauaji hayo yalikuwa yamefanyika tarehe 21 Machi, siku ya kukumbuka mauaji ya kikatili kwenye mji wa Sherpville mnamo mwaka 1960. Wakati wazalendo 69 walipouawa kikatili. Mnamo tarehe hiyo ya 24 Machi, huko mjini Port Elizabeth kulifanyika mkutano katika ofisi ya Mkuu wa Polisi mnamo saa sita usiku.

Ndani ya chumba cha mkutano huo walijumuika watu ambao wamekuwa chanzo cha vilio na malalamiko mengi kutoka kwa wazalendo wa Afrika Kusini dhidi ya makaburu. Katika mkutano huo alikuwemo waziri wa sheria na usalama wa makaburu, Kamishna wa Polisi, Mkurugenzi wa shirika la Ujasusi la makaburu na Kamanda wa kikosi cha Jeshi kiitwacho 'KULFUT'yaani 'Gongo la Chuma' wote hao walikuwa ni makaburu. Lakini vile vile mkutano huo ulihudhuliwa na watu weusi ambao walikuwa wameitwa haraka haraka.

Hawa walikuwa wamefanyiwa mipango maalumu ya usafiri ili mladi wafike kwenye mkutano huo muhimu. Walikuwa wamesafiri kwa kutumia ndege ya Jeshi la Anga la makaburu. Weusi hawa walikuwa ni Mkuu wa Magaidi wa UNITA, wenye kupinga Serikali ya Angola, Mkuu wa Magaidi wa MNR wenye kupinga Serikali ya Msumbiji na Mkuu wa Magaidi wa LLA wenye kupinga Serikali ya Lesotho, kwa kifupi tu ni kwamba, Magaidi wote hawa ni vibaraka wa Serikali ya Makaburu na ilikuwa ni serikali ya makaburu iliyowagharamia kufanya ujahili dhidi ya nchi zilizo mstari wa mbele katika Ukombozi wa Afrika Kusini, ili kuzizorotesha kisiasa na kiuchumi kwa nia ya kuziangusha hatimaye. Waziri wa sheria, ambaye alikuwa Mwenyekiti wa mkutano huo, alianza kwa kusema;

"Kwanza lazima nitoe shukrani zangu kwa nyinyi wote kuweza kufika hapa kwa muda uliopangwa, shukrani zangu za dhati ziwaendee nyinyi wageni wetu ambao mmetoka nje ya nchi hii. Pili tumeitana hapa usiku wa manane kuzungumzia suala muhimu sana. Ningependa tufanye na kumaliza mazungumzo yetu usiku huu ili muweze kuondoka kabla hapajapambazuka, kwani shughuli hii ni ya siri sana. Mimi nikiwa mwana siasa nitazungumza tu kwa ujumla kuhusu nia ya mkutano.

Halafu nitawaachia wataalamu wa utekelezaji walio hapa kuchambua vipengele vinavyohusika kwa undani zaidi".

"Nafikiri nyote mnaelewa kwamba kumekuwa na wimbi la maasi la waafrika katika nchi nzima ya Afrika Kusini. Wimbo hili, kwa kiasi fulani limetutia wasiwasi. Migomo imeongezeka katika sehemu za kazi kiasi cha kutishia uchumi wa nchi yetu. Maandamano yameongezeka kiasi cha kutishia utulivu na amani ya wananchi. Vitendo vya hujuma vinavyofanywa na magaidi wanaojiita wapigania uhuru'wa Afrika Kusini vimeongezeka kiasi cha kutishia mashirika ya nje yenye rasilimali zao humu nchini.

"Sasa Serikali imeamua kukomesha vitendo vyote hivi. Serikali ilikuwa na nia ya kulegeza vipengele fulani fulani katika sheria zetu kwa manuafaa ya weusi. Lakini imegundulika kuwa kufanya hivyo kutawafanya watu hawa kuwa kichwa ngumu zaidi. Na kama alivyosema Rais wetu, hakuna mtu yeyote Ulimwenguni atakaetuzuia kulinda usalama wa nchi yetu na watu wake wapendao amani!'. Na hapa nasisitiza tena hatutaki mchezo.

"Ghasia hizi ambazo zimekuwa zinaendelea zimefanya mashirika na makampuni kutoka nje kuwa na mtazamo mpya. Yanaanza kuwa wasiwasi juu ya uwezo wetu na pia kuelekea kuwa na imani katika vyama vinavyodai vinapigania uhuru. Hali hiyo siyo nzuri na ni tishio kubwa kwetu".

"Uchumi wetu umeanza kuanguka. gharama za maisha zimepanda kwa kadri asilimia kumi na saba!, ukame umeathiri uzalishaji wa chakula. Bei ya dhahabu imeanguka saba mwaka huu na kufanya bei za vitu muhimu, kama vile Petroli, kuongezeka kufuatana na kushuka kwa thamani ya fedha yetu, ukilinganisha na thamani ya dola ya kimarekani. Jumuia ya Kimataifa inapiga kelele na kuyataka makampuni yasiweke raslimali na vitegauchumi vyao nchini mwetu".

"Mambo yote haya yanatokana na mwamko wa Ulimwengu dhidi ya siasa yetu ya ubaguzi. suala la kuzungumzia ni nini kufanyike ili kulekebisha hali hii ndio sababu leo mko hapa kutafuta ufumbuzi. kuanzia sasa tunataka kufanya macho ya Jumuia ya Kimataifa kuelekea sehemu nyingine ili sisi tupate nafasi ya kurekebisha mambo humu nchini. Macho yao yanataka yaelekee kwenye nchi zilizo mstari wa mbele na vile vile Namibia. Tutafanya vitendo katika nchi hizo vitaifanya Jumuia ya Kimataifa kushughulikia sana; ikitafuta njia za kuwasaidia wananchi wa hizo. Wakati Jumuia ya Kimataifa inashughulika kiasi hicho, sisi tutaanza kuwapa fundisho hawa watu weusi wanaoleta ghasia hapa nchini. Jumuia ya Kimataifa ikija kugeuza macho yake kuyaelekeza kwetu. tutakuwa tumeisha

wakomesha hawa watu weusi ambao ni wakorofi watakuwa wamenyooka kama mpini".

"Hivyo tumeamua kuanzisha 'UTAWALA WA HOFU' dhidi ya weusi walio humu nchini na pia walio katika nchi zilizo mstari wa mbele kwa ujeuri. Ni imani yangu kuwa mmenielewa na ninawashukru tena kwa kunisikiliza. Wakuu wote wa usalama wako hapa. watawaeleza jinsi utekelezaji wa jukumu hili utakavyokuwa. Ahsanteni sana".

Alipomaliza kusema hayo, Waziri wa sheria na usalama alifunika jalada lake, kisha akasimama na wengine wakasimama pia. Huku akiwapungia mkono wa kwaheri, Waziri alisindikizwa na Kamishina wa Polisi mpaka kwenye mlango. Alifunguliwa mlango huo na kutokomea gizani.

Baada ya Kamishina wa Polisi kurudi kwenye nafasi yake, Mkurugenzi wa shirika la Ujasusi la Makaburu alichukua uwanja kueleza namna ya utekelezaji wa mpango huo.

"Nafikiri nyinyi wote mmemsikiliza waziri kwa makini. Mambo ni kama hayo na hatuna budi kutekeleza, nyinyi wenzetu wa UNITA, MNR na LLA tunahitaji msaadawenu kikamilifu. Tumesaidiana mambo mengi sana. Bila sisi kusingekuwepo na UNITA, MNR au LLA", alisema huku akiwakazia macho viongozi wa vyama hivyo vya magaidi.

Wote walimwemwesa huku wakionyesha kwa vichwa vyao ishala ya kukubaliana nae.

"Kuanzia sasa misaada kwenu inaongezwa mara dufu". Wote walishangilia kwa kupiga makofi.

"Lakini", aliendelea Mkurugenzi wa Shirika la Ujasusi la Makaburu, "Misaada hii haikuongezwa bure. Kutakuwa na kazi kubwa ya kufanya. Alinyamaza huku akiwaangalia viongozi wa magaidi kujua kama walikuwa wanampata. "Mmesikia kuwa tunaanzisha utawala wa hofu' dhidi ya watu weusi waliomo humu nchini na pia nchi zilizoko mstari wa mbele pamoja na Namibia. Utekelezaji wa mpango huo utakuwa kama ifuatavyo.

"Kwanza sisi tutajitangazia uhuru nchini Namibia. Baada ya kufanya hivyo tutapambana na SWAPO. Kama ikibidi tutauwa watu Namibia kwani nchi ile ni lazima kuitawala. Tumeanzisha Jeshi linaloitwa KULFUT, yaani Gongo la Chuma'. Hili ndilo Jeshi litakalosababisha Hofu huko Namibia na nchi fulani fulani

zinazojidai kuwa mstari wa mbele. Jeshi hili limeundwa na Makomandoo watupu na lenye uwezo mkubwa.

Limefundishwa kwa kipindi cha miaka kumi sehemu mbali mbali Ulimwenguni na sasa liko tayari kabisa kutia hofu popote litakapotumwa. Upande wetu umejiweka tayari. Baadhi ya vikosi vya Jeshi hili vitaletwa kwenu".

Wajumbe walipiga makofi.

"UNITA", aliendelea "Kazi yenu itakuwa kutia hofu huko Angola. Hakuna mazunguzo na Serikali ya Angola tena. Mtapewa kila msaada wa hali na mali. Lazima kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi hiyo unaanguka kabisa. Kamanda wa KULFUT yupo hapa atapewa kikosi cha Jeshi hilo kusaidia katika dhima hiyo, wapiganaji wenu wasiwe na huruma, bali kuchinja na kuua kiumbe chochote kilicho mbele yenu. Hakikisha mnawaangamiza wale wote wanaojiita wapigania uhuru wa Namibia. Sisi tuko nyuma yenu kwa lolote lile litakalotokea. Nguvu zetu mnazijuwa. Kwa hoyo hakuna atakayechezea".

"Nyinyi MNR", alimgeukia kiongozi wa MNR, "Kazi yenu mnaijuwa. Kama watakavyofanya hawa watu wa UNITA. Fanyeni vurugu ndani ya Msumbiji. Watu wapate hofu kuliko wale walioishi wakati wa NAZI iliyosababishwa na Wajerumani".

Mara alimuona Kamanda wa MNR amenyoosha kidole akitaka kuzungumza.

"Eh, unasemaje?, aliuliza kwa shauku kubwa.

"Sisi tuko tayari kabisa", alisema Kamanda wa MNR, "Lakini lazima niseme kwamba mkataba wenu wa Nkomati unatutatanisha. Ni mkataba wa amani kati ya Msumbiji na Afrika Kusini. Sasa kwetu sisi kuendeleza mapambano inakuwa vigumu ingawa mnatusaidia. Mkataba huo unatuathiri sana".

Mkurugenzi wa Shirika la Ujasusi la Makaburu alijibu. "Achana na siasa. Mkataba wa Nkomati ni siasa tu. Sahau kabisa. Tangu uwekwe saini hakuna mtu ambaye ameutekeleza. Ndio sababu misaada kwenu imeendelea. Kazi yenu ni kama nilivyosema: fanya hali ya Msumbiji iwe ya hofu tupu. Lengo la mkataba wa Nkomati ilikuwa kuwachota akili viongozi wa serikali ya Msumbiji. Tumegundua kwamba wanawaogopa sana nyinyi watu wa MNR. Nyinyi ndio mlikuwa chanzo cha mkataba huo. Walitaka amani. Sasa kinachohitajika ni kuwatia hofu zaidi kwa vita na si ajabu mkachukuwa madaraka. La sivyo, angalau waje kusujudu kwetu na kutulamba miguu. Kwa hivyo sahau kitu kama mkataba wa nkomati".

"Nakuapia", alisema Kamanda wa MNR, "Watakiona cha mtemakuni".

Ndipo Mkurugenzi wa shirika la Ujasusi la Makaburu alipoendelea, "Kazi ya LLA haina tofauti na wengine askari kutoka jeshi la KULFUT watawasaidia kuleta vurugu na hofu kubwa huko Lesotho na Botswana. Sisi tuachieni Zimbabwe, Zambia na Tanzania. Vikosi vyetu maalumu vya uhujumu katika Jeshi la KULFUT vitazionyesha cha mtemakuni nchi hizo. Ili kuonyesha nguvu zetu, sisi tutaanzia Tanzania. Tunataka tutie vurugu na kuleta rindi la hofu katika nchi hiyo dunia itashangaa. Tanzania haijawahi kupewa fundisho kwa sababu hiyo nchi ina kiburi na ndio shina la hawa wanaojiita wapigania uhuru".

"Bila Tanzania, hawa watu wasingetupa taabu kiasi hiki. Nchi hiyo inawapa hifadhi watu hao na kuwapatia mafunzo ya kijeshi. Baadae inawapenyeza kwetu na kutupa shida, shambulizi tutakalofanya huko Tanzania. litawatia hofu hao wanaojiita wapigania uhuru na kuwafanya wasambae bila mpango, itawachukua karne nzima kuweza kujikusanya tena. Litakuwa pigo takatifu ambalo litaiacha dunia nzima inagwaya. Mipango ya awali juu ya kipigo hicho iko tayari na hatuna wasiwasi".

Mkuu wa UNITA aliamusha mkono ikiwa ni ishara yake ya kuomba kusema.

"Eh, unasemaje?". Mkurugenzi wa Shirika la Ujasusi la Makaburu alimuuliza Mkuu wa UNITA.

"Mimi nasikia moyo wangu unakwenda mbio kwa shauku", alisema Mkuu wa UNITA. "Kama kweli mtaipa kipigo Tanzania mpaka ikakoma kutamba, basi sisi kazi yetu itakuwa rahisi kama kunywa maji. Nchi hiyo ina kiburi na ndio inayowapa kichwa ngumu wale wanaodai kupigania uhuru, na nchi nyingine za mstari wa mbele. Iwapo Tanzania itashika adabu, basi vyama vyetu vitapata ushindi wa kutawala. Lakini napenda kukutahadhalisha kuwa nchi hiyo ni imara sana. Mimi nimewahi kuishi huko na ninajua kazi yenu haitakuwa rahisi".

Mara alikatizwa na Mkurugenzi.

"Usiwe na wasiwasi", Mkurugenzi alianza kujitapa. "Hakuna nchi itakayonusurika. Na Tanzania itakuwa ya kwanza. Nyinyi mtasikia. Kusema kweli baada ya kipigo hicho, hao wapigania uhuru; na pia nchi nyingine zilizo mstari wa mbele watabaki wanagwaya".

"Ili yakutoke mashaka", alidakiza Kamanda wa KULFUT, "Matayarisho ya kipigo hicho yalianza siku nyingi. Jeshi la KULFUT likishikiana na Shirika la Ujasusi

hakuna wasiwasi kuhusu kipigo hicho, nakuhakikishia kuwa Tanzania na wenzake watakipata cha mtemakuni. Tumetumia miaka kumi kujitayarisha na muda huo siyo mchezo".

"Saa zimekwenda sana. Tumetumia muda mwingi sana kuzungumzia suala hili wakati ambapo nyie mnapaswa kuondoka kwa siri sana kabla ya mapambazuko". Hapa Mkurugenzi alinyamaza kidogo kisha akaendelea kusema. "Kamanda wa KULFUT' atawapatia msaada mnaohitaji katika kutekeleza mpango huo. Hatuwezi kukubali kushindwa kwani hiyo ina maana kuwa huo utakuwa ndio mwisho wetu - kitu ambacho hakiwezekani. Lazima nipate ripoti ya maendeleo ya mpango huu kila siku ili niweze kuipa taarifa serikali. Kamishina wa Polisi anasema hana wasiwasi juu ya weusi wa hapa kwani atawatia vurumai mpaka wajute kuzaliwa".

“Nafikiri mmesikia kuwa mwezi Februali tuliwakamata vingozi wa vyama vya upinzani. Hao tumewaweka kiporo na baada ya kuipa kipigo Tanzania. Nyinyi mtasikia vurumai tutakavyoifanya, au uongo Kamishina?".

Akionyesha majivuno, Kamishina wa Polisi alijibu, "Watajuta kuzaliwa kwani walikuwa wanaleta mchezo. walikuwa wamediliki kusababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe hapa nchini. Kitu kama hicho hakiwezi kutokea wakati bado niko hai".

Mkurugenzi alifunga mkutano huo kwa dharura kwa kusema, "Ahsanteni sana. Ni mategemeo yangu kuwa mmeelewa hali halisi na hivyo mtatekeleza itasavyo. Naamini tutakapokutana tena kwenye mkutano kama huu hali haitakuwa hivi, bali kusherekea ushindi dhidi ya adui. Sura ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara itabadilika kwa kupata tawala mpya".

Mkutano ulifungwa saa kumi na moja alfajiri.

***

HARARE

Ilikuwa tarehe 1 Aprili, Juma moja baada ya Mkutano uliofanywa na Maafisa wa Makaburu na vikaragosi vyao Mjini Port Elizabeth. Siku hiyo kulifanyika mkutano mwingine. Mkutano huo ulikuwa kati ya watu tofauti na wale Makaburu, mikutano yao ilikuwa na uhusiano. Mkutano huu ulifanyika mjini Harare, Zimbabwe, katika ofisi za wapigania uhuru wa Afrika Kusini. Tofauti na ule mkutano wa Makaburu uliofanyika usiku, mkutano wa wapigania uhuru ulifanyika mnamo saa nne hivi

asubuhi. Mkutano huo ulifanyika katika ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Chama cha kupigania uhuru. Waliohudhuria mkutano huu ni yeye Mkuu wa Upelelezi, Mkurugenzi wa Upelelezi na Serikali ya Zimbabwe pamoja na kijana mmoja aitwae Bon Sipele.

Huenda itakuwa kwa faida yako kama nitakueleza kidogo juu ya kijana huyu mradi usiniite mmbeya. Lakini kwa kuwa mimi huwa sisengenyi, fahamu kwamba mambo nitakayokueleza ni kweli tupu. Kijana Bon Sipele alikuwa na umri yapata miaka ishirini na nane. Kijana huyu alikuwa mzalendo wa Afrika Kusini ambaye alizaliwa katika kijiji cha Soweto. Kijana huyu alianza kujulikana kama mwana mapinduzi akiwa bado mbichi. Alipokuwa na umri yapata miaka kumi na tisa, yeye na wenzake baada ya kumaliza darasa la kumi na nne walivamia mitaa wakiwa na mawe na chupa kuupinga utawala wa kibaguzi wa Makaburu. Serikali ilijibu kuwa kuwauwa baadhi ya vijana hao na kuwatia ndani wengine. Bon pamoja na wenzake walipata bahati ya kutoroka. Huku wakisaidiwa na wapigania uhuru, waliweza kuingia Zambia na hatimaye Tanzania. Bon alijaa uchungu kutokana na vitendo vya kikatili vya Makaburu. Hivyo aliapa kuwa angejitoa mhanga kupigania uhuru wa nchi yake.

Bon alipewa nafasi ya kwenda nje ambapo alipata mafunzo ya kijeshi kijana huyu alipitia mafunzo magumu huko Urusi, China, Cuba na Korea Kasikazini. Aliporudi kutoka kwenye mafunzo alikuwa na ujuzi wa hali ya juu. Aliombwa kukaa katika ofisi za wapigania uhuru zilizo Tanzania ili awe mkuu wa idara ya uendeshaji vita. Lakini, Bon alikataa kazi hiyo kwani alitaka kuishi katika hali halisi ya vita. Hivyo alikwenda moja kwa moja mpaka Msumbiji kupambana na Wareno na Makaburu huko msituni. Baadaye aliweza kuhujumu viwanda kadhaa, mitambo ya umeme pamoja na Reli ndani ya Afrika Kusini. Bon aliwatia homa Makaburu.

Vyama vya wapigania uhuru viliona Bon alikuwa anafaa kuwa mpelelezi ili awakabiri majasusi wa Makaburu kutokana na ujasili wake na mafunzo aliyokuwa nayo. Baada ya muda siyo mrefu Bon alitokea kuwa mpelelezi aliyesifika na kuogopwa katika sehemu hii ya Kusini mwa Afrika. Makaburu walimhala kutokana na hasara kubwa aliyowatia. Serikali ya Afrika Kusini ilikuwa inamtafuta bila kufanikiwa. Kijana huyu ndiye Bon Sipele.

Tunarudi kwenye mkutano uliokuwa ukifanywa na watu hao watatu.

Mkurugenzi wa upelelezi wa Zimbabwe ndiye alikuwa mtu wa kwanza kutoa hoja yake. Alisema, "Tumekusanyika hapa ili niweze kuwaeleza ama sote kuzungumza

suala muhimu. Habari kuhusu suala hilo nimezipata kutokana na kazi yangu, suala hili linawahusu nyinyi pia. Ndio sababu nimeona ni vizuri niwahusishe".

Alimeza mate kulainisha koo akaendelea, "Mnakumbuka kuwa hapa majuzi watu wetu walifanya operesheni kwenye sehemu ya Beitbridge katika mpaka wetu na Makaburu. Mtakumbuka pia kuwa watu wetu waliweza kuvunja kundi la Majasusi waliokuwa wanafanya ujahili dhidi ya nchi yetu kutokana na amri za Makaburu".

"Tunakumbuka", walijibu kwa pamoja.

"Katika operesheni hiyo", Mkurugenzi aliendelea, "Tuliweza kuwakamata Majasusi ishirini. Baada ya kuyakamata, vijana wetu kama mjuavyo walishughulika kikamilifu. Baada ya kuhojiwa mmoja wao alitoa taarifa ambayo imetufanya tuwe macho. Kwa sababu hiyo nimelazimika kuwapa habari hizi. Kutokana na ripoti niliyopata ofisini kwangu ni kwamba, Makaburu wamebuni mpango wa kukomesha mashambulizi dhidi yao. Utekelezaji wa mpango huo ni kwamba Makaburu watatoa kipigo kitakatifu ambacho kitamaliza kabisa nguvu za wapigania uhuru kiasi kwamba wale watakaobahatika kubaki hawatathubutu kufanya mashambulizi dhidi yao. Vile vile kuna mpango wa kushambulia nchi yetu baada ya kipigo dhidi ya wapigania uhuru. Sasa kama inavyofahamika, viongozi wa wapigania uhuru wamesambaa katika nchi mbali mbali. Wako kwenye nchi zilizo katika mstari wa mbele. Vilevile wako katika nchi kadhaa za Afrika na hata nchi rafiki za Ulaya. Hivi tumefikiri sana juu ya hali hii lakini hatujapata ufumbuzi. Ndio sababu imeonekana ni vizuri tutafute ufumbuzi wote kwa pamoja".

Mkurugenzi wa upelelezi wa Zimbabwe alipomaliza kusema chumba kikajaa ukimya.

Baada kimya kirefu kilichoambatana na kutafakari maelezo hayo, Bon alisema, "mtakumbuka tarehe 21 machi, siku ambayo yalitokea mauaji ya kikatili katika kitongoji cha Langa. Siku mbili baadaye niliweza kujipenyeza na kuingia Afrika kusini. Wakati huo wazalendo walikua wamepamba moto wakiwaua polisi wa kiafrika waliomo katika jeshi la polisi makaburu. Mimi na watu wetu walio ndani ya Afrika kusini tuliweza kumpata mmoja wa polisi weusi aliyekuwa anakimbia. Kabla wazalendo hawajamfikia sisi tulimkimbiza na kumshika. Lakini tulimfanya asituogope kwani tulimridhisha na akaamini tulikua upande wake. Tulimchukua na kumficha.

"Tulipomwuliza maswali alitwambia kuwa watu weusi walikuwa hawajui kwamba Makaburu walikuwa hawawezekani. Kwamba weupe walishaamua kuua weusi bila kujali mpaka ghasia ikome kabisa. Vile vile nchi zote zinazosaidia wapigania uhuru zitakiona cha mtema kuni  kwani sasa hivi makaburu walo jeshi liitwalo Gongo la chuma'ambalo halijawahi kutokea duniani. Sasa hivi jeshi hilo lipo tayari kufagia aina yeyote  ya upinzani baada ya kutayarishwa kwa muda wa miaka kumi. Nakumbuka niliporudi nilileta ripoti hii. Sasa ukilinganisha ripoti yangu na maelezo aliyotoa mkurugenzi sasa hivi ni dhahiri kwamba yanaoana. Hii inaonyesha ni kwamba ni kweli Makaburu wanao mpango huo."

"Hata mimi naafiki kuwa yaliyosemwa ni kweli," alisema mkuu wa upelelezi wa wapigania uhuru. "Lakini kitu ambacho ni lazima kukiweka maanani ni hicho kipigo wanachotishia watakifanya. Je kipigo hicho kitafanywa wapi; lini na kwa namna ipi?"

Hapo mkurugenzi wa upelelezi wa Zimbabwe aliinua kichwa akasema, Hata mimi jambo hilo ndilo linalonipa wasiwasi maana kutokana na maneno ya jasusi tuliyemteka, nchi zetu zitaanza kushambuliwa mara tu baada ya kipigo hicho. Huenda wanataka kutupumbaza ili watushambulie wakati sisi tunasubiri watoe kipigo kwa wapigania uhuru  kwanza . Hata hivyo ni lazima tupate ufumbuzi wa suala hili."

"Mnajua kwamba sasa hivi makaburu wana wasiwasi mkubwa na wanatuogopa. Hivyo sasa hivi hawana njia yeyote ile bali kutafuta njia za kututeketeza. Uchumi wao umeanguka. Hivi juzi juzi tu wafanyabiashara wa Uingereza waliitisha mkutano huko mjini Leeds na kuwataka wafanya biashara wa Afrika Kusini wajaribu kutetea haki za wafanyakazi weusi. Waliwataka pia waibane Serikali yao ili iwaruhusu weusi kufanya biashara kwenye sehemu wanazoishi weupe. Vile vile waliwataka wapinge vikali siasa ya kibaguzi ili Waingereza waendelee kupeleka rasilimali zao huko Afrika kusini. Hivyo makaburu wamehaha kwani msimamo huo umewauma sana. Ni kama mjuavyo, mtu anayehaha anaweza kufanya jambo lolote. Hatuna budi kuwa macho kabisa kwani hali hii imewafanya makaburu kujizatiti. Sasa hivi wamebanwa sana ndani na nje".

"Nilikuwa nikifikiri sana sasa hivi", Bon alianza kusema na hapo hapo wale Wakuu wawili wakageuka kumsikiliza yeye. Walikuwa wanajuwa kuwa Bon alikuwa kijana mwenye akili sana na ubongo wake ulifanya kazi kama komputa. Kila lilipotokea tatizo, Bon aliweza kutoa ufumbuzi sahihi. Ndio sababu alihusishwa katika mikutano ya ngazi za juu kama huu.

"Mnajuwa kuwa mwezi ujao kutafanyika mkutano wa pekee wa wapigania uhuru wote wa Afrika Kusini huko Tanzania, baada ya ule uliofanyika mwaka 1969. Kuna uwezekano kwamba Makaburu wameshapata habari na wanajitayarisha kutushambulia huko. Maana kama wakiweza kutekeleza tishio lao hilo la kipigo, wakateketeza wajumbe wote kwenye mkutano huo. Basi hivyo wanavyojigamba itakuwa ni sahihi kabisa. Viongozi wetu wote kutoka sehemu mbalimbali duniani watakuwapo pamoja na watu wale wanaotuunga mkono".

Wakuu wale walimwangalia Bon na kumsikiliza kwa makini.

"Bila hata kuzungumza zaidi, nafikiri Bon amesema ukweli kabisa", Mkurugenzi alisema huku akikiri rohoni kuwa kweli Bon alikuwa kijana mwenye akili za kuzaliwa. "Hata mimi nafikiri hilo ndilo jawabu lake, asante sana Bon. Lakini kuna jambo moja, Tanzania iko mbali sana. Sijui watatumia mbinu gani?", aliuliza Mkuu wa Idara ya Upelelezi huku akiwaangalia wale wajumbe wawili.

Akidakia haraka kujibu swali hilo, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Zimbabwe alisema, "Usiwachezee hawa Makaburu. Wanao uwezo wa kufanya jambo lolote. Wako mbali na Tanzania ndio, lakini wakijigamba ujuwe wanao mpango madhubuti. Hivyo ni juu yetu kujiweka tayari kutekeleza jukumu letu".

"Jibu tumeshalipata", alipaza sauti Mkuu wa Idara ya Upelelezi. "Hakuna haja ya kuhangaisha vichwa vyetu zaidi. Lililobaki ni kwamba mimi nitaitisha mkutano wa wenzangu niwaeleze tuliyogundua. Halafu tuzungumzie nini la kufanya kabla ya mkutano huo kuanza. Makaburu wasije wakatuchezea kama watoto wadogo".

"Hata mimi nafikiri hilo ndilo wazo la busara wazee wenzangu. Tusipochukua hatua za tahadhari tutaadhirika." Bon alijibu huku akili yake ikiwa mbali kwani alishachekecha akilini mwake na kuona jinsi jukumu hili lilivyokuwa gumu na la hatari sana.

"Yote niachie mimi alirukia mkuu wa idara ya upelelezi. Leo hii nitaitisha mkutano ili mpango yote ya tahadhari ikamilike. Ahsanteni sana. Mimi nitawajulisha kila hatua ambayo tutafikia. Nitawapa habari zote kuhusu matokeo ya mkutano. Bon usiondoke hapa mjini. Kila wakati nataka kujua mahali utakapokuwa. Ninaweza kukuhitaji ghafla. Kuhusu wewe ndugu mkurugenzi, mimi nitakujulisha tarehe ya mkutano hapo baadaye kwani ni lazima uwepo."

Mkutano ulifungwa na watu watatu hao wakaagana

# SURA YA PILI

## NAIROBI

Mike Maina aliingia ofisini kwa mkubwa wake wa kazi akiwa ameshika jalada mkononi. Maina alikuwa ofisa upelelezi katika idara ya upelelezi nchini kenya. Kijana huyu alikuwa anategemewa sana na serikali ya Kenya kwa kazi yake kubwa ya kulinda usalama dhidi ya hujuma za kisiasa, kijeshi na kiuchumi. Alikwisha tokomeza mipango mingi dhidi ya serikali.

"Ehe, hebu nieleze Maina ." Mkurugenzi wa upelelezi alisema, "Ingawa nimeitwa huko Ikulu, afadhali tuzungumze kwanza ndiyo nielekee huko baadaye."

Katika kumkumbusha mkubwa wake wa kazi, Mike alitasua midomo yake na kusema, "Unakumbuka mwaka 1981 wakati mamluki, wakiongozwa na Michael Hoare, walipojaribu kuiangusha serikali ya visiwa vya Shelisheli; halafu wakashindwa?"

"Ndivyo, kwani vipi? Wanataka kuishambulia Shelisheli tena?"

"Hapana. Unakumbuka serikali ya Shelisheli iliilaumu serikali ya Kenya kwa kuhusika; na serikali yetu ikakanusha vikali madai hayo? Unakumbuka serikali hata hivyo, ilituamuru tuchunguze suala hilo. Unakumbuka kuwa mimi ulinipa kazi hiyo?".

"Nakumbuka sana, mike."

Ripoti yangu ilionyesha kwamba, ingawa serikali haikuhusika, kuna watu binafsi au hata wakazi tu waliohusika. Kutokana na ushahidi tulioupata watu wengine wenye heshima wamepoteza kazi zao. Wakazi wengine hata wamefukuzwa nchini."

"Nakumbuka."

"Wakati wa upelelezi wetu kuna mtu ambaye tulimshuku sana. Lakini kutokana na kukosa ushahidi thabiti, hakuchukuliwa hatua. Hata hivyo jalada lake lilibaki wazi. Niliweka kijana kuchunguza mienendo yake. Vile vile nilikuwa nimemwagiza achimbe historia ya maisha yake toka kuzaliwa kwake mpaka hivi leo. Mtu huyu anaitwa Peter Gerrit. Yeye ni mfanya biashara. Anayo kampuni ya kuhudumia watalii ijulikanayo kama Kinyonga Tours and Safaris."

"Lo, jina lenyewe linasisimua," alisema kwa mzaha mkurugenzi.

"Sasa jana huyu kijana wetu alinileteа ripoti ambayo ilinifanya niwe na wasiwasi mkubwa kiasi kwamba lazima nikueleze. Kwa muda wote huu kijana wetu alikuwa anampeleleza mtu huyu."

"Mtu huyu anajulikana katika idara ya uhamiaji kama Mjerumani. Vile vile Idara ya uhamiaji inayo taarifa kwamba biashara hii ya kuhudumia watalii aliianza huko huko Ujerumani. Baadae aliamua kuja kuianzisha hapa nchini Kenya. Hayo tu ndiyo wanayoyafahamu maafisa wa Uhamiaji. Lakini sisi kitu kinachotugutua ni kwamba siku ambayo askari wa kukodiwa walipovamia Visiwa vya Shelisheli, huyu Peter alikuwapo. Na wakati askari hao walipowasili kwenye uwanja wa ndege wa Victoria. Maana ripoti inasema Peter alikuwa uwanjani hapo. Ni baada tu ya kugutushwa na mapigano yaliyotokea pale wakati Peter alipojisalimisha kwa majeshi ya usalama ya shelisheli.

"Wakati wa kuhojiwa Peter alieleza kwamba alikuwa hapo uwanjani kusindikiza rafiki zake waliokuwa kwenye ndege ya shirika la ndege la India ambayo ilitekwa nyara. Askari wa Shelisheli walipoangalia pasipoti yake na kuona kuwa yeye ni mkazi wa Kenya na mfayabiashara ya utalii walimwachia mara moja. Wakati wa uchunguzi wetu tulipata fununu kuwa huyu Peter alikuwa kwenye uwanja wa ndege kwa nia ya kuwapokea askari wa kukodiwa. Lakini kwa kuwa tulikosa ushahidi wa kutosha, hatukuweza kumchukulia hatua, bali tulibaki tunamtuhumu tu. Wewe unajua tena jinsi mahakama zetu pamoja na serikali vinavyotaka haki itekelezwe. Heri kumwachia huru mhalifu kuliko kumwadhibu yule asiye na hatia.

"Sasa katika uchunguzi uliofanywa na kijana huyu kwa muda wa miaka yote hii. umegundua mambo yenye kututia wasiwasi. Kwanza kijana wetu amegundua kwamba Peter hakuzaliwa Ujerumani, bali yeye ni mzaliwa wa Afrika kusini. Ila mjomba wake alikuwa anaishi Ujerumani. Ndiye huyo huyo aliyemchukua Peter na kumpeleka huko. Aliishi na kukulia huko ambako alipata masomo. Alipofikia umri wa miaka ishirini alirudi Afrika kusini katika mji wa kwao wa Pietermaritzburg.  Inasemekana aliisha fanya kazi kwa Michael Hoare kama askari wa kukodiwa. Baada ya hapo alipotea na kisha akaibuka huko Ujerumani. Wakati huo mjomba wake alikuwa ameanzisha kampuni ya kuhudumia watalii ambayo alijiunga nayo. Baada ya muda kitambo, ndipo akaja Kenya. Sasa unaweza kuona kuwa kuwako kwake Shelisheli hakukuwa kwa bahati tu ila kwa sababu maalumu.

"Zaidi ya hayo, kijana wetu amegundua kitu ambacho kimetia wasiwasi na pia kunifanya mimi nifanye hima . Nikwamba kwa muda wa majuma mawili sasa

kumekuwa kunakuja wazungu wanaume wawili wawili kila baada ya siku tatu. Wazungu hao wanakwenda nyumbani kwa Peter huko Red hill kwenye njia ya kwenda Limuru. Kijana wetu anahisi kwamba baada ya hao wazungu kuingia nyumbani hawatoki nje tena. Wako kama watu sita sasa. Unajua kuwa analo shamba kubwa na pia nyumba kubwa. Katika shaba hilo kuna nyumba za wafanyakazi. Sasa tunajiuliza hivi: kama kweli hawa ni wageni wa kawaida, kwa nini hawaonekani angalau kutembea tembea au hata kwenda mjini? kwa nini wasithubutu hata kuzurura hapo kwenye shamba?"

"Huenda wanatembea usiku," alipendekeza mkurugenzi.

"Kama kweli ni usiku, kwa nini usiku? aliuliza Mike.

"Nafikiri unayo sababu nzuri ya kuwa na wasiwasi. Kufuatana na maelezo yako inabidi mtu huyu apelelezwe kikamilifu zaidi kwani huenda akawa na jambo. Bali kama mtu huyu anayo mahusiano na serikali ya makaburu, yafaa apelelezwe kwa uangalifu na tahadhari zaidi. Akigundua kuwa anachunguzwa si ajabu akateleza tena kama alivyofanya hapo kwanza. Hivyo, kwa baraka zangu, nakuruhusu uendelee na kazi ya kumpeleleza ili tujuwe hasa anapanga kufanya kitu gani. Umesema kuwa kipindi fulani alikuwa haonekani na haikujulikana alikuwa wapi. Basi ni dhahili kuwa anaweza kuwa jasusi wa makaburu ambaye alikuwa mafunzoni. Hapa inawezekana kaja kikazi, kwa hiyo chunga sana mtu huyu kwani anaweza kuwa hatari|".

"Asante. Nitafanya hivyo na kisha nitakujulisha maendeleo ya kila siku".

Mike Maina alichukuwa jalada na kutoka nje ya ofisi ya mkubwa wake.

Mike alipofika ofisini kwake alimwambia Katibu Muhitasi wake amuite kijana Mwaura. Kwa muda wa miaka yote hii Mwaura ndiye alikuwa akimpeleleza Peter.

"Mwaura", Mike alisema mara Mwaura alipoingia ofisini kwake. "Nimezungumza na Mzee na tumekubaliana kwamba tuendelee na upelelezi wetu. Sasa nitakuongezea vijana wengine na ninataka ripoti juu ya maendeleo yote ya mtu huyu, kila kitu atakachofanya, na mahali atakapokwenda".

"Nashukru sana, Bosi". Mwaura alijibu. "Nafikiri ukinipa vijana wawili, kama vile Onyango na Kipukoachi, kazi itafanyika vizuri".

"Maombi yako yatatimizwa mara moja, unafanya kazi nzuri Mwaura. Kuna haja ya idara kufikiria kuongeza maslahi yako".

"Asante sana, Bosi, kazi kwanza".

"Ningependa kazi hii ianze mara moja leo hii na mhakikishe kwamba Peter hapati mwanya wa kufanya jambo lolote dhidi yetu", alisema Mike.

"Kitu ambacho nimekosea bosi ni kwamba tangu asubuhi sikuweka mtu wa kuendelea na uchunguzi juu ya maendeleo ya mtu huyu. Katika muda huu wa masaa tisa huende amefanya majambo", Mwaura alijilaumu.

"Tusililie maji yaliyomwagika. Kuanzia sasa hivi fanya kazi kama kawaida".

Wakati Mike anazungumza na Mkurugenzi wa Upelelezi, ofisini mwa Peter Gerrit, katika mtaa wa Koinange, ambako ndiko yaliko Makao ya Kinyonga Tours and Safaris, simu ya siri ilikuwa ikilia. Simu hii ilikuwa inajulikana na watu wachache sana. Kila simu ilipokuwa inalia moyo wa Peter ulishtuka kidogo.

"Hallo, Peter hapa,"Peter alisema mara baada ya kuunyakua mkono wa simu na kuupachika katika sikio lake la kulia.

"Masoga hapa," upande mwingine wa simu ulimwitikia.

Masoga alikuwa ni afisa mwingine katika kurugenzi ya upelelezi. Lakini alikuwa kwenye orodha ya kulipwa na Peter Gerrit. Masoga alikuwa ni msaliti wa serikali ya wananchi wa Kenya kwa sababu ya tamaa ya pesa. Hivyo alikuwa anampa habari muhimu sana Peter ambazo alikuwa anzitumia dhidi ya wanamapinduzi wa Afrika.

Wajati Mwaura alipokuwa anamweleza Mike asubuhi ile jinsi alivyokuwa na wasiwasi juu ya wageni waliokuwa wakiingia nyumbani kwa Peter, Masoga alikuwa amepitia ofisini kwa Mike akiomba ruhusa kwenda nje. Na kwa vile hawakuwa na wasiwasi nae, Mwaura aliendelea kueleza wasiwasi wake kuhusu Peter Gerrit na wageni wake. Ndipo Mike aligeuka na kutaka kujuwa Masoga alikuwa na shida gani. Lakini Masoga alikuwa amesikia sehemu ya mwisho ya taarifa ya Mwaura juu ya wazungu walikuwa wakienda kwa Peter.

"Ehee, kuna nini?. Peter aliuliza kwa sauti kali.

Masoga alikuwa anapiga simu kwenye kibanda cha posta kando ya posta kuu, alisema, "Kuna habari ofisini kwetu kuwa unao wageni nyumbani kwako ambao wanaingia tu lakini hawatoki, idara yetu inao wasiwasi, vipi?".

Bila kujua umuhimu wa habari alizokuwa akizitoa kwa Peter, Masoga alitabasamu.

"Wana wazimu! naona sasa idara yenu haina kazi ya kufanya. Mimi sina wageni wa namna hiyo. Kama wana wasiwasi, kwanini wasije kuona?". Hivi ni nani anasema maneno hayo?", Peter aliuliza kana kwamba hajali kitu ingawa kwa kweli moyo wake ulikuwa ukidunda vibaya kwa hofu aliyokuwa nayo.

"Kijana mmoja anayeitwa Mwaura".

"Acha nae". Peter alimjibu. "Huenda anapalilia cheo".

"Huenda. Lakini mimi niliona ni vizuri kukwambia.

"Hivyo ni sawa. Lakini hakuna chochote wala usiwe na wasiwasi. Hata hivyo, asante. Njoo umuone Kanabhai. Utakuta anayo bahasha yako.

"Asante", alijibu Masoga huku anasikia raha alipojuwa kuna bahasha yake.

Baada ya Peter kuweka simu chini, alianza kufikiri. Alikuwa ameshangazwa na habari hizi kwani hakutarajia kabisa kuwa idara ya upelelezi ya Kenya ilikuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa kiwango cha juu kiasi hicho. Ni kweli kwamba Peter alikuwa na makomandoo maarufu kumi na wawili nyumbani kwake kutoka kwenye jeshi hatari la makaburu liitwalo KULFUT. Watu hawa walikuwa wameingia nchini Kenya kwa siri na ni yeye aliyetayarisha mpango huo. walikuwa wameingia nchini Kenya kupitia Mombasa. Walisafiri kwa mashua mpaka kwenye Bandari ya Mombasa baada ya kushushwa katika Bahari ya Hindi kutoka kwenye Meli moja ya makaburu walikuwa wamefika kwenye ufuko wa Nyali walipojifanya wao ni watalii waliokuwa wakicheza tu na mashua. Peter alikuwa ametayarisha kila kitu.

Akitumia wadhifa wake kama mfanyabiashara wa kuhudumia watalii, aliweza kuwasafirisha. Awamu kwa awamu, hadi Nairobi. Aliamua kutowasafirisha kwa mkupuo ili asije kugutukiwa. Hivyo watu hawa walikuwa nchini Kenya kinyume cha sheria. Idadi yao ya watu kumi na wawili kuwa yenye nguvu sawa na kikosi kizima cha jeshi. Vile vile walikuwa wamepewa mafunzo ya kila aina kuhusu kuua. Wawili kati ya hao walikuwa NINJA. Ninja ni mtu aliyehitimu mafunzo ya pekee ya karate na kung fu huko Ujapani na Korea. Kuelezea ninja kwa kirefu inaweza kuchukua siku nzima. Hivyo ridhika na ukweli huu kwamba ninja anakuwa amejifunza zaidi ya njia elfu moja za kuua. Mtu mmoja anaweza akakiangusha kikosi kizima. Ni watu wachache katika ulimwengu huu ambao wamehitimu mafunzo hayo. Askari jeshi mia moja na silaha zao hawawezi kufua dafu kwa ninja mmoja.

Makomando hawa wa makaburu walikuwa bado kufika mwisho wa safari yao. Walikuwa wanaelekea Tanzania. Hivyo kama wangegutukiwa bado wakingali Kenya, Peter angepata matatizo makubwa kutoka kwa wafadhili wake. Hivyo ilibidi abadili mpango haraka ili aweze kuingia Tanzania ambako ndiko walikuwa wakafanye kazi. Peter aliendelea kujifikiria yeye mwenyewe. Yeye pia alikuwa ni komando katika jeshi la KULFUT kwenye kikosi cha ujasusi. Alikuwa amehitimu kila aina ya mafunzo ya upiganaji na ujasusi. Alikuwa ameletwa Kenya kusubiri wakati wake wa kufanya kazi. Alikuwa tayari kufanya kazi wakati wowote alipohitajiwa na wakubwa wake. Na wakati huo sasa ulikuwa umewadia. Wakubwa zake Peter walikuwa wameamua kufanya kazi sehemu hii ya Afrika mashariki.

Kila wakati alipofikiria mpango huu na utekelezaji wake, Peter alisisimkwa na damu. Alikuwa amefikiri sana juu ya siasa za nchi huru za afrika na kuona vyema kuzitokomeza ili Afrika kusini iweze kulitawala bara zima la Afrika. Aliamini kabisa kwamba mtu mweusi hakuwa na haki ya kujitawala. Mtu mweusi alipaswa kuwa mtumwa wa wazungu. Kwake Peter mtu mweusi alikuwa kama paka au kwani hata mbwa anayo thamani. Mara nyingine alishangaa aliposikia mtu mweusi anazungumza neno la busara. Kwake yeye kama makaburu na pia kufuatana na walivyofunzwa na kulelewa, aliona mtu mweusi kama kitu kisichokuwa na thamani yoyote. Kwa sababu hiyo Peter alisisimkwa damu alipofikiri kuwa yeye mwenyewe angeshiriki kuwaangamiza watu weusi katika nchi zao ambazo walidai ni huru.

Ili mipango yake isije ikaharibika, Peter aliinua simu akazungusha namba kazaa, kisha kusubiri kuitikiwa.

"Hallo, hapo ni Arusha ?" Peter aliuliza baada ya kuitikiwa.

"Ndiyo. Habari gani, P. G.?"

"Nzuri, F. K."

"Mipango imebadilika. Tungoje mpakani saa mbili usiku. Naamini mipango yote iko shwari mpakani."

"Nimeisha suka kila mpango kama tulivyozungumza. Hakuna tabu kamwe."

"Ahsante F. K."

"Ahsante P G."

F. K

"Nyoka Tours and Safaris," Tondo aliitika kwenye simu.

"Njoo nyumbani haraka." Tondo alisikia sauti ya tajiri wake ikimwamrisha.

"Sawa mzee," aliitika kwa unyenyekevu.

Tondo aliweka simu chini na kuinuka. Bila hata kuaga alielekea kwenye gari lake ili aende kwa tajiri yake. Alipoangalia saa yake aliona inaonyesha saa nane na nusu mchana.

Chris Tondo alikuwa meneja mkuu wa kampuni ya Nyoka tours and Safaris ya mjini Arusha ambayo ilikuwa ni mali ya Mhindi mmoja. Mhindi huyo alikuwa anajulikana kwa jina la Firozali Kassam na watu wengi walimwita F. K. Yeye alikuwa tajiri sana. Alikuwa akiishi sehemu ya Them Hill ambako alijenga nyumba kubwa sana ambayo mashabiki waliita "White House" au Ikulu ya Arusha.

F. K alipendwa sana na wakazi wa Arusha kutokana na tabia yake ya kuwasaidia watu wenye uwezo mdogo wa kipesa. Alikuwa mtu mkarimu sana. Inasemekana nusu ya teksi zote za Arusha zilinunuliwa na wenyewe kwa mkopo usio na riba kutoka kwa F. K. Inasemekana kuwa alifuta madeni mengi ya watu walioonekana hawana uwezo wa kulipa. Ingawa hakuwa muumini wa dini ya kikristo, F. K alisaidia kujenga makanisa mengi ya madhehebu mbalimbali mjini Arusha.

Kwa muda mrefu F.K alikuwa mstari wa mbele katika kusaidia Chama na serikali katika mkoa huo, kufanya shughuli zake nyingi. Inasemekana. Kwa mfano alichanga pesa nyingi kwa ajili ya ujenzi wa makao makuu ya chama cha mkoa. Hivyo alipewa heshima kubwa sana na wakuu wa chama na serikali hapo mkoani Arusha. Kusema kweli kama angetokea mtu akasema kwamba F.K alikuwa ni mtu mbaya, basi angeuawa kwa kupigwa mawe hadhalani.

F.K alijulikana kama mtu wa watu, raia mwema na mpenzi wa watu wa rika zote. Alikuwa mtu maarufu na murua. Watu wote walimwelewa hivyo. Sifa zake zilizidi kuvuma kwani F. K alikuwa mfadhili, asiyebagua mtu awe mweupe au mweusi, masikini, fukala au tajiri. Watu wote mbele ya F.K walijiona sawa. Huo ulikuwa upande mmoja tu wa F.K.

Lakini F.K alikuwa na upande mwingine ambao ni watu wachache sana walioujuwa. Hata mtu kama Chris Tondo nae alimjuwa F.K juu juu tu.

F.K alikuwa mzaliwa wa Dar es Salaam, Tanzania, baba yake alikuwa mfanyabiashara maarufu sana Jijini Dar es Salaam, alikuwa na maduka makubwa matatu ya vipuri vya magari na alikuwa wakala wa makampuni mengi ya nchi za nje hapa Tanzania. Hivyo huyo mzee Kassam alikuwa tajiri sana. F.K alizaliwa mnamo mwaka 1945. Baada ya kusoma shule ya msingi hapo nchini, baba yake alimpeleka Uingereza ambako alipata elimu ya sekondari na chuo kikuu. Hii ilitokana na kwamba baba yake alikuwa na uwezo wa kumlipia F.K ada ya shule.

Mnamo mwaka 1967 serikali ya Tanzania ilitaifisha makampuni makubwa ya watu binafsi na kuyaweka katika mikono ya wananchi. Hatua hiyo ilifuatia kutangazwa kwa siasa za ujamaa na kujitegemea katika Azimio la Arusha. Mnamo mwaka 1972 serikali ilichukuwa hatua nyingine zaidi. Majumba makubwa ya watu binafsi yaliyaifishwa vilevile.

Wakati huo F.K alikuwa anasoma chuo kikuu huko Uingereza. Baba yake alimpigia simu na kumweleza mkasa uliokuwa umewapata nyumbani. Alimfahamisha kuwa nyumba zao therathini ambazo walikuwa wamejenga na nyingine kununua vile vile zilikuwa zimetaifishwa. Aliposikia vile F.K alipatwa na wazimu. Aliilaani serikali kiasi ambacho hajapata kusikia.

Siku hiyo jioni aliendа kwenye baa na kuchapa mtindi barabara. Mara alisikika akiapa, "Naapa kwa jina la Mungu, kuna siku nitalipiza kisasi dhidi ya serikali ya Tanzania", Kwa bahati mbaya au nzuri katika baa ile kulikuwemo jasusi mmoja kutoka Afrika Kusini lililokuwa kwenye shughuri zake lenyewe. Liliposikia hivyo lilikumbuka kuwa shirika la ujasusi la Afrika Kusini lilikuwa linamtafuta mtu raia wa Tanzania ambaye angelifanyia kazi ya kijasusi huko.

Hivyo ndivyo alivyopatikana F.K na kuwekwa katika orodha ya kulipwa na shirika la ujasusi la Afrika Kusini. Pamoja na kulipwa ili afanye kazi ya ujasusi, F.K aliahidiwa kuwa angepewa msaada kulipiza kisasi dhidi ya serikali ya Tanzania. Inasemekana kuwa baadae alipotea kwa muda wa miaka mitatu na haikujulikana mahali alipokuwa. Lakini habari zilisema kuwa alikuwa huko Afrika Kusini akipewa mafunzo ya kijasusi kwenye makambi mbali mbali.

Aliporudi Tanzania alikuta wazazi wake wako kwenye pilikapilika za kuhama na kwenda Canada F.K alikataa kuondoka na wazazi wake na kusema kwamba yeye alikuwa mzaliwa wa Tanzania hivyo hakuwa na sababu ya kuihama nchi yake na kwenda nchi nyingine. Hivyo familia yake ilimugawia sehemu ya mali iliyobaki naye akaamua kuhamia mjini Arusha. Huko ndiko alikoanzisha kampuni yake ya kuhudumia watalii iliyojulikana kwa jina la nyoka tours and safaris.

Alichagua jina hilo kwa sababu alizozijua mwenyewe. Mabwana zake walimpa fedha nyingi ambazo alizitumia kufanya mambo niliyoyaeleza na pia kujenga White house. Kutokana na utajiri wake F.K aliweza kuisaliti nchi bila mtu yeyote kumshuku. Fedha zake ziliwafumba watu macho. Nyumba hiyo iliyoitwa White House ilikuwa imejengwa kwa aina yake. Ilikuwa imejengwa kwa shabaha ya kufanya ujasusi. Nyumba hiyo ilikuwa na vyumba vingine chini ya ardhi. Kulikuwa na barabara kadhaa chini kwa chini ambazo zilitokea nje ya sengenge ilizunguka ekali kumi na mbili za kiwanja cha nyumba hiyo.

F.K alikuwa hajaowa wala kuwa na watoto. Hivyo aliishi katika nyumba hii peke yake. Watumishi wake waliishi kwenye nyumba kando kando ya jumba lake. Kwa muda wote huo F.K alifanikiwa kujenga kwa nje, akaonekana kama mbwa mwitu aliyevaa ngozi ya kondoo. Alionekana mzuri kwa nje lakini alikuwa hatari kwa ndani.

Dhamila yake kubwa ilikuwa ni kulipiza kisasi. Kwa kufanya hivyo F.K angekuwa amefanya kazi katika upande wa adui namba moja wa Afrika huru na Ulimwengu mzima kwa ujumla. Hii ndiyo ilikuwa upande wa pili wa F.K ambayo ilikuwa sura yake halisi.

Chris Tondo ambaye sasa alikuwa anaelekea Themi Hill ndiye aliyejuwa F.K hakuwa mtu mzuri kama watu wengine wa mjini Arusha walivyoamini. Yeye Tondo walikuwa wakionana na kufahamiana kiajabu. Tondo alikuwa na umri karibu sawa na F.K. Walionana mara tu baada ya Tondo kustaafishwa kutoka Jeshi la Polisi kwa manufaa ya umma. Alikuwa tayari amefikia cheo cha Kamishna Msaidizi, akiwa kati ya waafrika wa kwanza kufikia ngazi hiyo. Tondo alichukulia kustaafishwa kwake kama kitendo cha fitina na hivyo alikuwa na chiki dhidi ya serikali. Aliamini kuwa alionewa wivu kwani alikuwa na nafasi nzuri ya kuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi.

Hata hivyo, ukweli ni kwamba huyu Chris Tondo alikuwa akitumia cheo chake kusaidia wahujumu uchumi. Aliwasaidia kutorosha vipusa vyote vya thamani kwa njia ya magendo. Alipostaafishwa jina lake lilitolewa kwenye magazeti ya kila siku. Kwa njia hiyo F.K ambaye alishaambiwa habari za Tondo na wale wahujumu aliowasaidia, alijuwa kuwa amepata mtu aliyekuwa akimuhitaji. F.K alijuwa Tondo hakuwa mwaminifu kwa serikali. Vile vile alishakuwa mtu mkubwa na hivyo mwenye uzito katika jeshi la polisi. Huyu ndiye mtu aliyefaa katika mpango wake waliokuwa nao F.K pamoja na wafadhili wake.

# SURA YA TATU

**SIKU** moja F.K alimfuata Tondo Jijini Dar es Salaam. Alimdanganya kwamba kuna mtu amemwelekeza kwake. Alimwambia kuwa kama ingewezekana alipenda wafanye kazi pamoja kwa kuwa hakuwa na kazi. Bila kusita Tondo alikubali akaona ni bahati iliyoje. Siku hiyo Chris Tondo alimweleza jinsi alivyoichukia serikali ya Tanzania akidaiwa kuwa ilimstaafisha bila sababu ya msingi.

"Wewe tulia tu, kuna siku mtu atalipa", F.K alimhakikishia.

Baada ya kusikia maelezo ya Tondo, F.K alijuwa amempata mtu aliyekuwa akimtafuta. Tondo aliteuliwa kuwa Meneja Mkuu wa Nyoka Tours and Safaris. Kusema kweli kampuni hiyo ilikuwa ni kisingizio. Mambo ambayo F.K na Tondo walifanya kwa siri katika kuhujumu uchumi aliyejuwa ni Mungu peke yake.

Tondo alisimama na kuegesha gari nyumbani kwa F.K. F.K alifungua mlango na kumkaribisha ndani Tondo.

"Karibu ndani.

"Asante", alijibu Tondo.

"Nimekuita ghafla kwa sababu nimepata habari sasa hivi kutoka kwa yule rafiki yangu wa Nairobi kwamba wale wageni waliokuwa wafike kesho wataingia leo jioni. Kitu ninachotaka ufanye ni kwenda kubadiri mipango huko mpakani. Kama nilivyokuwa nimekueleza awali, watu hawa wataingia bila kupitia sehemu za kawaida. Wageni hao wanayo mizigo ambayo sitaki ikaguliwe wala wao wasionekane na mtu yeyote", alieleza F.K na kisha akaelekea kwenye chumba fulani. Aliporudi alikuwa amebeba pasipoti kumi na mbili na bahasha moja.

"Pasipoti hizi ni za hawa wageni. Nenda nazo huko mpakani kwa mtu wetu akugongee mihuri ya idara ya uhamiaji. Unajuwa ni siku nyingi hatujaangalia maslahi yake. Hivyo mpelekee hii bahasha yake".

F.K alimkabidhi Tondo hivyo vitu.

"Aidha nenda kwa Hasanali mwambia kuwa wale wageni watakwenda nyumbani kwake kwa kupitia njia ya porini mnamo saa mbili usiku. Mimi nitafika hapo kuwachukuwa mnamo saa mbili na nusu usiku, na yeey tuonane hapo. Kazi ifanyike kama kawaida Tondo".

"Sawa nitatekeleza yote kama ulivyosema".

Tondo alibeba mzigo wake akaelekea nje huku akisindikizwa na mwenyeji wake.

Wakati akielekea nyumbani kwake alifikiri kwamba wakati mwingine mambo waliyofanya yalikuwa ya ajabu kama sasa alishangaa alipoona F.K anazo pasipoti za watu ambao walikuwa bado kuingia nchini hata hivyo Tondo alijuwa haikuwa juu yake kuuliza maswali. kazi yake kubwa ilikuwa utekelezaji.

Tayari alikuwa amejenga nyumba tatu. Nyumba moja ilikuwa Dar es Salaam na aliipangisha kwa Ubalozi kwa elfu hamsini kwa mwezi. Nusu ya kodi hiyo Tondo alilipwa kwa fedha za kigeni. Nyumba nyingine alikuwa amejenga nyumbani kwao Njombe ambayo kwa viwango vya huko nyumba hiyo ilikuwa ya hali ya juu. Nyumba ya tatu ni hiyo aliyojenga Arusha. Tondo alikuwa hajawahi kuoa lakini alikuwa na watoto watatu aliowapata nje ya ndoa. Watoto wake wawili wakubwa walikuwa wanasoma shule ya msingi huko London, wakati yule mdogo alikuwa anakaa na mama yake huko Njombe.

"Tangu nistaafishwe na kuungana na F.K mafanikio yangu yamekuwa ya makubwa kuliko ya mtanzania wa hali ya juu. Kweli kazi hii inanifaa shauri yao watanikoma", Tondo alijisemea kimoyomoyo.

Mara alikutana na gari lilimumulika kwa taa zake. Kabla ya kupishana alitambua ni Nyaso, hivyo akapunga mkono, Nyaso naye akampungia mkono pia.

Nyaso alikuwa ni msichana mrembo sana. Hapakuwepo msichana mwingine mjini Arusha ambaye wangeweza kushindana naye kwa urembo. Nyaso alikuwa hawala yake F.K. Watu waliojuwa penzi lao walisema kuwa Nyaso alikuwa saizi ya F.K kutokana na utajiri wake. Bali tu walishindwa kufahamu kwanini hawakuoana. Hata hivyo rafiki zake na F.K ndoa ingekuwa kinyume cha mila za wahindi. Kwa kuamua kuishi na Nyaso kama hawala kulionyesha watu unafiki wa F.K na Wahindi wengine. Waliopenda kufanya mapenzi na waafirika lakini ilikuwa mwiko kuwaoa. Wahindi walitembea na wasichana wa Kiafrika na baadaye kuwatupa jalalani.

Kila wakati Tondo alipofikiria uhusiano wa watu hawa wawili aliona kuwa Nyaso hakumhitaji sana F.K. Alijuwa msichana yule alitaka pesa zake tu. Hii ilionyeswa na majibu ya mkato aliyompa F.K mara kwa mara. Lakini hata hivyo F.K alikuwa amemjengea Nyaso nyumba nzuri sana. Nyaso alikuwa haruhusiwi kwenda kwa F.K. Hivyo F.K alikuwa akienda kulala kwa Nyaso. Hata Tondo hakujuwa kwanini

F.K hakupenda Nyaso aende kwake bali alilidhika alipoambiwa na F.K kwamba hiyo ingekuwa kukiuka mila za Kihindi.

"Acha mtoto wa Kitanzania amule kidogo Mhindi huyu", Tondo alijisemea.

Aliegesha gari yake nyumbani kwake halafu akajitayarisha kwa safari ya kuelekea mpakani.

Wakati Mike anazungumza na Mkurugenzi wa Upelelezi, ofisini mwa Peter Gerrit, katika mtaa wa Koinange, ambako ndiko yaliko makao ya Kinyonga Tours and Safaris, simu ya siri ilikuwa ikilia. Simu hii ilikuwa inajulikana na watu wachache sana. Kila simu ilipokuwa inalia moyo wa Peter ulishtuka kidogo.

"Hallo, Peter hapa,"Peter alisema mara baada ya kuunyakua mkono wa simu na kuupachika katika sikio lake la kulia.

"Masoga hapa," upande mwingine wa simu ulimwitikia.

Masoga alikuwa ni afisa mwingine katika kurugenzi ya upelelezi. Lakini alikuwa kwenye orodha ya kulipwa na Peter Gerrit. Masoga alikuwa ni msaliti wa serikali ya wananchi wa Kenya kwa sababu ya tamaa ya pesa. Hivyo alikuwa anampa habari muhimu sana Peter ambazo alikuwa anzitumia dhidi ya wanamapinduzi wa Afrika.

Wajati Mwaura alipokuwa anamweleza Mike asubuhi ile jinsi alivyokuwa na wasiwasi juu ya wageni waliokuwa wakiingia nyumbani kwa Peter, Masoga alikuwa amepitia ofisini kwa Mike akiomba ruhusa kwenda nje. Na kwa vile hawakuwa na wasiwasi nae, Mwaura aliendelea kueleza wasiwasi wake kuhusu Peter Gerrit na wageni wake. Ndipo Mike aligeuka na kutaka kujuwa Masoga alikuwa na shida gani. Lakini Masoga alikuwa amesikia sehemu ya mwisho ya taarifa ya Mwaura juu ya wazungu walikuwa wakienda kwa Peter.

"Ehee, kuna nini?. Peter aliuliza kwa sauti kali.

Masoga alikuwa anapiga simu kwenye kibanda cha posta kando ya posta kuu, alisema, "Kuna habari ofisini kwetu kuwa unao wageni nyumbani kwako ambao wanaingia tu lakini hawatoki, idara yetu inao wasiwasi, vipi?".

Bila kujua umuhimu wa habari alizokuwa akizitoa kwa Peter, Masoga alitabasamu.

"Wana wazimu! naona sasa idara yenu haina kazi ya kufanya. Mimi sina wageni wa namna hiyo. Kama wana wasiwasi, kwanini wasije kuona?". Hivi ni nani

anasema maneno hayo?" Peter aliuliza kana kwamba hajali kitu ingawa kwa kweli moyo wake ulikuwa ukidunda vibaya kwa hofu aliyokuwa nayo.

"Kijana mmoja anayeitwa Mwaura".

"Acha nae". Peter alimjibu.

"Huenda anapalilia cheo".

"Huenda. Lakini mimi niliona ni vizuri kukwambia.

"Hivyo ni sawa. Lakini hakuna chochote wala usiwe na wasiwasi. Hata hivyo, asante. Njoo umuone Kanabhai. Utakuta anayo bahasha yako.

"Asante", alijibu Masoga huku anasikia raha alipojuwa kuna bahasha yake.

Baada ya Peter kuweka simu chini, alianza kufikiri. Alikuwa ameshangazwa na habari hizi kwani hakutarajia kabisa kuwa idara ya upelelezi ya Kenya ilikuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa kiwango cha juu kiasi hicho. Ni kweli kwamba Peter alikuwa na makomandoo maarufu kumi na wawili nyumbani kwake kutoka kwenye jeshi hatari la makaburu liitwalo KULFUT. Watu hawa walikuwa wameingia nchini Kenya kwa siri na ni yeye aliyetayarisha mpango huo. walikuwa wameingia nchini Kenya kupitia Mombasa. Walisafiri kwa mashua mpaka kwenye Bandari ya Mombasa baada ya kushushwa katika Bahari ya Hindi kutoka kwenye Meli moja ya makaburu walikuwa wamefika kwenye ufuko wa Nyali walipojifanya wao ni watalii waliokuwa wakicheza tu na mashua. Peter alikuwa ametayarisha kila kitu.

Akitumia wadhifa wake kama mfanyabiashara wa kuhudumia watalii, aliweza kuwasafirisha. Awamu kwa awamu, hadi Nairobi. Aliamua kutowasafirisha kwa mkupuo ili asije kugutukiwa. Hivyo watu hawa walikuwa nchini Kenya kinyume cha sheria. Idadi yao ya watu kumi na wawili kuwa yenye nguvu sawa na kikosi kizima cha jeshi. Vile vile walikuwa wamepewa mafunzo ya kila aina kuhusu kuua. Wawili kati ya hao walikuwa NINJA. Ninja ni mtu aliyehitimu mafunzo ya pekee ya karate na kung fu huko Ujapani na Korea. Kuelezea ninja kwa kirefu inaweza kuchukua siku nzima. Hivyo ridhika na ukweli huu kwamba ninja anakuwa amejifunza zaidi ya njia elfu moja za kuua. Mtu mmoja anaweza akakiangusha kikosi kizima. Ni watu wachache katika ulimwengu huu ambao wamehitimu mafunzo hayo. Askari jeshi mia moja na silaha zao hawawezi kufua dafu kwa ninja mmoja.

Makomando hawa wa makaburu walikuwa bado kufika mwisho wa safari yao. Walikuwa wanaelekea Tanzania. Hivyo kama wangegutukiwa bado wakingali Kenya, Peter angepata matatizo makubwa kutoka kwa wafadhili wake. Hivyo ilibidi abadili mpango haraka ili aweze kuingia Tanzania ambako ndiko walikuwa wakafanye kazi. Peter aliendelea kujifikiria yeye mwenyewe. Yeye pia alikuwa ni komando katika jeshi la KULFUT kwenye kikosi cha ujasusi. Alikuwa amehitimu kila aina ya mafunzo ya upiganaji na ujasusi. Alikuwa ameletwa Kenya kusubiri wakati wake wa kufanya kazi. Alikuwa tayari kufanya kazi wakati wowote alipohitajiwa na wakubwa wake. Na wakati huo sasa ulikuwa umewadia. Wakubwa zake Peter walikuwa wameamua kufanya kazi sehemu hii ya Afrika mashariki.

Kila wakati alipofikiria mpango huu na utekelezaji wake, Peter alisisimkwa na damu. Alikuwa amefikiri sana juu ya siasa za nchi huru za afrika na kuona vyema kuzitokomeza ili Afrika kusini iweze kulitawala bara zima la Afrika. Aliamini kabisa kwamba mtu mweusi hakuwa na haki ya kujitawala. Mtu mweusi alipaswa kuwa mtumwa wa wazungu. Kwake Peter mtu mweusi alikuwa kama paka au kwani hata mbwa anayo thamani. Mara nyingine alishangaa aliposikia mtu mweusi anazungumza neno la busara. Kwake yeye kama makaburu na pia kufuatana na walivyofunzwa na kulelewa, aliona mtu mweusi kama kitu kisichokuwa na thamani yoyote. Kwa sababu hiyo Peter alisisimkwa damu alipofikiri kuwa yeye mwenyewe angeshiriki kuwaangamiza watu weusi katika nchi zao ambazo walidai ni huru.

Ili mipango yake isije ikaharibika, Peter aliinua simu akazungusha namba kazaa, kisha kusubiri kuitikiwa.

"Hallo, hapo ni Arusha ?" Peter aliuliza baada ya kuitikiwa.

"Ndiyo. Habari gani, P. G.?"

"Nzuri, F. K."

"Mipango imebadilika. Tungoje mpakani saa mbili usiku. Naamini mipango yote iko shwari mpakani."

"Nimeisha suka kila mpango kama tulivyozungumza. Hakuna tabu kamwe."

"Ahsante F. K."

"Ahsante P G."

"Nyoka Tours and Safaris," Tondo aliitika kwenye simu.

"Njoo nyumbani haraka." Tondo alisikia sauti ya tajiri wake ikimwamrisha.

"Sawa mzee," aliitika kwa unyenyekevu.

Tondo aliweka simu chini na kuinuka. Bila hata kuaga alielekea kwenye gari lake ili aende kwa tajiri yake. Alipoangalia saa yake aliona inaonyesha saa nane na nusu mchana.

*****

Chris Tondo alikuwa meneja mkuu wa kampuni ya Nyoka Tours and Safaris ya mjini Arusha ambayo ilikuwa ni mali ya Mhindi mmoja. Mhindi huyo alikuwa anajulikana kwa jina la Firozali Kassam na watu wengi walimwita F. K. Yeye alikuwa tajiri sana. Alikuwa akiishi sehemu ya Them Hill ambako alijenga nyumba kubwa sana ambayo mashabiki waliita "White House" au Ikulu ya Arusha.

F. K alipendwa sana na wakazi wa Arusha kutokana na tabia yake ya kuwasaidia watu wenye uwezo mdogo wa kipesa. Alikuwa mtu mkarimu sana. Inasemekana nusu ya teksi zote za Arusha zilinunuliwa na wenyewe kwa mkopo usio na riba kutoka kwa F. K. Inasemekana kuwa alifuta madeni mengi ya watu walioonekana hawana uwezo wa kulipa. Ingawa hakuwa muumini wa dini ya kikristo, F. K alisaidia kujenga makanisa mengi ya madhehebu mbalimbali mjini Arusha.

Kwa muda mrefu F.K alikuwa mstari wa mbele katika kusaidia Chama na serikali katika mkoa huo, kufanya shughuli zake nyingi. Inasemekana. Kwa mfano alichanga pesa nyingi kwa ajili ya ujenzi wa makao makuu ya chama cha mkoa. Hivyo alipewa heshima kubwa sana na wakuu wa chama na serikali hapo mkoani Arusha. Kusema kweli kama angetokea mtu akasema kwamba F.K alikuwa ni mtu mbaya, basi angeuawa kwa kupigwa mawe hadhalani.

F.K alijulikana kama mtu wa watu, raia mwema na mpenzi wa watu wa rika zote. Alikuwa mtu maarufu na murua. Watu wote walimwelewa hivyo. Sifa zake zilizidi kuvuma kwani F. K alikuwa mfadhili, asiyebagua mtu awe mweupe au mweusi, masikini, fukala au tajiri. Watu wote mbele ya F.K walijiona sawa. Huo ulikuwa upande mmoja tu wa F.K.

Lakini F.K alikuwa na upande mwingine ambao ni watu wachache sana walioujuwa. Hata mtu kama Chris Tondo nae alimjuwa F.K juu juu tu.

F.K alikuwa mzaliwa wa Dar es Salaam, Tanzania, baba yake alikuwa mfanyabiashara maarufu sana Jijini Dar es Salaam, alikuwa na maduka makubwa matatu ya vipuri vya magari na alikuwa wakala wa makampuni mengi ya nchi za nje hapa Tanzania. Hivyo huyo mzee Kassam alikuwa tajiri sana. F.K alizaliwa mnamo mwaka 1945. Baada ya kusoma shule ya msingi hapo nchini, baba yake alimpeleka Uingereza ambako alipata elimu ya sekondari na chuo kikuu. Hii ilitokana na kwamba baba yake alikuwa na uwezo wa kumlipia F.K ada ya shule.

Mnamo mwaka 1967 serikali ya Tanzania ilitaifisha makampuni makubwa ya watu binafsi na kuyaweka katika mikono ya wananchi. Hatua hiyo ilifuatia kutangazwa kwa siasa za ujamaa na kujitegemea katika Azimio la Arusha. Mnamo mwaka 1972 serikali ilichukuwa hatua nyingine zaidi. Majumba makubwa ya watu binafsi yaliyaifishwa vilevile.

Wakati huo F.K alikuwa anasoma chuo kikuu huko Uingereza. Baba yake alimpigia simu na kumweleza mkasa uliokuwa umewapata nyumbani. Alimfahamisha kuwa nyumba zao therathini ambazo walikuwa wamejenga na nyingine kununua vile vile zilikuwa zimetaifishwa. Aliposikia vile F.K alipatwa na wazimu. Aliilaani serikali kiasi ambacho hajapata kusikia.

Siku hiyo jioni alienda kwenye baa na kuchapa mtindi barabara. Mara alisikika akiapa, "Naapa kwa jina la Mungu, kuna siku nitalipiza kisasi dhidi ya serikali ya Tanzania", Kwa bahati mbaya au nzuri katika baa ile kulikuwemo jasusi mmoja kutoka Afrika Kusini lililokuwa kwenye shughuri zake lenyewe. Liliposikia hivyo lilikumbuka kuwa shirika la ujasusi la Afrika Kusini lilikuwa linamtafuta mtu raia wa Tanzania ambaye angelifanyia kazi ya kijasusi huko.

Hivyo ndivyo alivyopatikana F.K na kuwekwa katika orodha ya kulipwa na shirika la ujasusi la Afrika Kusini. Pamoja na kulipwa ili afanye kazi ya ujasusi, F.K aliahidiwa kuwa angepewa msaada kulipiza kisasi dhidi ya serikali ya Tanzania. Inasemekana kuwa baadae alipotea kwa muda wa miaka mitatu na haikujulikana mahali alipokuwa. Lakini habari zilisema kuwa alikuwa huko Afrika Kusini akipewa mafunzo ya kijasusi kwenye makambi mbali mbali.

Aliporudi Tanzania alikuta wazazi wake wako kwenye pilikapilika za kuhama na kwenda Canada F.K alikataa kuondoka na wazazi wake na kusema kwamba yeye alikuwa mzaliwa wa Tanzania hivyo hakuwa na sababu ya kuihama nchi yake na

kwenda nchi nyingine. Hivyo familia yake ilimugawia sehemu ya mali iliyobaki naye akaamua kuhamia mjini Arusha. Huko ndiko alikoanzisha kampuni yake ya kuhudumia watalii iliyojulikana kwa jina la nyoka tours and safaris.

Alichagua jina hilo kwa sababu alizozijua mwenyewe. Mabwana zake walimpa fedha nyingi ambazo alizitumia kufanya mambo niliyoyaeleza na pia kujenga white house. Kutokana na utajiri wake F.K aliweza kuisarti nchi bila mtu yeyote kumshuku. Fedha zake ziliwafumba watu macho. Nyumba hiyo iliyoitwa White House ilikuwa imejengwa kwa aina yake. Ilikuwa imejengwa kwa shabaha ya kufanya ujasusi. Nyumba hiyo ilikuwa na vyumba vingine chini ya ardhi. Kulikuwa na barabara kadhaa chini kwa chini ambazo zilitokea nje ya sengenge ilizunguka ekali kumi na mbili za kiwanja cha nyumba hiyo.

F.K alikuwa hajaowa wala kuwa na watoto. Hivyo aliishi katika nyumba hii peke yake. Watumishi wake waliishi kwenye nyumba kando kando ya jumba lake. Kwa muda wote huo F.K alifanikiwa kujenga kwa nje, akaonekana kama mbwa mwitu aliyevaa ngozi ya kondoo. Alionekana mzuri kwa nje lakini alikuwa hatari kwa ndani.

Dhamila yake kubwa ilikuwa ni kulipiza kisasi. Kwa kufanya hivyo F.K angekuwa amefanya kazi katika upande wa adui namba moja wa Afrika huru na Ulimwengu mzima kwa ujumla. Hii ndiyo ilikuwa upande wa pili wa F.K ambayo ilikuwa sura yake halisi.

Chris Tondo ambaye sasa alikuwa anaelekea Themi Hill ndiye aliyejuwa F.K hakuwa mtu mzuri kama watu wengine wa mjini Arusha walivyoamini. Yeye Tondo walikuwa wakionana na kufahamiana kiajabu. Tondo alikuwa na umri karibu sawa na F.K. Walionana mara tu baada ya Tondo kustaafishwa kutoka Jeshi la Polisi kwa manufaa ya umma. Alikuwa tayari amefikia cheo cha Kamishna Msaidizi, akiwa kati ya waafrika wa kwanza kufikia ngazi hiyo. Tondo alichukulia kustaafishwa kwake kama kitendo cha fitina na hivyo alikuwa na chiki dhidi ya serikali. Aliamini kuwa alionewa wivu kwani alikuwa na nafasi nzuri ya kuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi.

Hata hivyo, ukweli ni kwamba huyu Chris Tondo alikuwa akitumia cheo chake kusaidia wahujumu uchumi. Aliwasaidia kutorosha vipusa vyote vya thamani kwa njia ya magendo. Alipostaafishwa jina lake lilitolewa kwenye magazeti ya kila siku. Kwa njia hiyo F.K ambaye alishaambiwa habari za Tondo na wale wahujumu aliowasaidia, alijuwa kuwa amepata mtu aliyekuwa akimuhitaji. F.K alijuwa Tondo hakuwa mwaminifu kwa serikali. Vile vile alishakuwa mtu mkubwa na

hivyo mwenye uzito katika jeshi la polisi. Huyu ndiye mtu aliyefaa katika mpango wake waliokuwa nao F.K pamoja na wafadhili wake.

Siku moja F.K alimfuata Tondo Jijini Dar es Salaam. Alimdanganya kwamba kuna mtu amemwelekeza kwake. Alimwambia kuwa kama ingewezekana alipenda wafanye kazi pamoja kwa kuwa hakuwa na kazi. Bila kusita Tondo alikubali akaona ni bahati iliyoje. Siku hiyo Chris Tondo alimweleza jinsi alivyoichukia serikali ya Tanzania akidaiwa kuwa ilimstaafisha bila sababu ya msingi.

"Wewe tulia tu, kuna siku mtu atalipa", F.K alimhakikishia.

Baada ya kusikia maelezo ya Tondo, F.K alijuwa amempata mtu aliyekuwa akimtafuta. Tondo aliteuliwa kuwa Meneja Mkuu wa Nyoka Tours and Safaris. Kusema kweli kampuni hiyo ilikuwa ni kisingizio. Mambo ambayo F.K na Tondo walifanya kwa siri katika kuhujumu uchumi aliyejuwa ni Mungu peke yake.

Tondo alisimama na kuegesha gari nyumbani kwa F.K. F.K alifungua mlango na kumkaribisha ndani Tondo.

"Karibu ndani.

"Asante", alijibu Tondo.

"Nimekuita ghafla kwa sababu nimepata habari sasa hivi kutoka kwa yule rafiki yangu wa Nairobi kwamba wale wageni waliokuwa wafike kesho wataingia leo jioni. Kitu ninachotaka ufanye ni kwenda kubadiri mipango huko mpakani. Kama nilivyokuwa nimekueleza awali, watu hawa wataingia bila kupitia sehemu za kawaida. Wageni hao wanayo mizigo ambayo sitaki ikaguliwe wala wao wasionekane na mtu yeyote", alieleza F.K na kisha akaelekea kwenye chumba fulani. Aliporudi alikuwa amebeba pasipoti kumi na mbili na bahasha moja.

"Pasipoti hizi ni za hawa wageni. Nenda nazo huko mpakani kwa mtu wetu akugongee mihuri ya idara ya uhamiaji. Unajuwa ni siku nyingi hatujaangalia maslahi yake. Hivyo mpelekee hii bahasha yake".

F.K alimkabidhi Tondo hivyo vitu.

"Aidha nenda kwa Hasanali mwambia kuwa wale wageni watakwenda nyumbani kwake kwa kupitia njia ya porini mnamo saa mbili usiku. Mimi nitafika hapo kuwachukuwa mnamo saa mbili na nusu usiku, na yeey tuonane hapo. Kazi ifanyike kama kawaida Tondo".

"Sawa nitatekeleza yote kama ulivyosema".

Tondo alibeba mzigo wake akaelekea nje huku akisindikizwa na mwenyeji wake.

Wakati akielekea nyumbani kwake alifikiri kwamba wakati mwingine mambo waliyofanya yalikuwa ya ajabu kama sasa alishangaa alipoona F.K anazo pasipoti za watu ambao walikuwa bado kuingia nchini hata hivyo Tondo alijuwa haikuwa juu yake kuuliza maswali. kazi yake kubwa ilikuwa utekelezaji.

Tayari alikuwa amejenga nyumba tatu. Nyumba moja ilikuwa Dar es Salaam na aliipangisha kwa Ubalozi kwa elfu hamsini kwa mwezi. Nusu ya kodi hiyo Tondo alilipwa kwa fedha za kigeni. Nyumba nyingine alikuwa amejenga nyumbani kwao Njombe ambayo kwa viwango vya huko nyumba hiyo ilikuwa ya hali ya juu. Nyumba ya tatu ni hiyo aliyojenga Arusha. Tondo alikuwa hajawahi kuoa lakini alikuwa na watoto watatu aliowapata nje ya ndoa. Watoto wake wawili wakubwa walikuwa wanasoma shule ya msingi huko London, wakati yule mdogo alikuwa anakaa na mama yake huko Njombe.

"Tangu nistaafishwe na kuungana na F.K mafanikio yangu yamekuwa ya makubwa kuliko ya mtanzania wa hali ya juu. Kweli kazi hii inanifaa shauri yao watanikoma", Tondo alijisemea kimoyomoyo.

Mara alikutana na gari lilimumulika kwa taa zake. Kabla ya kupishana alitambua ni Nyaso, hivyo akapunga mkono, Nyaso naye akampungia mkono pia.

Nyaso alikuwa ni msichana mrembo sana. Hapakuwepo msichana mwingine mjini Arusha ambaye wangeweza kushindana naye kwa urembo. Nyaso alikuwa hawala yake F.K. Watu waliojuwa penzi lao walisema kuwa Nyaso alikuwa saizi ya F.K kutokana na utajiri wake. Bali tu walishindwa kufahamu kwanini hawakuoana. Hata hivyo rafiki zake na F.K ndoa ingekuwa kinyume cha mila za wahindi. Kwa kuamua kuishi na Nyaso kama hawala kulionyesha watu unafiki wa F.K na Wahindi wengine. Waliopenda kufanya mapenzi na waafirika lakini ilikuwa mwiko kuwaoa. Wahindi walitembea na wasichana wa kiafrika na baadaye kuwatupa jalalani.

Kila wakati Tondo alipofikiria uhusiano wa watu hawa wawili aliona kuwa Nyaso hakumhitaji sana F.K. Alijuwa msichana yule alitaka pesa zake tu. Hii ilionyeswa na majibu ya mkato aliyompa F.K mara kwa mara. Lakini hata hivyo F.K alikuwa amemjengea Nyaso nyumba nzuri sana. Nyaso alikuwa haruhusiwi kwenda kwa F.K. Hivyo F.K alikuwa akienda kulala kwa Nyaso. Hata Tondo hakujuwa kwanini F.K hakupenda Nyaso aende kwake bali alilidhika alipoambiwa na F.K kwamba hiyo ingekuwa kukiuka mila za Kihindi.

"Acha mtoto wa Kitanzania amule kidogo Mhindi huyu", Tondo alijisemea.

Aliegesha gari yake nyumbani kwake halafu akajitayarisha kwa safari ya kuelekea mpakani.

# SURA YA NNE

## DAR ES SALAAM

Jijini Dar es Salaam, Tanzania, siku hiyo watu walikuwa wanasherehekea Sikukuu ya Eidd El Fitr kwa hoi hoi na vifijo. Mchana huo watu walikuwa wamejaa katika hoteli ya Kunduchi. Baadhi yao walikuwa wanaogelea, wakati wengine wakitafuna na kula vitu laini. Watu wengine walikuwa wanacheza disco la mchana. Vile vile kuna wale ambao walibaki nyumbani kwa kujuwa wangekosa nafasi kwani hoteli ya Kunduchi ilikuwa imejaa kibati.

Nje ya hoteli hiyo, karibu na ufukwe, kulikuwepo na meza moja kubwa. Kwenye meza hiyo walikaa vijana wanane. Wanaume wanne na wasichana wanne hii ina maana kuwa kila mtu alikuwa na kitu chake. Wote hawa walikuwa wamefika kusherehekea Iddy pia. Walikuwa wamekaa wakibishana huku wanauchapa mtindi. Wakati huo walikuwa wanabishana juu ya siasa ya ujamaa nchini Tanzania.

"Mimi nawaambieni, hii siasa ndio inayoturudisha nyuma. Mbona kabla ya siasa hii mambo hayakuwa hivi?", Eddy aliuliza.

"Lakini nchi nyingine zina shida vile vile", alijibu Khadija, "Siyo. Sisi peke yetu".

"Shida za nchi nyingine siyo kama zetu. Ukienda nchi za jirani, utaona wana kila kitu. Kwanini?, kwa sababu hawana siasa hii, bwana. Tusidanganyane", Eddy alisisitiza.

"Hata mimi nakubaliana na wewe Eddy", Rashid aliunga mkono.

"Mimi nilikulia kijijini. kulikuwepo mabasi manne kila siku, lakini juzi nimekwenda huko sikukuta basi hata moja. nilitembea kwa miguu umbali wa kilometa arobaini. Hivi sasa sina hata hamu ya kwenda likizo nyumbani".

"Sikilizeni jamani", Esther alianza kutoa nasaha zake, "Dunia nzima ina matatizo. Mimi naamini siasa yetu ni nzuri, ila kuna mahali ambako makosa yamefanyika. Mnajuwa kila kitu kina uzuri na ubaya wake. Inawezekana siasa hii imeleta madhala ya kiuchumi, lakini tumefaidika kwa upande mwingine watanzania tumekuwa watu wanaopendana na kuheshimiana. Tunao umoja, na mtu mkubwa hamnyanyasi mdogo. Hatuna ukabila. Katika nchi nyingine mnazozungumzia,

kama wewe ni mtu mdogo kama sisi wengine hapa unaonekana huna thamani hata kidogo. Achani jamani, siasa hii imetuletea hadhi na haki kwa kila kitu".

"Kwenda zako! wewe utakula au kuvaa heshima?, hii siasa inatuumiza, bwana, acheni", alijibu Rukia kwa hasira.

Mmoja wa vijana hao aliyekuwa anasikiliza maendeleo ya mabishano alimwemwesa, kisha akasema, "Rukia, usikasilike. Hapa tunazungumza tu na kila mtu anatoa mawazo yake. Hivyo poa mtoto, ngoja mimi niwaelezeni jinsi nyinyi mnavyobishana bila msingi. Mnajuwa, kama mtu anataka kubishana juu ya jambo fulani, lazima alielewe kwa undani jambo lenywe. Kila mtu hapa anasema ujamaa ndio umeleta hali ngumu. Lakini hali hiyo imesababishwa vipi na siasa hii?".

"Haya basi, tueleze kama unafahamu", Sammy alichokoza. "Wewe si unajiita mchumi?", Kwanza nyinyi mliosomea uchumi ndio mnatoa ushauri mbaya kwa wanasiasa hapa nchini".

Hapa vijana wote waliangua kicheko.

Kijana huyu alitabasamu kisha akawaashiria wanyamaze na yeye akaendelea kusema. "Azimio la Arusha lilitangazwa mnamo mwaka 1967. Kutokana na tangazo hilo, makampuni makubwa ya binafsi yalitaifishwa. Hatu hiyo ilifanya siasa ya ujamaa ianze kuonekana. Lakini utaona kwamba tangu kutaifishwa kwa makampuni hayo uchumi wa nchi uliendelea kukua kwa kiwango kilichoridhisha. Uchumi ulikua kwa asilimia tano kila mwaka, hadi mwaka 1977. Tulikuwa na fedha za kigeni kiasi cha kutuwezesha kuagiza bidhaa za kukidhi mahitaji ya taifa kwa muda wa miezi mitano. Wakati huo wote sisi tulikuwa hatupati msaada wa fedha kutoka benki ya dunia wala shirika la fedha la kimataifa".

"Hao wenzetu mnaowasema, uchumi wao wakati huo ulikuwa ukikuwa kwa asilimia mbili tu kwa mwaka. Na kukuwa kwa uchumi wao huo kulitokana tu na misaada ya fedha kutoka benki ya dunia na shirika la fedha la kimataifa. La sivyo hali yao ingekuwa mbaya zaidi kuliko sisi. Kwa muda wa miaka kumi ya kwanza ya siasa ya ujamaa, uchumi ulikuwa vizuri sana. Ni muhimu kukumbuka kuwa mnamo miaka ya 1973 - 1976 bei ya mafuta ilipanda. Vile vile kulitokea ukame. Lakini uchumi wa nchi uliendelea vizuri hii inaonyesha wazi kuwa siasa ya ujamaa haikuwa chanzo cha kuanguka kwa uchumi wa taifa letu".

"Ngoja nikukate kilimi", Sammy alimkatiza yule kijana.

"Sasa unafikiri nini kimetokea kama kweli sababu zako ni sawa sawa?".

"Nilikuwa naelekea huko", yule kijana aliendelea kusema.

"Kuanzia mwaka 1978 mambo yalikwenda mrama. Na mambo yote yalitokana na chanzo kilizho nje ya siasa ya aina yoyote. Kwanza Jumuia ya Afrika Mashariki ilivunjika. nyinyi mnajuwa kuwa hiyo ilitifanya tukose vitu kadhaa pamoja na huduma kutoka nchi wanachama wa jumuia hiyo. Bei ya mafuta iliongezeka sana kiasi cha kuathiri uwezo wetu utokanao na fedha za kigeni. Ukame pia uliathiri uchumi wetu. Zaidi ya hayo kulitokea vita kati yetu na majeshi ya uvamizi ya Nduli Iddy Amin. Mambo hayo ndiyo yalifanya uchumi wetu kuyumba. Na mbali na hayo, kumetokea hali fulani ndani kwa ndani. Ari ya mfanyakazi imedhorota".

"Hali ngumu ya maisha imewafanya maafisa wa ngazi za juu kuendekeza rushwa. Ni dhahiri kuwa kuna maamuzi yanafanywa na maafisa wa serikali bila kujali maslahi ya umma. Si ajabu kuona vibari vinatolewa kuhusu matumizi ya fedha za kigeni kwa shughuri ambazo siyo muhimu. Wakati ule ule sekta za uzalishaji kama kilimo na viwanda zinanyimwa fedha za kigeni za kununulia pembejeo na kadharika siyo sahihi, kwa kweli, kusema kwa njia ya mkato kwamba mambo haya yamesababishwa na siasa ya ujamaa. Na kama nilivyokuwa nimesema hapo awali, shirika la fedha la kimataifa na benki ya dunia havikutupatia hata senti tano. Wakati huo huo wenzetu walipewa mamilioni ya fedha za kigeni".

"Nia ya vyombo hivi ilikuwa kuhakikisha kuwa uchumi wetu unaanguka kwani vilichukia siasa ya ujamaa ambayo ni ya kimapinduzi. Walikataa kutusaidia huku wakifahamu fika kuwa matatizo yetu hayakutokana na siasa ya ujamaa. Lakini iliwafaa kutusingizia. Sasa pia na nyinyi mmejiunga na mabepari katika kulaumu badala ya kujiimarisha...".

"Mara muhudumu mmoja wa hoteli hiyo alifika hapo mezani na kuuliza, "Wewe si ndiye Willy Gamba?".

"Ndio", yule kijana alimjibu haraka muhudumu.

"Kuna simu yako mapokezi".

"Ahsante. Hebu nikasikilize simu halafu nitakuja tuendelee".

Yule kijana aliondoka na kuwaacha wameduwaa kutokana na maelezo yake mazito na yenye msingi.

Pale mapokezi alimkuta muhudumu wa kike.

"Wewe mwanamume, hapo ulipokaa una bibi na bado unatafutwa na bibi mwingine", muhudumu wa kike alimtania yule kijana. "Hutosheni mwenzetu?".

"Nifanye nini, bibie, na wakati ndio huu! lazima niutumie ujana wangu, sitaki kuujutia nikishazeeka", Willy alijibu, kisha akauchukua mkono wa simu na kuupachika kwenye sikio lake.

"Unauchapa tu mwenzetu", sauti ya Maselina ilisikika waziwazi sikioni mwa Willy Gamba.

"Unataka kuja?", Willy aliuliza.

"Unataka huyo bibi yako anikate masikio?" Sina haja ya kuharibiwa sura mwenzako.

"Sasa unasemaje?".

"Nasema hivi: niko ofisini pamoja na Chifu. Unatakiwa kama ulifikili mambo yamekunyookea na huyo msichana uliyenae, basi ulie tu. Unatakiwa sasa hivi. Umenielewa?", Maselina alisema kwa kebehi.

"Hamniachii angalau sikukuu hii nikala raha kidogo?".

"Njoo umweleze mwenyewe maneno hayo huyu babu yako, kwani mimi hiyo raha siitaki? Au kwa kuwa umenizoea unafikiri mabwana hawanitaki. Hata mimi nimechomolewa kutoka kwenye raha na pilika pilika safi za Iddy El Fitri.

"Wacha utani; nakuja sasa hivi".

Willy aliyakata mazungumzo, kisha akaiweka simu chini.

"Vipi huyo mkeo?", yule msichana wa mapokezi alimuuliza Willy mara alipokata simu.

"Afadhali ningekuwa na mke", alijibu Willy huku akielekea kwa wenzake.

Alipofika mezani ilibidi anywe pombe yake haraka ili aweze kuondoka. Jambo zuri ni kwamba vijana wote walikuwa wanafanyakazi ofisi moja na Willy ndiye alikuwa mkubwa wao wa kazi.

"Samahani", Willy aliwataka radhi vijana wenzake. "Imenilazimu nikitoe. Kuna mZee wangu ameshikwa na ugonjwa wa ngiri. Lazima nimpeleke hospitali".

Wale vijana wenzake walielewa ana maana gani ila wale wasichana masikini walidhani maneno ya Willy yalikuwa ya kweli.

"Oh pole sana," Rukia na Esther walisema kwa pamoja.

"Ahsante. Mwana, tunakwenda au unabaki? Willy alimwuliza mpenzi wake.

"Nibaki vipi?" Mwana alihamaki, "huoni kitu mtu hapa? Je, ukiniacha halafu wenzangu wakaamua kuchukua vyumba vya kulala, mimi nitafanyaje?"

"Kwangu wawili ni saizi," Sammy alitania" usiwe na wasiwasi".

"Rukia mwenzetu, mbona unayo shida."

"Maneno tu. Atawahi? kila siku jasho linamtoka," Rukia alijibu huku Mwana na Willy wakiinuka kuondoka.

Willy Gamba alikuwa ni mpelelezi maarufu aliyekuwa akifanya kazi katika idara ya upelele ya Tanzania. Sifa zake zilitapakaa katika Bara zima la Afrika. Kutokana na ujasiri wake, watu wengi walifikiri mtu huyu alikuwa wa kubuniwa tu maanaa watu walifikiri kuwa vitendo vya Willy Gamba vilikuwa kama mchezo wa sinema.

Lakini ukweli ni kwamba huyu mtu yupo na vitendo vyake ni vya kweli tupu. Kijana huyu alikuwa amefanyakazi kubwa sana katika kusaidia harakati zinazoendeshwa na umoja wa nchi huru za Afrika. Kwa sababu hiyo yeye alijulikana katika Afrika nzima. Watu wengi waliohusika na kazi yake na wale waliobaki waliishia kusoma na kusikia habari zake bila kuamini.

Wakati akiendesha gari lake kuelekea mjini, Willy alikuwa na mawazo mengi. Maswali mengi yalimjia kichwani. Kwanini, kwa mfano, Chifu alikuwa anamhitaji wakati wa sikukuu kama hii?, lakini alihisi kulikuwako na kazi muhimu, kwani haikuwa kawaida ya Chifu kumbugudhi wakati wa mapumziko kama hayo. Chifu, kama alivyoitwa, ndiye alikuwa mkubwa wake wa kazi. Alikuwa Mkurugenzi wa upelelezi nchini Tanzania. Alikuwa Mzee wa miaka mingi katika kazi hiyo na sifa zake zilitapakaa mahali pengi, hasa kwa kumtoa kijana shupavu kama Willy.

Willy alipofika njia panda kati ya New na Old Bagamoyo ndipo mawazo yake yaliporudi kwa huyu msichana ambaye alikuwa pamoja nae kwenye gari. Msichana huyu alikuwa ameanza kusinzia. Mwana alikuwa anaishi sehemu za Mwenge, sehemu iliyo nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

"Mwana", Willy alisema. "Nitakupeleka nyumbani kwako halafu mimi nitaendelea na safari".

"Aka, babu, twende wote", Mwana alilalamika.

"Kwani huyo Mzee wako mimi siwezi kumpeleka hospitali?".

"Wewe unajuwa Mzee anayeumwa ngili anakuwaje?, unataka kukosa radhi kwa kuangalia vitu vya wazee, nini?", Willy alimwasa huku akipinda kona kuingia barabara ya New Bagamoyo.

"Hukosi sababu wewe. si ajabu ni mwanamke mwingine unayemfuata huku ukinidanganya, maana wewe umezidi", Mwana alijibu huku machozi yanamlengalenga.

"Wacha wivu usiokuwa na msingi mama, haukusaidii kitu. Kama ningekuwa na bibi mwingine kwanini nikuchukue wewe tangu asubuhi?, na huyo bibi ana nini mpaka nikurudishe na kumfuata yeye wakati wewe kwangu ndio mipango inanyooka?", Willy aliuliza huku akicheka.

"Eh, huenda mipango yake ni zaidi. Nitajuaje mie?", MWana alisema kwa kejeli.

"Afadhali ningekuwa na bibi kama huyo. Lakini hawajaanza kuzaliwa. Nasikia wataanza kuzaliwa mwaka Elfu mbili", Willy alijibu.

"Wacha maneno mengi, utarudi?".

"Usiwe na wasiwasi. Nikimaliza shughuri na mzee nitarudi".

"Au ukaniache nyumbani kwako", Mwana aliomba kwa sauti nyororo.

"Mimi nitakuja kwako, si mzee yuko nyumbani au hunielewi?".

"Si mimi nitampikia?".

"Asante, lakini bado sijakutambulisha rasmi. Subiri mpaka nifanye hivyo kwani wazee hawa wana nyadhifa zao", Willy alisema huku akikata kona kuelekea nyumbani kwa Mwana. Walipofika Mwana alimvuta Willy na kumpa busu kali kisha kumwachia huku akisema, "Usiporudi usishangae kusikia kuwa nimekula kulolokwini kumi, wala usinilaumu".

"Nitarudi", Willy aliahidi.

Baada ya Mwana kutelemka, Willy aliondoa gari, moyoni alikuwa anashangaa jinsi wasichana walivyo. Hii ilikuwa miadi ya pili tu kati yake na Mwana. Hata hivyo msichana huyu alikuwa amekufa hasa kwa Willy. Willy aliendesha moja kwa moja hadi ofisini kwake katika mtaa wa Samora, katikati ya Jijini. Baada ta kuegesha gari alipanda ngazi. Aliongoza moja kwa moja mpaka kwenye ofisi ya

Chifu. Alipofungua mlango kuingia kwa Katibu Muhtasi wa Chifu, alimkuta Maselina ameng'ang'ana na simu.

"Pole mwenzangu, nakwambia kazi hii itakuja kutuua siku moja", Maselina alimkebehi Willy.

"Inatufaa lakini. Yupo?", Willy aliuliza.

"Aende wapi!, leo kawa mzee ile mbaya, sijui nini kinamtia homa mzee wako", Maselina alimwalifu.

"Basi ukiona hivyo ujuwe mambo ni yale yale. Asipostaafu huyu mzee atakuja kutufia humo ofisini kutokana na ugonjwa wa moyo".

"Afe kwa ugonjwa wa moyo?, kwa ugonjwa huo utakufa wewe kabla yake. Mzima kweli huyo", Maselina alisema.

"Umeshajaribu kutingisha kiberiti na kujua ziko njiti ngapi nini?", Willy alitania.

Maselina alichukua rula na kutaka kumpga nayo. Willy aliepa huku akikimbilia mlango wa ofisi ya Chifu.

"Muhuni mkubwa, we!", hayo ndio maneno aliyoyasikia Willy yakitoka kinywani mwa Maselina.

Watu hawa wawili walikuwa wamefanyakazi pamoja kwa muda mrefu. walikuwa wakielewana kiasi kwamba walikuwa kama kaka na dada mtu au hata mpenzi.

Willy alipofungua mlango wa kuingia ndani alimkuta Chifu anasoma gazeti la Daily News.

"Shikamoo mzee", Willy alisalimia.

Chifu aliinua kichwa na kumtazama usoni.

"Marahaba. Imebidi nikuite maana nimepata habari ambazo zinahitaji sisi kuzishughulikia mara moja", Chifu alieleza.

"Nimepata habari kutoka Lusaka kuwa kumefanyika mkutano kati ya wakurugenzi wa upelelezi wa Zambia, Zimbabwe, Angola, Msumbiji na Botswana, pamoja na wakuu wa upelelezi wa wapigania uhuru. Sisi hatukuweza kuwakilishwa kutokana na sababu ambazo hazikuweza kuzuilika. Mazungumzo yao yalihusu mkutano wa wapigania uhuru ambao utafanyika kesho kutwa huko Arusha. Nafikiri unazo habari".

"Ndio ninazo".

"Kuna habari za kuaminika kwamba makaburu wana nia ya kuleta maafa makubwa na kuvuruga mkutano huo. Habari hizi ni za kipelelezi. Sasa sisi tunaombwa tuwe macho. Ingawa idara ya Polisi ilishajidhatiti kwa ulinzi huko Arusha, ni lazima na sisi tushughulikie suala hili kikamilifu. Hii ni kwamba kama kweli makaburu wamenuia kutenda kitendo hicho, bila shaka watatumia majasusi wa hali ya juu ambao wana uwezo mkubwa. Tayari wapigania uhuru wameshatuma mpelelezi wao maarufu Bon Sipele. Serikali ya Zimbabwe nayo imetuma mpelelezi wake mashuhuri Rocky Malele. Hao watawasili hapa leo jioni wakiwa njiani kuelekea Arusha...".

"Kwa hiyo hatuna budi kuungana nao leo hii ili kuimalisha usalama wa mkutano huu. Wakuu wa nchi wamekwisha julishwa. Vile vile Kamati ya ukombozi wa nchi huru za Afrika pamoja na wapigania uhuru wameaziimia mkutano huo lazima ufanyike. La sivyo, litakuwa pigo kubwa kwa wapigania uhuru na Afrika nzima na ushindi kwa makaburu. Kwa hiyo Willy hatuna uhakika makaburu watatumia mbinu gani. Ni dhahiri kuwa makaburu hawatatumia Jeshi ingawa Jeshi letu tayari limewekwa katika hali ya tahadhari tunahisi makaburu watatumia majasusi ili kuhujumu mkutano na ikibidi kuua wajumbe wengi kadiri inavyowezekana...".

"Kazi yako wewe na wenzako ni kuhakikisha kwamba jambo hili halitokei na mkutano utafanyika kama ulivyopangwa. Huo ndio utakuwa ushindi kwa Bara la Afrika na vile vile kuwatia hamasa wapigania uhuru. Baada ya mkutano huo wapigania uhuru watakuwa na nguvu mpya. Hivyo makaburu watakiona cha mtema kuni. Nafikiri umenielewa", alimalizia Chifu.

"Hatua gani za tahadhari zimechukuliwa awali, kwani inawezekana majasusi na makaburu wameshaingia nchini tayari", Willy aliasa.

"Walinzi wote kwenye mipata wameshatahadhalishwa na jeshi la polisi linafanya kazi yao. Viwanja vya Ndege vya Dar es Salaam na Kilimanjaro viko kwenye hali ya tahadhari. Wana usalama wanapekuwa vikali kila mtu anayeingia na kutoka. Wote wako macho. Kama ni kuingia nchini Majasusi hawawezi kuingia nchini mapema kwa kuogopa kugutukiwa", alijibu Chifu.

"Je wajumbe wameshawasili?", Willy aliuliza.

"Kufuatana na ripoti ya Polisi baadhi ya wajumbe wameshaanza kuingia. Wengine wako Arusha tayari. Ndio sababu lazima nyinyi muondoke leo. Tuketi yako iko

tayari kwani Maselina kaishaandaa kila kitu kwa ajili ya safari yako", Chifu alimwambia Willy.

"Ni nani tutashughulika nae huko Arusha?".

"Hatutaki Polisi huko Arusha wajuwe kuwa nyinyi mnakwenda huko. Wakijuwa hivyo wanaweza kuridhika kuwa usalama upo halafu wasifanye kazi yao barabara. Hata hivyo Afisa Usalama wa mkoa anayo habari. Hivyo huyo ndiye mtu wa kumuona. Ndiye mtu wa kumwamini".

"Ni sawa kabisa, Hamisi ni mtu wa kuaminika. Lakini mbali na Hamisi, nisingependa mtu mwingine ajuwe kwani mimi nafahamu majasusi wa makaburu wanavyofanya kazi yao", Willy aliongezea.

"Sasa nenda ukajitayarishe. Vile vile nataka ripoti kutoka kwako kila wakati unapogundua kuna kitu kipya. Kama utahitaji msaada wa vijana wako uko huru kufanya hivyo, kwani watakaa hapa ofisini katika hali ya tahadhali", alisema Chifu.

"Ahsante, tuombe Mungu", Willy alijibu.

Alipofika karibu na mlango Chifu alimwita tena.

"Willy, chunga sana kwani makaburu siyo watu wa kawaida", Chifu alionya.

"Nitajihidi na Mungu atatusaidia". Willy alijibu na kutokea kwenye ofisi ya Katibu Muhtasi.

"Kwanini ukunibonyeza kwamba ninasafiri na wewe ndiye uliyekata tiketi, una visa wewe", Willy alimwambia Maselina.

"Nikwambie nini, mimi ndiye niliyekuajiri?. Mimi siyo mmbeya, bwana wewe", Maselina alisema.

"Najua unafurahi rohoni kwa kuwa mimi nasafiri. Wacha roho mbaya".

"Wewe Willy, wacha kuniumiza roho. Unajuwa jinsi gani ninavyojisikia ovyo unaposafiri. Mimi siyo kama hao wahuni wako, leo ukienda usirudi kesho wanao wengine. mimi kwangu wewe ni rafiki ambaye hana kifani na siwezi hata kufikiri ninaweza kuishi vipi bila wewe", Maselina alieleza kwa masikitiko makubwa.

"Niombee na Mola atanisaidia", Willy alijibu.

"Nakuombea kila siku", alimwambia Willy huku akimpa tiketi yake, "Chunga sana".

"Ahsante Maselina, nitajitahidi", Willy alijibu akainama akambusu kwenye shavu halafu akaondoka.

Wakati Willy alipokuwa anaelekea kwake alianza kuwafikiria akina Bon na Rocky. Kule kuwafikiria kulimfanya apate nguvu rohoni mwake. Hii ilitokana na kwamba Willy aliwafahamu fika hao wenzake na zaidi ya hayo aliwaamini. Alifikiri sana juu ya kazi iliyokuwa mbele yake. Ni kweli kwamba kazi hiyo ilikuwa imewekewa uzito wa hali ya juu kama ilibidi kuwatuma watu wote hawa watatu katika operesheni moja. Mchukue Bon. Kwa mara kwanza Bon kufahamiana na Willy ilikuwa huko Japan ambako wote wawili walikuwa wanachukua mafunzo ya Ninja. Willy alikuwa amehitimu mapema na kumwacha Bon ambaye alikuwa amejiunga na chuo hicho nyuma yake. Willy alikuwa amemsaidia sana Bon katika masomo yake na alijuwa fika kwamba Bon nae angehitimu tu.

Bon alimchukulia Willy kama kaka yake na wote wawili walipendana sana. Baada ya mafunzo yake Bon alirudi Zimbabwe ambako alikuwa anakaa. Wakati huo Kamati ya Ukombozi ya nchi huru za Afrika iliwatuma kazi muhimu ambayo waliifanya kwa mafanikio makubwa. Kazi hiyo ilifanyika ndani ya Afrika Kusini na mpaka leo makaburu hawaamini kwamba kazi hiyo ilifanyika na watu wawili. Kisa hiki kukieleza kingechukua siku nzima, hivyo naachia hapa. Bali tu niseme kuwa safari yao huko Afrika Kusini iliwafanya wafahamiane vizuri na kila mmoja kudhibiti ujuzi na uwezo wa mwenzake. Kwa hiyo Willy, alipojuwa kuwa angekuwa na Bon katika kufanya kazi hii, basi wasiwasi ulitoka.

"Ninja wawili kutumwa Arusha. Kwani huko kuna nini?, labda makaburu watume jeshi zima", Willy alijisemea kimoyomoyo. Alimfikiria Rocky pia. Ingawa ni mara yake ya kwanza kufanyakazi nae, umaarufu wake ulijulikana Afrika kote. Walikuwa wameonana mara mbili. Lakini ilijulikana Rocky alishatumwa kazi ambazo zilifanana sana na kujituma mikononi mwa kifo. Pamoja na hali hiyo, Rocky alikuwa amefanyakazi hizo na kurudi salama. Kuweza kufanyakazi kama hizo kulimdhihilishia Willy kuwa Rocky alikuwa mtu jasiri sana. Willy aliamini kuwa yeye na vijana hao wawili walikuwa na uwezo wa kuwazuia makaburu kusababisha maafa katika mkutano huo muhimu wa wapigania uhuru.

Kulikuwapo habari za kipelelezi kuwa baada ya mkutano huo, mapambano ya kupigania uhuru yangeahamia ndani ya Afrika Kusini. Kwa hiyo kama makaburu

walikuwa na fununu juu ya habari hizi, ilikuwa ni dhahiri kwamba wangejitahidi kuvuruga mkutano huo, kinyume cha kufanya hivyo ilikuwa kufungua mlango ili wapigania uhuru waiangishe serikali ya makaburu. Makaburu walijuwa fika kuwa mkutano huo ulikuwa hatua ya kwanza muhimu katika safari ya kuuangusha utawala wao bila kujali safari hiyo ilikuwa ndefu kiasi gani. Kuzuia hatua hiyo ilikuwa lazima kwao.

Alipofika nyumbani Willy alikwenda bafuni na kuoga. baadae alifungua sanduku lake ambamo alikuwa anatunza zana zake muhimu za kufanyia kazi. Alizichukua na kuziweka kwenye mkoba wake, alipiga simu kwa Sammy ambaye alimwarifu kuwa alikuwa anasafiri kwenda Arusha na kuwa habari zaidi angezipata ofisini. Vile vile aliomba atumwe mtu uwanja wa ndege kwa ajili ya kurudisha gari lake. Sammy alikuwa chini ya Willy kikazi lakini walikuwa marafiki wakubwa sana na mara nyingi walifanyakazi pamoja. Baada ya kupiga simu aliondoka kuelekea Mwenge ili kumwaga Mwana.

# SURA YA TANO

**ALIFIKA** nyumbani kwa Mwana mnamo saa moja usiku. Tiketi yake ilikuwa inaonyesha kuwa safari yake ilikuwa saa tatu na nusu usiku. Hivyo Willy alikuwa bado na muda kuzungumza machache na mpenzi wake. Alipofika alibisha hodi na kufunguliwa mlango. Alikaribishwa ndani. Mwana alikuwa amejinyoosha na huku amejifunga kanga tu.

"Afadhali umekuja, nilikuwa na wasiwasi! vua ulale", Mwana alimwambia Willy.

"Nimekuja kukuaga", alijibu Willy.

Mwana aliinuka na kanga aliyokuwa amejifunga ikadondoka. Willy alitupa macho yake na kuona mwili wa mtoto huyu ambaye ubichi wake ulisisimua na kuchangamsha roho. Matiti yalisimama kwenye kifua chake kilichokuwa kinatweta utafikiri ni mapera yaliyoiba. Mwana alimrukia Willy aliyekuwa amekaa kwenye tendegu la kitanda na kumkumbatia. Joto la msichana huyu lilimwingia willy kama kisu kinavyotoka na kuingia ndani ya siagi. Ilihitaji mtu mwenye roho ngumu kama Willy kushinda jaribu hili.

"Mwana tafadhari niache niende", Willy alimsihi.

Mwana ambaye sasa alikuwa anatokwa na machozi alisema kwa uchungu, "Willy, kwanini unanitesa? kama hunitani si heri unieleze tu. Kama huna hamu na mimi kwanini ulinidanganya tangu siku ya kwanza. Kwanini usingeniambia ukweli kuliko kunitesa hivi, ooh! mungu wangu nimekosa nini mie".

Mara Mwana alijitupa kitandani na kuanza kulia; machozi yakimtililika kama mtoto mdogo.

"Mwana tafadhali, kuna kazi imetokea ghafra. Nilipotoka tu hospitali kumpeleka mzee nilikuta tiketi na ujumbe kutoka kwa mkubwa wetu wa kazi kuwa lazima niende Arusha. Kama ujuavyo sisi wafanyabiashara safari zetu ni za ghafra ghafra tu. Wewe unafikiri ni kijana gani ambaye anaweza kumwacha msichana mbichi kama wewe kwa siku na saa kama hii, na hasa baada ya raha ya leo mchana? Huyo huenda siyo mwanaume kamili", Willy alijibu kwa uchungu pia kwani hata yeye alikuwa amesisimka.

"Basi lala angalau kidogo. Dakika tano tu", Mwana alimwomba Willy.

"Mwana mambo haya hayaendi namna hiyo. mimi nitarudi baada ya siku mbili au tatu. Baada ya hapo wewe mwenyewe utajua kuwa nina hamu kiasi gani mimi na wewe," Willy alijibu.

"Haya nenda. Nakuruhusu," MWana alisema kwa uchungu.

Willy aliinama na kumbusu. Alisikia lile joto tena. Bila kusita aliinuka, akafunga mlango nyuma yake na kwa maudhi alijisemea, "Kwa kweli kazi nyingine......!".

Alipoingia ndani ya gari aliweka nyuma mawazo kuhusu Mwana. Wakati akiendesha gari, alifikiria safari iliyokuwa mbele yake.

Alifika uwanja wa ndege saa mbili usiku. Aliweka gari lake kwenye maegesho. Kisha alitoa swichi kwenye funguo zake na kuiweka mahali pa hifadhi ya swichi za magari. Hivyo ingemwezesha kijana ambaye angekuja kurudisha gari lake kuichukua hapo. Alifunga milango mitatu na kuacha mmoja umerudishiwa. Kisha kuchukua mkoba wake na kuelekea kwenye jengo la uwanja wa ndege.

"Tiketi yake tafadhari", aliomba Afisa Usalama hapo uwanjani.

Wakati anatoa tiketi yake alikuwa akiangaza huku na kule katika jengo zima.

"Haya endelea", alisema Afisa Usalama huku akimrudishia Willy tiketi yake.

Alielekea ndani. Kwenye kaunta alimkuta msichana aliyemfahamu.

"Willy, safari tena?", msichana aliuliza.

"Ndio", alijibu Willy.

"Wapi".

"Arusha".

"ZIko ndege mbili usiku huu. Wameongeza nyingine kwa sababu wageni wengi wanakwenda Arusha kwenye mkutano", msichana yule alimweleza Willy.

"Alaaa, sasa mimi niko ndege ipi?", Willy aliuliza.

"Chaguo lako. Sema unataka ipi. Iko ya saa tatu na nusu na pia ile ya saa nne na nusu", mischana alijibu.

"Subiri kwanza, ile ndege kutoka Harare imefika?".

"Ndio. Imefika saa moja".

"Kulikuwamo wageni wangu wanaopitiliza kwenda Arusha", Willy alisema.

"Majina yao tafadhari", msichana aliomba huku akimsogeza Willy pembeni ili watu wengine wasiweze kusikia. Halafu alimtaka aendelee.

"Sipele na Malele".

Msichana yule aliangalia kwenye orodha ya majina ya wasafiri kisha akainuka.

"Ya, wote wapo. Sasa hivi wanakula kwenye mghahawa hapo juu. Wataondoka kwa ndege ya saa nne na nusu", msichana alieleza.

"Oke, mimi niweke kwenye ndege ya saa tatu na nusu", Willy alisema.

Jina lake liliwekwa katika orodha.

Halafu alisema, "Hebu nikawaangalie hapo juu".

Alipopanda kwenye baa na mghahawa alikuta watu wamejaa ndii. Huku akisalimiana na watu huku na pale, Willy alijipenyeza kupita kwenye baa mpaka kwenye mghahawa. Mara aliwaona Bon na Rocky wamekaa kwenye kona wakila na kuzungumza. Aliwaendea polepole na Rocky ndiye alikuwa wa kwanza kumuona Willy.

"Bon, Willy yule".

"Aaaa mzee!", Bon alisema kwa furaha huku akiinuka na kumkumbatia Willy.

"Usinipakazia uzee, Bon, au huoni humu ndani kuna watoto. Unataka kuniharibia soko, vipi?", Willy alisema kwa mzaha.

"Hujaacha matani yako tu?", Bon aliuliza huku wakipeana mikono.

"Keti, bwana", Rocky alimvutia kiti.

"Ehee, leteni habari", Willy alisema.

"Mambo safi", Rocky alijibu.

"Safari, je".

"Safi kabisa", alijibu tena Rocky.

"Tulipata habari kuwa tungeungana hapa", alisema.

"Mimi nimeambiwa leo mchana", Willy alijibu.

"Kila mara huyo mzee wako anapenda kukushtusha", Bon alitania.

"Wazee wengine kama ujuavyo...", alisema Willy.

"Chakula vipi", Rocky alimuuliza willy.

"Mimi ndiye napaswa kuwauliza swali hilo kwa kuwa mko nyumbani kwangu", alisema Willy.

"Tumwisha jikaribisha", Bon alijibu.

"Vipi mzee wako kakupasha kidogo?", Rocky alimuuliza Willy kwa sauti ya chini.

"Kanipasha", Willy alijibu.

"Je, tutasafiri katika ndege moja".

"Hapana, mimi sina budi nitangulie na ile ya tatu na nusu, kama ujuavyo wote hatuwezi kusafiri katika ndege moja, ikianguka, je", aliuliza Willy.

"Willy hubadiliki", Rocky aliuliza.

"Siku nikibadilika ndio siku nitakapoacha kazi hii", Willy alijibu.

"Ni kweli, maana waati huo itakuwa ni hatari kwa maisha yako", Bon aliongeza.

Waliendelea kuzungumza huku wakiangalia kwa chati; kila kona ili kuona kama kuna watu waliowatia maanani. Lakini kufuatana na hali ya mambo ilionekana kila mtu alikuwa anashughulika na mambo yake.

"Tukutane hotelini kwangu mnamo saa sana usiku", Rocky alieleza.

"Wewe uko hoteli gani?", Willy aliuliza.

"Mimi niko Equator Hoteli kwa leo halafu nitahamia Mount Meru hapo kesho, Bon alitaka Safari Hoteli", Rocky alimjibu.

"Basi mimi naona tukutane kesho asubuhi, mpate kupumzika leo kwani huenda kukawa na kazi kali baadaye. Mimi nitafikia New Arusha Hoteli", Willy alieleza.

"Mimi nafikiri maneno yako ni sahihi Willy", Bon alijibu.

"Oke, tuonane wapi na saa ngapi".

"Njooni hotelini kwangu saa tatu asubuhi", alijibu Willy.

"Oke, ahadi........", Rocky alijibu.

Mara walisikia tangazo;

Shirika la ndege Tanzania: Ndege namba 1001 iendayo Arusha, niko tayari kuondoka, abiria wote wanaosafiri na ndege hii wanaombwa kuelekea kwenye ndege hiyo sasa hivi.

"Jamani eeh, kwaherini. Tutaonana kesho", Willy aliwaaga wenzake na kukimbia akiteremka chini.

Alipofika kwenye kaunta alimkuta tena yule msichana.

"Siku nyingine utaachwa wewe".

"Niko macho", Willy alijibu.

"Utaniletea nini ukirudi?".

"Vitunguu".

"Nitafurahi sana. Haya safiri salama", yule msichana alimuaga.

"Ndipo Willy alikumbuka kuwa alikuwa hajakata tiketi ya malipo ya kiwanja. Hivyo alifanya karaka na kukata tiketi hiyo. Halafu alirudi na kwenda kwenye chumba cha kuondokea. Hapo chumbani Willy alikuta msururu bado mrefu sana.

"Loh! Leo pana jua nini iko. Watu hapana panda", Mhindi mmoja alilalamika.

Huenda kuna mtu anayo bastola. Labda wanaogopa kutekwa nyara maana hapo ndani wanakagua sana", Kijana mmoja alijibu.

Msururu huo ulikwenda polepole, lakini hatimaye wote walipekuliwa. Kisha waliruhusiwa kuingia ndani ya ndege. Willy alikuwa ameridhishwa na upekuzi ule kwani ulikuwa upekuzi kweli kweli.

Willy alikaa nyuma kiti cha mwisho kama kawaida yake. Alifunga mkanda na kisha na kisha akakaa akisubiri matangazo ambayo alishayasikia mara elfu kidogo. Hayo yalikuwa matangazo ya IATA yahusuyo usalama wa usafiri wa anga. Baada ya matangazo hayo, ndege yao aina ya Boing 737 ilirushwa na vijana hawa wa Kitanzania.

Willy aliinamisha kiti chake kikakaa sawa. Akaanza kufikiri juu ya yale yote aliyokuwa akiambiwa na Chifu. Alichambua kipengele kimoja baada ya kingine na namna ya utekelezaji wa kazi nzima.

"Patakuwa na kazi", Willy alisema moyoni kwake.

Ilikuwa sikukuu ya Idd. Siku ile Willy na Chifu walipozungumzia mipango kujidhatiti kiulinzi ili kuzuia uwezekano wa majasusi wa makaburu kuingia nchini bila kujulikana na kuvuruga mkutano wa wapigania uhuru. Wakati huo huo majasusi tayari wameshaingia mjini Arusha na tayari walikuwa wanapumzika nyumbani kwa F.K wakiwa tayari kuanza kazi. Hiyo ilikuwa na maana kwamba usiku wa jana yake F.K na Tondo kwa upande wa Tanzania na Peter kwa upande wa Kenya walikuwa wameweza kuwaingiza nchini kwa siri. Zaidi ya hayo, majasusi wa Makaburu walikuwa wameingiza mizigo yao yote. Asilimia mia tisini ya mizigo hiyo zilikuwa ni silaha za aina mbali mbali na vyombo vya kisasa vya kufanyia ujasusi.

Kwa kuwa gari la F.K lilikuwa halipekuliwi, safari yao kutoka mpakani hadi Arusha haikuwa na kisanga chochote. Pamoja na ulinzi mkali uliowekwa kwenye vizuizi njiani, watu hao waliweza kupita. Kila alipofika kwenye kizuizi F.K alitoa kichwa chake nje tu na maafisa wa polisi kimzaha walimpigia saluti na kumwashilia aendelee. Hivyo sifa za kinafiki za F.K ziliweza kusaidia majasusi wa makaburi wa Afrika Kusini kuingia Tanzania tayari kutoa kipigo dhidi ya wapigania uhuru wa Afrika huru kwa ujumla.

Baada ya kuvuka mpakani, Peter alirudi Nairobi akiwa ameridhika kuwa nusu ya kazi yake ilikuwa imefanyika tayari.

Mchana wote wakati majasusi walipokuwa nyumbani kwa F.K walikuwa wanajitayarisha walisafisha silaha zao, na wale Ninja wawili walifanya mazoezi madogo madogo. F.K alikuwa amewapeleka likizo wafanyakazi wake wote hivyo aliacha nyumba yake nzima itumike na majasusi. Walikuwa wakijipikia na kujifanyia mambo kadhaa. Kama nilivyoeleza hapo awali, nyumba ya F.K ilikuwa imejengwa kwa madhumuni kama hayo. Hata mtu angefika kwa F.K asingeweza kugundua kuwepo kwa majasusi kwani walikuwa wanatumia vyumba vya siri.

Ilikuwa yapata saa za jioni wakati F.K alipowakusanya majasusi ili kuwapasha habari.

"Sasa hivi nimepata habari kupitia kwenye chombo cha kupashana habari kilicho chumbani kwangu", F.K alisema "Wakubwa wetu wamepata habari kuwa mpelelezi mashuhuri wa wapigania uhuru, Bon Sipele na mpelelezi mwingine mashuhuri kutoka Zimbabwe, Rocky Malele, wameondoka leo mchana mjini Harare na Ndege ya shirika la ndege la Tanzania wakiwa njiani kuelekea Arusha. Taarifa niliyonayo inasema kwamba watu hawa ni hatari sana. Hivyo ni lazima

wauawe, la sivyo watatia dosari katika mipango yetu. Vile vile nimeelezwa kuwa Paul na Fouche wanawafahamu watu hawa".

Nyumbani kwa F.K kulikuwa na chombo kupashana habari cha hali ya juu sana. Chombo hicho kilikuwa kinapokea habari kutoka kwenye Setelaiti. Setelaiti hiyo iliwekwa angani na Makaburu wa Afrika Kusini wakisaidiwa na Marekani. Kazi yake kubwa ilikuwa kupashana habari za kijasusi. Hivyo mawasiliano kati ya F.K na mabwana zake yalikuwa hayapitii njia za kawaida. Ndiyo sababu aliweza kupashana habari na hao bwana zake bila kugunduliwa na vyombo vya upelelezi vya Tanzania.

"Ndio, tunawafahamu vizuri sana", Paul alijibu.

"Kama kweli hawa watu wanakuja", Fouche alieleza "ni lazima kujiweka tayari. Hao mimi nawajuwa siyo mchezo. Kama maagizo yanasema wauawe mara moja ni sahihi kabisa. Wakisha fahamu na kuwa na wasiwasi wanaweza kufanya kazi yetu iwe ngumu. Ujuzi na uwezo wao ni mkubwa. Mimi naamini kuwa hata kama wanatutilia wasiwasi, bado hawajui kama tayari tumeingia. Wao wanatarajia sisi tuingie kwa ndege. Hivyo watajishughulisha na kuchunga viwanja vya ndege vya Dar es Salaam na Kilimanjaro".

"Kama wameweza kutuma wapelelezi mashuhuri kama hao", John aliasa "Ina maana hata serikali hizi zinahisi kitu".

"Lazima. Lazima mjue nchi hizi sasa hivi siyo mchezo", F.K alionya "nchi hizi zina uwezo mkubwa wa kipelelezi. Hivyo mfahamu kuwa mmekuja kupambana na watu wenye ujuzi kama wenu hivyo msifanye mchezo".

"Watafika saa ngapi watu hawa", Geoger aliuliza. Yeye ndiye alikuwa mkubwa wa kikosi hiki na pia mmoja wa wale ninja wawili. Yeye na Dave walikuwa na uwezo mkubwa kuliko wale wenzao.

"Ndege hiyo inatarajiwa kufika hapa saa tatu na nusu", F.K alieleza "Lakini nimepata habari sasa hivi kutoka kwa watu wangu walioko uwanja wa ndege kwamba kutokana na wingi wa wageni kutakuwa na ndege mbili. Kama mnavyojuwa mpaka sasa wageni wengi wameshaingia. Hadi kufikia kesho kila mjumbe anatakiwa awe hapa kwa ajili ya ufunguzi wa mkutano hapo kesho kutwa. Hii ina maana kwamba lazima tufunge kazi takatifu mnamo muda wa masaa sabini na mbili yajayo".

"Hiyo kazi itafungwa katika muda huo wala usiwe na shaka", George alijibu.

"Sasa umeamua nini juu ya watu hawa wawili Dave, ambaye wenzake wanamwita Devil, yaani shetani, aliuliza.

"Watu hawa lazima wauawe usiku huu huu". George alijibu "Kitendo hicho kitawafanya adui wapagawe. na hivyo kutupa sisi nafasi nzuri zaidi kufanya kazi yetu".

"Hali ya ulinzi huko uwanja wa ndege ikoje", aliuliza.

"Ilinzi mkali sana", F.K alijibu. "Na siyo tu kwenye uwanja wa ndege, hali katika mji mzima, wameletwa askari polisi wageni kabisa kutoka mikoa mingine kulinda mkutano. Hivyo ulinzi ni mkali sana.

"Waacheni waonge ulinzi. Jambo hilo lisiwafanye tumbo moto. Ikiwezekana F.K uiambie serikali ya Tanzania ilete jeshi lake zima hapa Arusha na bado cha mtema kuni watakiona tu", Dave alijigamba.

"Paul na Fouche, hiyo ni kazi yenu sitaki Bon na Rocky walione jua litakalochomoza kesho. Mipango yote mnaijua ni kama kawaida", George alisema.

"Hesabu kwamba hiyo kazi imefanyika", Paul alijibu.

"F.K. Nataka unipatie majina ya viongozi wote wa vyama vya wapigania uhuru ambao wameshaingia. Vile vile nataka unipatie majina ya hoteli na vyumba wanakolala. Habari hizi nazitaka leo hii", George alimwagiza F.K.

"Utapata bila matatizo", alijibu F.K.

"Wengine mliobaki nitawaeleza baadaye nini cha kufanya kwa usiku wa leo", George alisema huku akigeuka upande mwingine. Na nyie Paul, Fouche na F.K nataka utekelezaji sahihi kutoka kwenu.

Siku hiyo ilikuwa sikukuu ya Idd-elftri. Mjini Nairobi mchana ule Mike alikuwa ofisini akipokea ripoti kutoka kwa Mwaura.

"Tangu jana mimi na vijana ulionipa tulikuwa tunachunga nyumba hii kwa zamu", Mwaura alisema. "Hata hivyo, hatujagundua kitu chochote. Hakuna mtu hata mmoja ambaye ametoka nje ya nyumba ile. Ila kuna kitu kimoja kinashangaza. Ni kwamba jioni hatumwona Peter akirudi nyumbani. Na Onyango ameniletea habari kuwa amemwona akirudi sasa hivi tunahisi kwamba Peter hakulala nyumbani".

"Unayo hakika hakurudi na kutoka?", Mike aliuliza.

"Labda hiyo iwe wakati tulipokuwa hatujaanza doria wakati wa mchana".

"Hivyo una maana wale watu bado wako ndani?".

"Bila shaka. Labda tu ule muda ambao nilikuja hapa kuwasiliana nawe. Maana kama nilivyokwambia jana, kwa muda ule wa masaa manne hapakuwa na ulinzi", Mwaura alijibu.

"Mike Maina alifikiri sana na kisha akasema. "Sidhani, lakini lazima tuwe na uhakika mtu anaweza kufanya hivyo kama amehisi kuwa tunamfuata".

"Sidhani kama alikuwa ameniona", Mwaura alieleza, "Mimi naelewa kuwa mtu ambaye huchukua tahadhari na mwenye ujuzi kama Peter hawezi kuwa katika hali ile kama alihisi kufuatwa na watu. Bali Onyango aliniambia alipokuwa anarudi leo mchana alionekana kama mtu mwenye wasiwasi kuwa anafuatwa".

"Ndio. Hapa kuna kitu kinanitia wasiwasi sijui ni nini! Mwaura jiweke tayari mnamo saa sita usiku nipitie nyumbani kwangu. Tutakwenda kwa Peter kwani lazima tuhakikishe kuwa mambo gani yanaendelea ndani ya nyumba yake. Waache wale vijana waendelee kufanya kazi", Mike aliagiza.

"Sawa mzee", Mwaura alijibu.

# SURA YA SITA

**MNAMO** saa nne na nusu ndege namba TC 1001 iliwasili kwenye uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro. Willy Gamba alikuwa mmoja wa abiria walioteremka. Alijichanganya na kundi la abiria wenzake mpaka akafaulu kutoka nje ya uwanja bila mtu yeyote kumtambua. F.K, Paul na Fouche walikuwa kwenye kundi la wapokeaji wakichunguza watu kwa makini. F.K hakuweza kumtambua Willy. Mawazo ya Paul na Fouche yalikuwa juu ya Bon na Rocky na hata chembe hawakumfikiria Willy, mbali ya kumtambua.

Alipofika nje ya jumba, Willy alikuta madereva taksi wakigombania abiria. Ingawa taksi za kawaida huwa haziruhusiwi uwanjani hapo, siku ile zilijaa tele. Ziliruhusiwa kwa vibali maalum kutokana na haja ya kuhudumia wageni ambao walikuwa ni wengi sana.

"Oh, mzee njoo huku", teksi dereva mmoja aliyemfahamu Willy alimwita huku madereva wengine wakimwandama na kumsihi apande magari yao.

"Oh, Omari, habari za siku nyingia?", Willy alimsalimia.

"Nzuri tu, mzee, ila wewe tu umepotea", Omari alijibu huku akipokea mkoba wa Willy na kuelekea kwenye gari.

"Sababu ya biashara, bwana. Siku hizi imekuwa ngumu", Willy alijibu.

Wakati walipokuwa karibu kuondoka Willy alisita kidogo.

"Hebu subiri kidogo, kuna kitu nimekumbuka", Willy alisema.

Omari ambaye alikuwa ameliwasha, gari alilizima.

Ilikuwa jambo la kawaida kwa Willy kulitumia gari la Omari. Mara nyingine Omari alimwachia gari Willy aendelee yeye mwenyewe kwa malipo fulani.

Baada ya kupanga na kupangana Willy aliamua kuwangojea wenzake ambao wangekuja kwa ndege ya pili.

"Omari, samahani nitakusumbua, kuna mahali ambapo nataka niende lakini nataka niende peke yangu. Je, sijui kama utaniachia gari yako ili nifanye shughuli yangu? wewe unaweza kupanda gari nyingine", Willy alisema "Mambo mengine kama kawaida yetu".

Bila kusita Omari alikubali ombi la Willy, alijua fika kwamba Willy alikuwa kizito na kila alipochukua gari lake kwa shughuli zake kwa muda mfupi, aliweza kulipwa kiasi ambacho angeweza kukifanyia kazi kwa zaidi ya mwezi mzima.

"Bila shaka", Omari alijibu kwa furaha, Petrol imejaa mzee na gari kama kawaida halina matatizo. Ukisha maliza kazi utanipigia simu kunijulisha hata kama ni baada ya juma zima.

"Ahsante", Willy alijibu huku akichukua swichi ya gari.

Omari alimwaga Willy na kuambaa zake.

Omari aliachana na Willy kwenye maegesho ya magari uwanja wa ndege. Katika gari la sita katika safu kutoka alipokuwa Willy. F.K. pamoja na wenzake walikuwa wamekaa ndani. Walifanya hivyo ili kusubiri maadui zao ambao wangefika kwa ndege ya pili.

"Mimi nafikiri niwaache maana hakuna usalama tukionekana pamoja. Nisingependa mambo yetu yagundulike kabla hata kazi yetu hatujaianza", F.K. aliwashauri wenzake.

"Wewe nenda, kazi hii sisi ni saizi yetu, mambo yote tuliyotaka umefanya. Kazi yako umemaliza", Paul alimruhusu.

"Nawatakia bahati njema", F.K aliwaambia huku akiondoka kuelekea kwenye gari lake jingine ambamo Tondo alikuwa anamsubiri.

"Ahsante", PAul alijibu.

Bila kujua, Willy. Paul na Fouche walikuwa wakisubiri wageni wale wale, lakini kwa nia na madhumuni tofauti.

Ndege iliwasili mapema kuliko ilivyotarajiwa. Ilifika saa tano kasoro dakika kumi.

"Ndege hii imewahi kuondoka Dar", Willy alijisemea moyoni huku akiwa tayari kwenda kuwapokea wenzake.

Paul na Fouche walitoka kwenya gari lao mara moja na kwenda kujichanganya tena na wapokeaji wengine waliofika kuwalaki wenzao.

Ndege ilisimama na abiria wakatelemka kama kawaida.

Willy aalikuwa tayari amejigeuza kimawazo na kimazingira kutokana na ujuzi pamoja na uzoefu wa muda mrefu katika kazi hii. Alijibanza katikati ya nguzo

moja kama asiyekuwa na hili wala lile. Hata hivyo aliweza kumwona kila mtu aliyetoka nje ya jumba la uwanja kutoka pale aliposimama. Paul na Fouche pia, wakitumia ujuzi wao walijitosa kwenye vurugu la wapokeaji kiasi kwamba hakuna mtu ambaye angewahisi chochote. Hii ilitokana na kwamba wao hawakuwa wazungu peke yao hapo uwanjani. Watu waliotoka kwanza ni wale waliokuwa wanasafiri bila mzigo mikubwa.

Hatmaye Rocky Malele alitokea. Paul alimgonga Fouche begani na wote wakamtambua Rocky. Willy nae alimwona Rocky lakini akaendelea kubana. Rocky aliangaza huku na kule kisha akaamua kupanda Kombi ya shirika la Taifa la Huduma za Kitalii.

"Wakati kama huu wa usiku ni vizuri kupanda gari la watu wengi kwa tahadhari na usalama", Rocky alijisemea.

Kulikuwa na watu wengine ndani ya gari hili lakini lilikuwa bado kujaa. Hivyo iliwabidi kusubiri abiria wengine zaidi. Paul, Fouche na Willy Gamba walimwona Rocky akipanda gari hilo. Ingawa Paul na Fouche hawakujuana na Willy. Wote waliendelea kumsubiri Bon atokee.

Lakini jambo la kushangaza ni kwamba Bon hakutokea. Pande zote mbili zilitarajia kuwa angefika kwa ndege hii. Lakini kwa mshangao mkubwa Bon hakuonekana kamwe.

Willy ambaye alikuwa anachunguza nyendo za hapa kwa makini, aliona wazungu hawa wawili wanaondoka na kuelekea kwenye gari lao. Katika akili yake Willy alifikiri kitu fulani kilichojitokeza kama hakieleweki. Ilikuwa kwamba Willy aliwaona wakati anafika. Na sasa alikuwa amewaona tena Wazungu wale wale. Ilionekana kama kwamba nao pia walikuwa wanasubiri mgeni ambaye hakuwasili kwani wao pia walikuwa wa mwisho.

Pamoja na hayo, Willy alijisemea, "Lakini inawezekana walikuwa wamekuja kuwapokea wageni wao halafu wakakuta hawakuwasili. Hii inawezekana na haina ubaya wowote".

Hata hivyo Willy aliamua kufuatilia nyendo za Wazungu hao. Aliwaangalia wakiingia kwenye gari naye pia aliamua kuingia ndani ya gari lake. Mara gari alilokuwemo Rocky liliondoka.

"Tulifuate gari hilo", Paul alimwambia Fouche ambaye alikuwa anaendesha.

"Itakuwa vigumu kulishambulia gari hili; ingekuwa vizuri kama angekuwa amechukua teksi yeye peke yake", Fouche alieleza.

"Kuna wakati atabaki peke yake. Usiwe na wasiwasi kwani tunayo siku nzima ya kufanya kazi hii", Paul alijibu.

Gari la akina Rocky lilifuatwa na gari moja, halafu lilifuatwa na gari la akina Paul na Fouche. Willy alisubiri gari lingine lifuate ndio naye aweze kujiunga na msafara. Alipotaka kuondoka aligundua kuwa tairi mbili za nyuma hazina upepo!

"Shenzi", Willy alilaani.

Wakati F.K anawaaga Paul na Fouche ili aende kwenye gari alilokuwa ameegesha Chris Tondo, Chris Tondo alikuwa amemwona Willy Gamba akitoka nje ya uwanja na kumtambua. Vile vile wakati Chris Tondo alipokuwa ofisa wa polisi aliwahi kumfahamu Willy kikazi na kimaisha. Kwa upande mwingine, Willy hakumweka Chris Tondo maanani. Hivyo alikuwa hawezi kumkumbuka.

"Nimemwona Willy Gamba", Tondo alimwambia F.K.

Aliposikia hivyo F.K alishituka kwani alimfahamu Willy kutokana na umaarufu wake kama nilivyokwisha kusimulia.

"Oh, yuko wapi?", liuliza F.K kwa mshangao mkubwa.

"Namwona anangojea ndani ya teksi ile".

"Basi, bila shaka na yeye anawasubiri", F.K alisema.

"Anawasubiri akina nani?", Tondo aliuliza.

Pamoja na mambo yote ambayo Tondo alikuwa anayafanya kwa wizi nzima, F.K alikuwa hajamweleza kinagaubaga operesheni hii ilikuwa ya namna gani. Baada ya kufikiri kwa muda aliona ni vyena amweleze habari zote kwani kumficha Tondo kungeweza kusababisha makosa ambayo yangeweza kuleta hatari kubwa, hasa kwa wakati kama huu.

"Unajua Tondo, wewe nakuchukulia kama ndugu yangu. Ni mtu ambaye nakuamini katika maisha yangu. Hivyo wakati umefika na mimi kukueleza kinaganaga juu ya shughuli yote hii", F.K alimwambia Tondo na kisha akamweleza juu ya operesheni hii kuanzia mwanzo mpaka mwisho, kisha alisema. "Hivyo umefika wakati wa kulipa kisasi dhidi ya serikali ya Tanzania kama ulivyowahi kuahidi. Bila shaka utakuwa upande wetu".

"F.K wewe ni ndugu yangu. Mimi niko pamoja nawe. Naahidi kuwa nitatumia ujuzi wangu wa kipolisi kikamilifu ili nilipize kisasi changu cha kunionea na kunifedhehesha ", Tondo aliahidi.

Hivyo F.K na Tondo walibaki ndani ya gari lao wakimchunguza Willy alikuwa anafanya nini. Wakati ndege ilipwasili na Willy akatoka kuelekea mahali alipojibanza ili kuwaangalia akina Riocky. Tondo aliteleza gizani mpaka kwenye gari la Willy. Hapo hapo alitoa upepo kwenye matairi mawili ya nyuma.

"Nimemweza", Tondo alijigamba huku akirudi kwenye gari.

"Kazi hii itakuwa kubwa", F.K alisema. "Itakuwa ni vita vya kutafutana. Vita kwa akili na ujuzi kwani wapelelezi mashuhuri wa Afrika naona wako hapa. Heri sisi tutangulie tuwape habari wenzetu halafu tujitayaruishe kwa ajili ya mapambano makali. Hapa tulipo hatuna hata silaha yoyote. Kama tunapenda kuiona kesho tumkwepe Willy. Kazi tuliyofanya inatosha kwa leo. Willy anaweza kusubiri mpaka kesho. Waache Paul na Fouche nao wafanye kazi yao. Kesho tutakuwa tayari kumumaliza Willy. Hata yeye mwenyewe ataingiwa na woga baada ya kusikia wenzake wameuawa".

"Nafikiri tungoje tuone kama Willy alikuwa anawasubiri wenzake", Tondo alisema. "Ikiwa ni hivyo itakuwa rahisi kwa Paul na Fouche kuwamaliza wote kwa wakati mmoja".

"Sidhani, hawawezi kusafiri wote pamoja, Tondo", F.K alipinga usemi. "Mimi ni jasusi na mchezo huu naufahamu. Paul na Fouche wanajua sana mchezo huu pia. Hivyo wao waachie, wewe ni mchezaji wa ridhaa. Katika shughuli hii ya kijasusi vizuri kuwaachia wajuzi. Achana na Willy huyo atakuwa nyama yetu kesho".

Tondo aliwasha gari na kujipenyeza kwenye msururu na kuondoka.

Wakati Tondo anatoa upepo kwenye tairi za nyuma za gari la Willy. Lyimo alikuwa sehemu ile. Lyimoa alikuwa mwizi mkubwa. Wizi wake alifanya wa kuvunja magari yaliyoegeshwa na kuiba vitu vilivyomo ndani. Siku ile alikuwa katika pilika zake hapo uwanja wa ndege wa Kilimanjaro, baada ya kusikia magari mengi yangekuwa hapo. Wakati huo Lyimo alikuwa hajabahatisha kitu chochote. Alikuwa amejibanza kwenye gari karibu na lile la Willy. Ndani ya gari lile Lyimoa alikuwa ameona mkoba ambao alikuwa anaunyemelea. Alikuwa anajaribu kufungua mlango wa nyuma. Mara alisikia mtu anasogea karibu na gari lililokuwa jirani. Aliinuka kidogo na kuchungulia. Alimwona mtu anakuja kwa kunyata. Kwanza kabisa Lyimo alifikiri yule alikuwa mwizi mwenzie. Lakini sura yake

pamoja na jinsi alivyokuwa ilionyesha kinyume. Aliona huyo mtu anatoa upepo kwenye gari halafu kunyata na kuondoka.

Lyimo aligundua kwamba gari lile lilikuwa teksi ya Omari ambaye anamfahamu sana. Ili kuchunguza vizuri kisa hiki Lyimo alimfuatilia yule mtu na kuona gari alimoingia. Alichukua kalamu yake na kuandika namba za gari hilo kwenye kiganja chake cha mkono. Akitarajia kumweleza Omari kana angetokea. Mara nyingine Omari alikuwa akimsaidia. Safari hii aliona amepata nafasi ya kulipa ukarimu wake angalau kwa ishara hiyo ndogo.

"Mimi ni mwizi", Lyimo alijisemea moyoni. "Ninaiba ili nipate fedha za kunifanya niishi. Lakini watu wengine ni waharibifu tu. Kwa mfano mtu huyu amemsumbua mwenzake bure. Afadhali mara mia angekuwa na nia ya kuiba kitu".

Mshangao wake ulizidi alipoona lile gari linaondoka kuelekea mjini.

Wakati Willy alipokuwa anaangalia matairi, Lyimo alitokea."Habari gani, mzee", Lyimo alimsalimia Willy kwa heshima.

"Nzuri", Willy alijibu huku akimwangalia Lyimo kwa makini. Kisha aliendelea, "Ngoja kidogo".

Willy alisogea mbele na kuandika namba za gari la Wazungu lililokuwa linapita mbele yake halafu akarudi.

"Eh, unasemaje?", Willy alimsaili Lyimo."Mwenye gari hii ni rafiki yangu. Siyo gati la Omarui hili", Lyimo aliuliza.

"Ndio, na mimi ni rafiki yangu. Ameniachia gari hili. Lakini ajabu nimekuta limepata pancha mbili sasa hivi", Willy alijibu.

"Nimeona mtu anatoa upepo ndani ya matairi haya", Lyimo alieleza.

Mara Willy alisikia kengele zinalia kichwani mwake.

"Eh, mtu wa namna gani?", Willy aliuliza kwa shauku kubwa.

"Mtu mmoja nadhifu sana. Mwanzo nilifikiri ni mwizi. Lakini hakuonyesha dalili ya wizi. Aliinama, akatoa upepo na kuondoka. Aliingia kwenye gari ambalo lilikuwa na mtu mwingine ndani halafu wakaondoka zao. Hata hivyo, mimi nilichukua nambari za gari hilo ambayo ni ARKK 567", Lyimo alimwambia Willy huku akisoma kwenye kiganja chake.

Willy alikariri nambari hiyo na kushangaa, kwa kujiona alikuwa na bahati iliyoje.

"Wewe unaitwa nani?", Willy aliuliza

"Naitwa Lyimo".

"Na wewe ni dereva wa teksi?".

"Hapana, mimi ni shanta".

"Shanta maana yake nini?".

"Mimi huwa nawasaidia madereva kama wanao usingizi. Huwa naendesha halafu wao huwa wananilipa chochote", Lyimo aliongopa.

Wakati huo akili ya Willy ilikuwa inafanya kazi haraka haraka. Mara alipata jawabu.

"Ninaweza kupata gari nyingine hapa?".

"Subiri niangalie", Lyimo alijibu na kuondoka.

Punde si punde Lyimo alirudi na kijana mmoja.

"Huyu anaitwa Tarimo, ni rafiki yangu vile vile, hata Omari ni rafiki yake pia", Lyimo aliwajulisha.

"Aah, mimi naitwa Willy. Omari ni rafiki yangu. Kiniachia gari lakini nimepata mkasa".

"Sasa unataka tukusaidie vipi?", Tarimo aliuliza.

"Unayo pampu?".

"Ndio", Tarimo alijibu.

"Nafikiri kama utakubali utanipatia gari lako, mimi nitakulipa shilingi elfu tatu. Weka upepo kwenye gari la Omari halafu tuonane kesho asubuhi huko New Arusha Hoteli. Gari lako utalikuta hapo".

Bila kuchelewa Willy alianza kutoa fedha na kumhesabia Tarimo. Tarimo aliona kama ameangukiwa na ngekewa. Alichukua fedha na huku Lyimo akibeba mizigo ya Willy, wakielekea kwenye gari.

"Lyimo umenisaidia sana. Chukua hizi shilingi tano ukanywe angalau bia moja", Willy alimwambia Lyimo.

"Lo! ahsante sana. Leo siku nzima nilikuwa sijapata kitu. Mungu akuongezee.

"Amina", Willy alijibu huku akifikiria namna Lyimo alivyokuwa amemsaidia bila kujua.

"Kesho asubuhi", Tarimo alisema.

"Kesho asubuhi", Willy alijibu na kuondoka.

"Sasa ni lazima niyakamate yale magari", Willy alijisemea moyoni.

Gari la Tarimo lilikuwa aina ya Peugeot 404 lenye umri kidogo. Lakini lilikuwa na nguvu ya kutosha. Tangu yale magari yaondoke ilishapita muda wa dakika kumi na tano. Willy alilipamba moto na kuendesha kwa mwendo mkali sana. Wakati akiendesha Willy alifikiri mambo yote haya. Na ajabu zaidi, Willy alimfikilia Bon Sipele ambaye alikuwa hakuonekana hapo uwanja wa ndege.

Karibu na mpakani, katikati ya sehemu ya Tengeru, nje ya mji wa Arusha. Willy aliyafikia magari yaliyokuwa yametangulia. Alilipita gari moja ndipo akaliona lile lililokuwa linaendeshwa na wazungu. Vile vile aliona ile Kombi iliyombeba Rocky. Hivyo aliamua kubana nyuma ya magari hayo.

Kituo cha kwanza cha ile kombi kilikuwa Saba Saba Hoteli. Rocky alikuwa amemwambia Willy kuwa angefikia Equator Hoteli. Alipofika Sabasaba Hoteli na kuona ile kombi pamoja na gari la wazungu vikiongoza kwenda hoteli hiyo, yeye Willy aliamua kwenda moja kwa moja akabane Equator Hoteli. Alifanya hivyo ili akaone kama alivyofikiri ilikuwa kweli. Akiliwa ameegesha gari katikati ya magari mengine karibu na Safari Hoteli, aliona ile kombi inasimama pale Equator Hoteli. Watu watatu wakiwa na mizigo walitelemka. Rocky alikuwa mmoja wapo punde si punde, Willy aliona gari lile la wazungu linaegeshwa karibu na Hoteli hiyo hiyo. Lakini kwa upande mwingine wa barabara.

Mzungu mmoja aliondoka na kuelekea huko Hotelini. Willy alisubiri. Baada ya kama dakika kumi hivi, yule Mzungu alirudi na kuingia ndani ya gari. Willy aliendelea kusubiri. Alipoangalia saa yake ilisema saa sita usiku.

Ilipofika saa saba usiku Paul alimwambia Fouche, "Sasa twende, mimi nitapita kwa nje wewe utapita kwa ndani. Kama nilivyokueleza, chumba chake kiko kwenye pembe ya kulia. Huwezi kukikosa kwani ni moja kwa moja. Mimi nitaingilia dirisha la bafuni ambalo ni kubwa la kutosha. Bila shaka atakuwa amelala".

Waliondoka ndani ya gari na kutokomea gizani, Willy naye aliondoka kwenye gari baada ya kuwaona wanafanya hivyo. Alifanya hima kuelekea kwenye kijumba cha simu kando ya barabara. Alipiga simu Equator Hoteli kwani aliyokuwa anatuhumu yajidhihirisha kuwa ni kweli.

"Hallo, Equator Hotel?", simu iliitika.

"Nipe mapokezi", Willy aliomba.

"Mapokezi hapa", Willy alijibiwa baada ya muda kitambo.

"Rocky Malele yupo chumba gani?", Willy aliuliza.

"205".

"Nipe nizungumze naye".

Baada ya muda kidogo, sauti ya Rocky ilisikika.

"Hallo, Rocky hapa".

"Willy hapa", Willy aliitika na kisha aliendelea, "Chunga tai wawili wanataka kula nyama yako sasa hivi".

"Chunga", Rocky aliitikia huku akiweka simu chini.

Aliamka haraka kutoka kitandani na kuchukua bastola yake kutoka chini ya mto. Aliikagua.

Willy naye alitoka kwenye kibanda cha simu, akaigusa kwa chati bastola yake huku akimwemwesa.

Ilikuwa saa saba za usiku. Mjini Nairobi Maina na Mwaura walipanda ua na kuingia ndani ya uwanja wa jumba hili la kifahari la Peter Gerrit. Waliangaza na kumwona mlinzi aliyekuwa bado amekaa kwenye kijumba chake huku akisinzia sinzia. Walizunguka nyumba kwa uangalifu mkubwa ili waweze kupata mahali pazuri pa kuingilia.

"Wewe zungukia kulia na mimi nizungukie kushoto, kisha tukutane mbele", Maina alimweleza Mwaura. "Jaribu kuangalia mahali pazuri pa kuingilia".

"Sawa, Mzee".

Walipokutana, Mwaura alimwambia Maina. "Kuna mlango pembeni. Nafikiri unatokea jikoni. Unaonaje tukiingilia huko?".

"Funguo zako unazo?".

"Ndio".

"Na! kufuli ni la aina gani?".

"Ni la kawaida. Nitafungua, hamna taabu", alijibu Mwaura.

Huku kila mtu akiwa ameweka bastola yake tayari, walifungua mlango huo. Mara walijikuta wako jikoni. Wafungua na kujikuta kwenye chumba kikubwa. Walihisi hicho kilikuwa chumba cha chakula. Kwani humo ndani kulikuwemo meza kubwa iliyozungukwa na viti visivyopungua kumi na nane. Wakifanya tahadhali kubwa, walisonga mbele . Walikwenda wakiangalia chumba hadi chumba. Jumba lenyewe lilikuwa kubwa kiasi cha mtu kuweza kupotea.

"Shiii!", Maina alimtahadhalisha Mwaura.

Alifanya hivyo kwa sababu alikuwa amesikia kitu kama mashine ya teleksi inalia kutoka kwenye chumba alichokuwa amekitazama. Huku akimuonyesha ishara abaki nyuma ili aweze kumsaidia iwapo ingetokea shida yoyote, Maina alifungua mlango ule. Mle chumbani hakukuwa na kitu, lakini bado alisikia mlio wa mashine ukizidi. Aliangaza huku na kule ndipo, kutokana na uzoefu wa kazi yake wa siku nyingi, alipouona mlango aliokuwa akiutafuta. Alibonyeza kifungo hapo ukutani na mlango ule ukafunguka. Mwaura alichungulia huku moyo wake ukipiga haraka haraka. Mara alimwona Maina anamuonyesha ishara ya kumfuata baada ya muda mfupi. Aliingia ndani na kuurudisha mlango.

Alikuta ngazi zinazoelekea chini ambazo alizifuata. Sasa alikuwa na hakika kabisa ndani ya jumba hili kulikuwamo makubwa. Alichunguza bastola yake ya kawaida na ile ya akiba. akajiweka tayari wakati akizidi kutelemka chini.

# SURA YA SABA

**ALIUFIKIA** mlango mwingine. Huku ameweka bastola yake tayari, aliufungua. Hapo alijikuta kwenye ukumbi mkubwa uliomuonyesha kuwa alikuwa kwenye sehemu za maofisi. Alitega tena masikio yake vizuri. Ndipo alipogundua ni chumba gani ambacho mlio wa mashine ulikuwa ukitokea.

Aliangaza huku na kule na kusikia kimya, alianza kufungua ule mlango. Kwanza alifungua kidogo kiasi cha kuweza kuangalia ndani. Aliona Wazungu watatu wakiangalia mashine kubwa ya komputa ikileta habari. Wawili walikuwa wamesimama na yule aliyekaa Maina alimtambua kuwa ni Peter Gerrit. Aliweza kumtambua kwani waliwahi kuonana wakati wa upelelezi kuhusu mauaji yaliyotokea katika Visiwa vya Shelisheli.

Alirudisha mlango kidogo, akafikiri, halafu akaufungua ghafla na kwa nguvu.

"Hapo hapo mlipo!", Maina aliamru kwa sauti kali. "Mtu akileta ushenzi amekufa!. Mikono juu!.

Waligeuka na bila kubisha wakainua mikono juu. Bila kupoteza wakati. Maina alisoma maandishi yaliyokuwa kwenye ile mashine:

"LAZIMA UTUONGEZEE WATU MAANA HATUTAKI KUSHINDWA IKIWA HATA HUYU GAMBA YUKO HAPA HAPA JIBU".

Ghafla maandishi yalifutika.

"Peter, jibu", Maina alimwambia Peter.

"Nijibu nini".

Wakati huo Maina alikuwa tayari amewafikia na kuwapekuwa ili kuhakikisha kama walikuwa na silaha. Alikuta wale Wazungu wengine wanazo bastola ambazo aliwanyang'anya na kuzitupa kando.

"Maina mbona unanifuata fuata. Kazi inaitaka ama huitaki".

"Naitaka Peter, na safari hii huwezi kunipo...".

Ghafla chumba kikawa giza Maina alijirusha kutoka aliposimama na kuanguka kando. Wakati huo huo risasi zikamiminika pale alipokuwa amesimama. Naye alijibu mapigo huku akijiviringisha chini."Oh, nakufa", sauti ya mtu ilisikika.

Watu waliobaki walifungua mlango na kukimbia nje. Huko alisikia risasi zinalia na akajua Mwaura alikuwa kazini.

Aliinuka haraka na kufungua mlango wa ukumbini alikuta maiti nyingine mbili. Aliamua kuelekea sehemu aliyosikia mlio wa risasi. Mwaura alikuwa amefanya kazi kubwa. Mara aliona maiti nyingine moja. Mambo yalikuwa yanakwenda haraka. Kumbe sehemu hiyo pia kulikuwa na ngazi nyingine. Maina alizifuata ngazi hizo. Mwisho wa ngazi chini alimkuta Mwaura ameanguka chini baada ya kupigwa risasi ya kifua.

"Bosi, wamebaki wawili tu, wawahi, Mwaura alisema kwa maumivu.

"Mwaura! Mwaura!", Maina aliita kwa uchungu. Mwaura aligeuza macho na kumtazama Maina, kiasi akakata roho.

Machozi yakamtililika Maina.

"Umekufa kishujaa, Mwaura, mimi nitakulipizia kisasi. Natoa ahadi.

Kwa haraka alikimbia kumfuata Peter lakini alikuwa amechelewa. Kwani alisikia gari linawashwa na kuondoka. Kwa kasi.

Alirudi ukumbini ambamo kuliwa na simu. Alimpigia Mkurugenzi wa Upelelezi nyumbani kwake.

"Ni nani...?", Mkurugenzi aliuliza kwa sauti ya kulalamika. Lakini maelezo ya Maina yalifuta mawazo yake.

"Peter amekimbia. Mwaura ameuawa katika mapambano. Majasusi sita wameuawa. Maiti zote ziko hapa nyumbani. Naomba Polisi wafike haraka ili waweze kuchukua ushahidi ambao ni mkubwa na wa uwazi. Vile vile viwekwe vizuizi kwenye barabara zinazotoka mjini hapa. Wasiliana na wenzako huko Tanzania. Nataka kujua Willy Gamba yuko wapi".

"Sawasawa. Tuonane ofisini saa kumu na mbili. Nafikiri hapa kuna kazi kubwa", Mkurugenzi alijibu.

"Kwaheri, mzee", Maina alijibu halafu akaweka simu chini na kuondoka.

Fouche alikwenda katika sehemu ya mapokezi ya Equator Hoteli. Mhudumu wa mapokezi alikuwa akisinzia sinzia pale kwenye kiti.

Aliangalia kwenye bodi ya funguo na bila kusita akamwambia mhudumu. "Chumba mia mbili na ishirini".

Yule kijana bila hata kugutuka alichukua funguo. akampatia na kuendelea kustambari.

Fouche alipanda mpaka ghorofa ya pili na kwa tahadhali kubwa alielekea chumba namba 205.

Paul alizunguka na kuuangalia ukuta. Alivaa mifuko yake ya mikono. Mifuko hiyo ilikuwa ya aina yake, kwani iliweza kushika ukutani kama sumaku. Hivyo ilimwezesha kupanda ukuta bila matatizo. Aliangalia saa yake halafu akaanza kukwea.

Baada ya Rocky kupata simu ya Willy, aliyomtahadharisha, alitengeneza kitanda chake vizuri. Alikunja Blanketi na kuifunika na shuka mpaka ikaonekana kama mtu aliyelala. Baada ya kufanya hivyo, alibana mahali na kusubiri.

Akiwa katika hali ya kunyata. Willy alijipenyeza kwenye njia kati ya Equator Hoteli na Jengo la posta kwa upande wa kulia. Kwa haraka akamuoana mtu anaelekea kwenye ukuta. Mara akahisi ni nani. Aliendelea kunyata haraka haraka mpaka akafikia usawa wa mtu yule ambaye sasa alikuwa amekaribia kushika dirisha.

"Shiii", Willy alitoa sauti ya kustua mtu.

Paul aligeuka kumtazama mtu aliyetoa sauti hiyo. Kutokana na mwanga wa mbalamwezi. Paul alijikuta anatama kwenye mdomo wa bastola.

Willy alimwamru atelemke. Vinginevyo angemkita risasi ya matako. Kufumba na kufumbua, Paul alifyatuka kama risasi na kumwangukia Willy. Willy alipiga risasi ambayo ilimkosa Paul na wote wakaanguka chini. Bastola ya Willy ilidondoka umbali wa kama futi sita kutoka mahali walipokuwa. Hapo ndipo vita vya ana kwa ana vilipoanza. Willy alitaka kupiga mbio kuelekea kwenye bastola. Lakini Paul aliwahi kumrukia kwa pale pale chini. Hata hivyo, Willy alimpiga teke-farasi na Paul akaanguka upande mwingine lakini akaamuka mara. Hapo ndipo walipogundua kuwa walikuwa wamekutana wajuzi watupu.

Hapo mwanzo Paul alikuwa amefikiri huyu alikuwa askari wa kawaida, lakini sasa alikuwa na mawazo tofauti. Kupambana naye bila kutumia silaha isingewezekan. Alijaribu kutoa bastola yake iliyokuwa kwenye mkoba wake chini ya kwapa. Lakini Willy aligundua janja yake. Alimwahi kipigo cha karate kilichomfanya Paul aone nyota. Pale pale Paul alitoa mapigo manne ya karate haraka haraka. Lakini Willy aliyaona. Willy alimgeuzia Paul na kumpiga teke la kinena lililomwangusha

chini. Alimrukia ili amumalize kabisa. Lakini Paul alijiviringisha kando na Willy akamkosa.

Lakini alijiviringisha tena kabla ya kutua na kumwahi Paul ambaye wakati huo alikuwa amechomoa bastola. Aliipiga teke ile bastola nayo ikafyatuka wakati ikitoka mikononi mwa Paul. Teke lile lile lilikuwa limevunja mkono wa Paul wa kulia. Paul aliamka ili akimbie, lakini Willy alimwahi kwa kumpiga ngwara. Alipoanguka chini Willy alimpiga Paul teke ambalo lilimvunja mbavu kama tatu hivi za upande wa kulia na hapo hapo moto ukamwishia. Akabaki kugwaya.

"Nyinyi ni nani?", Willy alimwuliza Paul, huku amembana pale chini asiweze kufurukuta.

"Sisi ni Wazungu", Paul alijibu kwa jeuri maana alijua huo ndio mwisho wa maisha yake, haraka sana alifikiri jinsi alivyokwisha waweka watu wengine katika hali kama aliyokuwemo kwa sasa hivi. Kwa mara ya kwanza kati maisha yake alijiwa na woga na hali ya kuogopa kifo. Hata hivyo alijuwa huo ndio ulikuwa mwisho wake kwani hapakuwa na ujanja wa kuokoka.

"Wenzako wako wapi?", Willy aliuliza kana kwamba alikuwa akijua.

"Niko peke yangu tu", Paul alijibu huku akisikia maumivu makali kutoka mbavuni.

"Aah, kumbe bado unafanya mchezo", Willy alitishia.

"Kama ni kuniua si uniue tu?, unataka nini zaidi", Paul alimuuliza Willy.

"Kwanza ujibu maswali yangu, vinginevyo bado unayo safari ndefu ya kwenda ".

"Hutapata jibu hata chembe, unapoteza muda wako".

"Basi, kama wewe ni Kaburu leo umefika kwa wazalendo wa Afrika. Utakiona cha mtema kuni. Kama hutaki kifo chako kisiwe cha maumivu makali bora uanze kusema", Willy alimwambia huku akigandamiza mbavu za Paul zilizovunjika.

Paul alisikia maumivu makali ambayo alikuwa hajawahi kusikia. Lakini pamoja na uchungu wote ilikuwa ni sheria ya 'KULFUT' kwamba hakuna askari wake kutoa siri bali kutafuta njia ya kujiua ili kupunguza muda wa mateso.

"Sema wenzako wako wapi, Kaburu wee", Willy alimuuliza huku akizidi kumbana mbavu kwa kukandamiza mkono wake.

Mara alishitukia Paul anatoa ulimi wake nje ghafla halafu akaukata kwa meno yake kama mkasi.

"Shenzi mkubwa we!", Willy alitukana.

Kaburu alikuwa ameamua kujiua kwa njia ya ajabu sana.

"Kweli tunayo kazi maana Majasusi hawa wa Makaburu siyo watu wa kawaida", Willy alijisemea moyoni.

Fouche aliendelea kuziparamia ngazi kana kwamba naye alikuwa mgeni aliyefikia chumba namba 205, aliangaza huku na kule, halafu akatoa bastola yake na kujiweka tayari. Kama ilivyo desturi, bastola yake ilikuwa na kizibo cha kuzuia sauti. Alichukua funguo zake malaya akafungua kufuri la mlango.

Rocky, ambaye alikuwa ndani amezima taa lakini akiwa amevuta pazia kuacha mwanga wa mbalamwezi uingie kidogo, alisikia kwa mbali kufuli likifunguliwa. Hivyo alijiweka tayari.

Fouche alikuwa amelidhika kwamba kufuri halikupiga kelele. Hivyo alishika komeo. Kwa kasi ya umeme. Fouche alifungua mlango na moja kwa moja akamimina risasi kama kumi pale kitandani. Halafu aliingia chumbani na kuwasha taa huku akiangaza kitandani.

"Umefanya kazi nzuri", Rocky alisema kwa sauti ya kebehi.

Fouche aligeukia kule sauti ilikokuwa inatokea na pale pale akawa amegundua jinsi alivyokuwa amedanganywa. Alijuwa mambo yamekuwa mambo. Hivyo alifyatua risasi lakini Rocky alikuwa tayari amekaa imara. Alimpiga Fouche risasi moja ya kifua akaanguka chini. Alipomkaribia alimkuta kawa maiti tayari.

"Mara Rocky akasikia kitu kinadondoka bafuni. Aliruka ili azime taa. Hapo hapo mlango wa bafuni ukafunguliwa kama radi kabla hajazima taa. Huku bastola zikiwa zimeelekezana. Alishangaa kumwona Willy.

"Chunga sana. Willy", Rocky alisema. "Siku nyingine unaweza kuumia.

"Mimi nafikiri wewe chunga zaidi; ongeza kasi", Willy alijibu.

Wote wakacheka.

"Umempiga sachi ?", Willy aliuliza huku akiangalia maiti ya Fouche.

"Zaidi ya hii bastola yake", Rocky alijibu. "Hana kitu kingine".

"Hata yule wa nje hana kitu", Willy aliongeza Rocky alielewa mara moja.

"Hivi ulijuaje nia ya watu hawa?", "Kama si wewe Willy, mimi ningekuwa maiti hivi sasa.

"Hiyo ndio faida ya kuwa wengi", Willy alisema. "Hebu chukua vitu vyako tuondoke hapa. Nitakueleza zaidi huko njiani".

Waliondoka chumbani humo kwa kupitia dirishani.

Ilikuwa saa moja asubuhi wakati F.K alipoegesha gari lake. Huku nusu akitembea nusu akikimbia , aliingia nyumbani. Majasusi wote walikuwa wanamsubiri kwa hamu.

"Eh imekuwaje?", George aliuliza.

"Paul na Fouche wameuawa!", F.K alijibu.

"Nini?", Dave aliuliza kwa ghadhabu.

"Wamekufa", F.K alieleza. "Polisi wanasema maiti zao zimekutwa Equator Hotel. Sasa hivi Polisi wanafanya upelelezi kwani watu hawa hawana rekodi kuhusu kuwa kwao nchini. Zaidi ya hayo, hakuna jibu lolote kutoka kwa Peter Gerrit, sijui kumetokea nini!".

"Mungu wangu, maana hata Peter ameuawa?", Dave aliuliza.

"Sijui, lakini hakuna jibu. Hivyo wanahisi kuna kitu kimetokea".

"Oke, sasa kazi imeanza. Katika mchezo huu mambo kama haya sharti yatokee. Hivi Bon na wenzake wametupiku. Sasa ni zamu yetu kufunga kazi; F.K kazi yetu ya usiku wameisha izungumzia? George aliuliza.

"Kati ya wale watu wawili ni ofisa mmoja wa wapigania uhuru ambaye ameuawa. Yule wa sabasaba Hoteli alikuwa mfanyabiashara. Kwa hiyo hicho chumba kimekosewa", F.K alijibu kwa sauti ya uwoga.

"Nafikiri ni lazima uifanye kazi yako vizuri, F.K sharti ulete habari sahihi maana kazi kubwa iko leo usiku. Kusema kweli kama mtafanya mchezo mtateketea nyote. nyinyi wenyewe mmeona jinsi Paul na Fouche walivyoangamia. Inatubidi kujidhatiti na kufunga kazi haraka. Jambo moja lazima niwahakikishie; hakuna kushindwa, sawa?", George alisema kwa ukali.

"Sawa", wote walijibu kwa pamoja.

"Oke, tuendelee na maelezo kuhusu mipango ya mashambulizi ya siku nzima", George alishauri.

Wote walisogea ili kila mmoja wao ajue kazi yake na jinsi ya kuitekeleza.

Saa tatu juu ya alama Bon Sipele alibisha hodi kwenye chumba cha Willy, huko New Arusha Hotel, kama walivyokuwa wamepanga jana yake.

"Hakllo vipi", Bon alimsalimia. Rocky alikuwa amejilaza kitandani.

"Wewe ni mchawi nini?, ulipotelea wapi?", Willy aliuliza.

"Wewe mwenyewe unajuwa kwamba kujibadilisha kama kinyonga na kuwapotea watu ndio mchezo wangu", Bon alijibu kwa mzaha.

"Hivi ulipita pale pale? Sidhani. Hata mimi nisikutambue?", Willy aliuliza kwa mshangao.

"Mimi nilikuona umejibanza kwenye nguzo. Nikakurushia busu la uzima halafu nikawahi kwenda kulala ili leo niamke safi", Bon alijibu.

"Si kitu. SItaki kujua ulitoka vipi", Willy alisema. "Inatosha kukuona mzima kwani tulikuwa na wasiwasi huenda umetekwa nyara. Huo ukinyonga wako uweke iwe siri yako, kwani huenda utakufaa baadaye. Maana kusema kweli ulitupotea kishenzi. Hapo hata mimi nimevua kofia".

"Eh, vipi, mbona kama kwamba nyinyi nyote mmelala humu maana naliona sanduku la Rocky Equator Hoteli ilijaa", Bon aliuliza.

"Ilijaa?", Rocky alidakia, "Hebu Willy mpashe kabla hajauliza mengi".

"Sisi bado hatujalala kama wewe. Mpaka sasa lazima ujuwe kwamba majasusi wameshaingia hapa. Zaidi ya hayo, jana usiku tumepambana nao!", Willy alianza kumweleza yote yaliyotokea usiku ule.

Bon alisikiliza kwa mshangao mkubwa.

Ilikuwa saa mbili na nusu asubuhi. Peter Gerrit alikuwa anazungumza na maafisa wa Uhamiaji na Ushuru wa Forodha wa upande wa Tanzania. Alidai alikuwa anakwenda Arusha kuhudhuria mkutano wa wapigania uhuru. Paspoti yake ilimtambulisha kama Askofu Peter Jackson kutoka Zimbabwe. Alipitishwa haraka haraka bila kushukiwa. Wakati ule ule Mike Maina alikuwa na mazungumzo ofisini kwa Mkurugenzi wake ofisini.

"Kama Willy yuko Arusha, basi wasiwasi wangu umekwisha", Mike alisema.

"Kwa vipi?".

"Kwa sababu hawa wageni wa Peter ni majasusi wa makaburu na tayari wako Arusha. Aidha Peter yuko Arusha ambako ndiko alikokimbilia ili kuungana na wenzie".

"Sawa kabisa. Sasa?", Mkurugenzi aliuliza.

"Sasa naomba umwalifu mwenzako huko Dar es Salaam kuwa mimi niko njiani kwenda kuungana na Willy na wenzake. Hii ni lazima kwani nilimwahidi marehemu Mwaura kwamba nitalipiza kisasi dhidi ya Peter Gerrit", Maina alisema.

"Unayo ruhusa", Mkurugenzi alisema. "Heri uende kuongeza nguvu dhidi ya majahili haya yenye nia ya kuhujumu mkutano wa ukombozi kusini mwa Afrika".

"Ahsante, mzee", Maina alishukuru.

"Nakutakia kila la heri".

"Nashukuru".

"Ukifika Arusha utamkuta Willy New Arusha Hoteli. Atakuwa na habari zako. Matayarisho mengine yako tayari kama kawaida", Mkurugenzi alimalizia.

Mike aliondoka. Wakati anatelemka ngazi alianza kumfikiria Will Gamba.

Walikuwa wamefanyakazi pamoja huko Angala kwa mara ya mwisho.

"Mbona itakuwa hatari", alijisemea huku akimwemwesa. Aliangalia saa yake ilionyesha kuwa ni saa tatu asubuhi.

"Chakula cha mchana leo nitakula mjini Arusha". Maina alijisemea tena.

"Hallo, naomba kuzungumza na ndugu Hamisi".

"Wewe ni nani?", sauti ya Katibu Muhtasi ilisikika.

"Mwambie ni mdogo wake aitwaye Willy".

"Mbona yeye analo jina la Ki-islamu na wewe na Kikristo? Utakuwaje mdogo wake".

"Kamwulize".

"Haya, babasubiri".

Baada ya muda kitambo Willy alisikia sauti kwenye simu. "Hallo, Hamisi hapa".

"Willy. Shikamoo, mzee".

"Marahaba. Vipi unaingia mji wa watu bila kuwaona wenyeji?".

"Hivi sasa ndio nawaeleza wenyeji kuwa nipo", Willy alisema.

"Sawasawa. Vipi, sasa unakuja?".

"Nisubiri. Nitakuwa ofisini kwako mnamo dakika tano zijazo".

"Willy alikuwa amepiga simu kutoka kwa rafiki yake karibu tu na ofisi ya upelelezi ya mkoa. Hivyo haikumchukulia muda mrefu kufika ofisi hapo.

"Eh, wewe binti ndiye unayetaka kujua ndugu za mkubwa wako wa kazi? Haya niulize vizuri au umeshamwuliza?", Willy alimwambia Katibu Muhtasi.

Msichana yule alimwangalia Willy kwa jicho la kuibia. Alimwona ni mvulana mwenye sura ya kupendeza na nadhifu. Roho ilimdunda.

"Aha, wewe ndiye Willy", aliuliza.

"Bila shaka", Willy alijibu.

"Kaka yako anakusubiri. Amesema ukifika uingie moja kwa moja", yule msichana alisema huku akilembua macho.

Willy naye alimtolea tabasamu la mwaka akamwacha amebung'aa.

Alifungua mlango na kuingia ndani ya ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa.

"Lo! Mwanaume huyu anaweza kukutia kiwewe. Anavutia hasa", yule msichana alibaki anajisemea kimoyomoyo.

Willy alifungua mlango na kuingia ndani ya ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa mkoa.

"Karibu, Willy", Hamisi alitoa tabasamu.

"Ahsante, mzee", Willy alimjibu Hamisi.

"Kazi iliyofanyika jana usiku nimearifiwa".

"Vizuri".

"Sijui watu hawa wameweza vipi kuingia maana polisi na sisi pia tulifanya tulivyoweza kuhakikisha kwamba watu wanaostahili tu ndio wale wanaingia nchini".

"Mzee Hamisi, lazima ufahamu kuwa watu hawa ni majasusi wa hali ya juu. Hivyo usione ajabu jinsi walivyoingia kwani hiyo ni moja ya kazi yao".

"Ni kweli Willy. Mimi nimeogopa sana. Jana usiku mpigania uhuru mmoja aliuawa kati ya saa tisa na saa kumi huko Mounti Meru Hoteli. Alikuwa chumbani kwake. Hii inaonyesha kwamba, kutokana na kazi mliyofanya, ni dhahiri kwamba siyo hao tu. Kuna kundi kubwa la majasusi tayari liko hapa mjini. Hivi sasa tunakabiliwa na upinzani mkubwa wa kutisha. Ingawa hata wewe uko hapo".

"Hii ni kazi na sisi tuko hapa kwa ajili ya kazi hii. Tunachokiomba ni Mungu atusaidie tuweze kuyasaka na kuyaangamiza majahili hayo, ili mkutano uanze hapo kesho kama ulivyopangwa. Lakini nakubaliana na wewe kwamba kazi kubwa lazima ifanyike, na tutaomba ushirikiano wenu".

"Sisi tuko hapa masaa ishirini na nne na hatutalala".

"Vizuri. Sasa ningependa kujua kama mmekagua hoteli zote ili kuhakikisha kuwa wageni wote waliojiandikisha kulala kwenye hoteli hizi wanatambuliwa sawasawa?".

"Hilo limefanyika baada tu ya kukuta Wazungu wamefariki". Hamisi alijibu. "Polisi pamoja na vijana wangu wamefanya ukaguzi wa hoteli na nyumba za kulala wageni. Ajabu ni kwamba hata wale Wazungu waliouawa walikuwa hawakujiandikisha kulala mahali popote".

"Basi hii ina maana hawalali hotelini wala katika nyumba za kulala wageni. Hivyo tunabaki na jibu moja; Majasusi hawa wanaishi nyumbani kwa mtu". Willy aliongeza.

"Sasa huyo atakuwa ni mtu gani?", Hamisi aliuliza.

"Hiyo ndio kazi yetu. Ninyi na sisi lazima tutafute watu hawa wanaishi nyumba gani. Ila tu nasema hii itawezekana kama vijana wenu watafanyakazi vizuri. Ili kuwa na uhakika naomba warudie kufanya ukaguzi kwenye hoteli hizo".

"Sawa, tutafanya hivyo. Lakini ikiwa ni nyumbani kwa mtu itakuwa ni vigumu", Hamisi alisema. "Kukagua nyumba hadi nyumba litakuwa jambo la ajabu".

"Sikiliza mzee", Willy alidakia. "Nyinyi hapa mnajua ni watu gani ambao mnahisi wanaweza kununuliwa kwa pesana kufanya kitendo kama hicho, watu mnaowashuku sharti kuwapeleleza usiku na mchana ili kufahamu ni nani

wanaingia au kutoka kwenye nyumba zao. Kama mkihisi au kugundua kitu chochote, tafadhali tunaomba mtujulishe".

"Mawazo yako ni sawa kabisa. Hata hilo pia nitalitekeleza", Hamisi aliitikia."

"Kuna habari nilizoleta ofisini kwako kuhusu magari mawili ili yachunguzwe ni ya aikina nani, sijui kama umepata majibu?", Willy aliuliza.

"Ndio, lile walilokuwa wanaendesha wale Wazungu linaonekana halikusajiliwa hapa Arusha. Wala popote nchini Tanzania. Ni jambo la ajabu sana kwani namba za injini siyo namba za gari ya aina hiyo iliyoingia hapa nchini, bali gari aina ya Peugeot 505 na muundo wa karibuni. Tumepeleleza na kushirikiana na wenzetu wa Kenya nao wanasema nambari hiyo hawana", Hamisi alieleza.

"Basi anchana nalo. Je, na lile gari lenye namba ARKK 5677?".

"Gari hilo linamilikiwa na kampuni ya kitalii ya Nyota Tours and Safari ya hapa mjini Arusha. Lakini tumechunguza na wenye gari hilo. Wao wanasema gari hilo halikwenda uwanja wa ndege jana. Aidha ni watu tunaowaamini sana hapa mjini. Mwenye Kampuni hii ni Mhindi mmoja tajiri sana ajulikanaye kwa jina la Feroz Kassam; mtu ambaye anaaminiwa sana hapa mjini. Ni Mhindi wa aina yake hapa nchini Willy alikumbuka habari kuhusu Mhindi huyo. Alikuwa ameelezwa sifa zake siku nyingi. Hasa alisifika kutokana na misaada yake na utiifu wake kwa Chama na Serikali.

"Aha, ni nani aliyetoa majibu haya? Ni F.K mwenyewe, kama mnavyomwita, au ni mtu mwingine", Willy aliuliza.

"Hapana. Ni meneja mkuu wa kampuni hiyo anaitwa Chris Tondo".

"Huyo ni nani?".

"Nilisema ni Meneja Mkuu wa Kampuni hiyo".

"Nina maana ya kuuliza ni mtu wa namna gani kutokana na mwenendo wake kiusalama?".

"Huyu amewahi kuwa afisa wa cheo cha juu katika Jeshi la Polisi na alistaafu kwa manufaa ya umma miaka iliyopita. Hatua hiyo ilichukuliwa kutokana na tuhuma kwamba alikuwa anasaidia wafanya magendo kuvusha mali nje ya nchi. Lakini toka siku hizo mpaka leo rekodi yake ni nzuri sana. Hajawahi kuwa na tatizo kiusalama wala katika maisha ya kawaida".

Willy alifikiri kidogo halafu akauliza tena. "Je, katika jalada lenu kuna habari kuhusu ilikuwaje mpaka akafanyakazi kwa F.K?".

"Hapana, bali tulifikiri aliombewa hiyo kazi na rafiki zake".

Willy alikuwa hakuridhika juu ya Chris Tondo. Aliinuka na kuaga akisema. "Nafikiri wewe tekeleza hayo mambo tuliyozungumza halafu tuonane baadaye".

"Sawa", Hamisi aliitikia.

Waliagana na Willy aliondoka kwa kupitia mlango wa Katibu Muhtasi.

"Wewe unaitwa nani?", Willy aliuliza.

"Naitwa Carol!" Yule msichana alijibu huku moyo wake ukimdunda.

"Iko siku Carol", Willy alimwambia Carol huku akifungua mlango na kupotea.

Alimwachia Carol kiu ya maelezo zaidi Willy alipoondoka pale ofisini aliamua kwenda Nyoka Tours and Safaris.

# SURA YA NANE

**P.G** aliwasili nyumbani kwa F.K kwa miguu baada ya teksi kumtelemsha karibu na ofisi ya mbao. Alisema amedai ndiko alikokuwa akienda ili kununua mbao za kununua. Alitembea kwa tahadhari kubwa. Ilikuwa saa nne na nusu alipojipenyeza kwenye ua wa nyumba ya F.K na kubisha hodi. F.K ndiye aliyefungua mlango. Alishangaa kumwona P.G.

"Hakuna mtu aliyekuona unakuja huku?", F.K alimwuliza huku uso wake ukionyesha huzuni na mashaka.

"Hakuna, F.K".

"Karibu ndani, P.G".

"Ahsante".

F.K alimwongoza P.G mpaka kwenye chumba cha siri. Majasusi wengine walikuwa ndani wanapumzika. Walipomwona walipomwona tu P.G wote walikaa kitako huku wakihisi kuna tatizo limetokea.

"Hebu tupe habari", F.K aliomba.

P.G alieleza yote yaliyotokea usiku ule na jinsi alivyokuwa ameamua kuja kuwaongezea nguvu wenzake baada ya kupoteza watu wake wote na kubaki yeye na mtu mmoja tu.

"Hivi nimemwacha Smith Namanga. Ataingia hapa mchana huu. Nimeona siyo vizuri sisi wote wawili kuja pamoja mchana huu", alisema P.G.

"Pole sana", walimjibu kwa pamoja.

Baadaye F.K naye alimweleza mambo yaliyokuwa yamewatokea.

"Hii ina maana kwamba mpaka sasa hivi mambo hayaendi vizuri. Lakini nina hakika tutashinda maana sasa tunajua nguvu za adui; na yeye hajui nguvu zetu wala maskani yetu". F.K alieleza.

"Sasa mipango ikoje", P.G aliuliza.

"Mipango iko kama ifuatavyo", F.K alieleza. "Usiku tutagawanyika mafungu mafungu. Kwanza lazima tuwamalize hawa watu watatu sababu ni kwamba sasa

tunafahamu vyumba vyao na hoteli. Vile vile sasa tunafahamu mienendo yao. Muda mfupi tu uliopita Chris alinipigia simu. Amesema kwamba amepata habari kuwa Willy Gamba amemwambia Mkuu wa Upelelezi kwamba hakuridhika na maelezo kuhusu gari letu nambari ARKK 567. Ameongeza kuwa Willy angeendelea kufanya uchunguzi kuhusu gari hilo. Hivyo nimemwasa Chris ajaribu kumkwepa Willy maana huyo ndiye mtu hatari zaidi. Yeye ndiye aliyefanya mauaji ya jana".

"Je, huyu Mkuu wa Upelelezi yuko upande wetu?". P.G aliuliza.

"Ndio na hapana", F.K alijibu. "Huyu Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa ni mtu ambaye tumemsaidia sana kifedha. Zaidi ya hayo yeye anaamini kwamba sisi ni watu wanaotii sana Serikali. Kutokana na misaada yetu kwake, neno lolote linaloweza kutudhuru sisi yeye atatusaidia kwa kila njia. Lakini akijua ukweli katika swala kama hili, lazima atatuuza. Kutofanya hivyo kunaweza kuwa na yeye kupoteza kazi yake au hata kupewa adhabu kali ya kifo kama mhaini. Kusema kweli wanamwogopa sana Willy".

"Hao viongozi wa wapiganian uhuru watakaohutubia mkutano wameshaisha fika".

"Watatu wamefika na wengine wawili watafika jioni hii, kuhusu wale ambao wamefika tayari tumechukua habari juu yao. Mienendo yao pia tumeisha ifahamu. Hata wale wawili wakiingia tutapata habari zao. Kama ujuavyo P.G, mimi naaminika hapa kama mwanamapinduzi. Habari zozote ninazozitaka nazipatamoja kwa moja kutoka kwa watayarishaji wenyewe wa mkutano huo. Hivyo lazima tuwafungie kazi hawa viongozi leo usiku, halafu tuone kama mkutano utafunguliwa", F.K, alisema.

F.K alisema. "Sasa hivi natoka ili nikamilishe mipango ya usiku kwa kupata habari zaidi. Na wewe Peter, George atakupa mipango yote ambayo tumeifanya kwa ajili ya usiku. Kwa vile na wewe umeongezeka. ni dhahiri kwamba tutashinda. Tutatenda kitendo ambacho kitaiacha dunia nzima inagwaya".

"Vizuri. Mimi nitaelewana na George halafu nitapumzika maana mpaka sasa sijalala. Wewe kakamilishe mipango hiyo kuhusu kazi", P.G alijibu huku yeye na George wakielekea chumba kingine

Willy alikaribia ofisi za Nyota Tours and safaris. Hapo hapo alimwona msichana mrembo sana akitoka nje ya ofisi hiyo. Kila wakati Willy alipokutana na wasichana warembo namna ile aliwaona kama sumu kwake kwani alikuwa mgonjwa sana juu yao.

Willy alibana kwa mbali kidogo ili aweze kuyapa nafasi macho yake yapate chakula chake. Alipenda amwone vizuri mrembo huyu ambaye aliumbwa ili wanaume wajisikie raha. Willy aligundua kwamba hakuwa yeye peke yake aliyekuwa anamwangalia, bali wanaume wengine pia walikuwa wanalisha macho yao kwa chati.

Msichana huyu alitembea mpaka kwenye gari moja. Alitoa funguo kwenye pochi yake na kusimama ili afungue mlango. Willy alijuwa kuwa gari hiyo mpya aina ya Toyota KE 30, ilikuwa ya huyo msichana. Lakini hakushangaa kwani msichana mrembo kama yule angeweza kumpata mtu yeyote mwenye pesa akamnunulia kitu chochote. Hata gari angemnunulia ili mradi tu aridhike.

Wakati huyo msichana anaingiza funguo kwkenye tundu la kufuri katika mlango wa gari. Ghafra akatokea kijana. Alikwapua pochi yake halafu akakimbia. Huku akiwa ametoa jisu kali alitisha mtu yeyote ambaye angethubutu kumfuata. Yule msichana wa watu alitoa sauti kali yenye kutia hofu halafu akaanguka chini. Watu waliokuwa karibu walisambaa kwa kuogopa hilo jisu kali.

Willy ambaye alishuhudia kitendo hicho cha kijambazi, alianza kumfukuza yule kijana. Alipoona kuwa watu wote wamesambaa isipokuwa mtu mmoja tu aliyekuwa bado anamsakama, yule kijana alisimama kumsubiri Willy apambane nae ana kwa ana.

"Hunijui mimi eh? Mji mzima wananijua mimi ni nani... sogea nikukate kichwa ", alitamba yule jambazi kijana.

Willy alimwendea kwa tahadhari kubwa huku watu wote wakipiga makelele kumsihi arudu nyuma kusalimisha maisha yake. "Rudi, rudi! Kimbia! huyo ni mwuaji! Anamaliza watu hapa".

Kama kwamba hasikii Willy alizidi kumsogelea yule jambazi. Mara yule jambazi alimvamia Willy kama mchezo vile. Willy alikwepa shambulizi la kwanza na lile jisu. Alimnasa mkono wake na kumkata mkono mmoja wa karate kwenye bega lile jisu lilianguka. Willy alilipiga ngwala lile jambazi mpaka chini. Kuona vile yule msichana alikimbia mpaka pale. Huku akiwa ameshikilia kiatu chake mkononi alimpiga na kisigino yule jambazi. Hapo ndipo watu wengine walipofika pamoja na polisi wa doria. Akiwa ameshika pochi aliyoporwa, Willy alimvuta kando yule msichana.

"Ahsante sana", msichana alimwambia Willy. "Ahsante bwana. Sijui nikushukuru vipi kwa kujitolea maisha yako ili kuokoa mali yangu".

"Sijali", Willy alisema. Kwa mtoto kama wewe. Kila mwanaume kamili yuko tayari kujitoa mhanga maisha yake".

Polisi alimfuata Willy akimtaka akatoe maelezo ya wizi huo katika kituo cha polisi. Lakini Willy alimnong'oneza Polisi huyo naye akamwacha huru. Huku amemfunga pingu jambazi yule na kundi la watu walimfuata. Polisi alianza safari kuelekea kituo cha polisi. Alimwacha Willy akizungumza na yule msichana hapo pembeni mwa barabara. Yule msichana alianza kutokwa na hofu na kurejea katika hali ya kawaida. Sasa alimwangalia yule kijana aliyekuwa ameokoa mali yake. Alikuwa kijana mwenye sura ya kupendeza sana. Vile vile alikuwa na kitu kingine ambacho ilikuwa vigumu kukieleza. Huyo kijana alisisimua damu yake.

"Ehe, unaitwa nani?", Willy alimwuliza.

"Naitwa Nyaso", msichana alijibu.

"Nyaso tu, basi?".

"Ndio, Nyaso tu basi! Na wewe waitwaje?".

"Mimi naitwa Willy".

"Oh, vizuri. Sijui nikupe nini Willy!".

"Usijali, sasa hivi nina shughuli. Tunaweza kuonana jioni mnamo saa kumi na mbili hivi, angalau kwa muda mfupi, niweze kukununulia kinywaji", Willy alimwuliza.

Nyaso alifikiri sana kwanza. Alimwogopa sana F.K. angechukia ikiwa angejua alitoka nje na mtu, hasa mtu mgeni. Hali hii aliipima na jinsi F.K. alivyokuwa hataki kumwona siku hizi kwa kisingizio eti alikuwa na shughuli nyingi. Alifikiria sana jinsi F.K. alivyokuwa amemkaripia eti kwa kumpigiapigia simu nyumbani kwake wakati yeye alikuwa na kazi nyingi. Kama namna moja ya kumkomoa F.K. Nyaso alikubali mwaliko wa huyu kijana ambaye alimsisimua damu.

"Sawa, una miadi!" Nyaso alijibu.

"Arusha, Oke, nichukue hapo New Arusha saa kumi na mbili kamili", Willy alisema.

"Nitafika bila kukosa", Nyaso aliahidi.

Huku akitingisha matako yake huku na huku, alielekea kwenye gari lake na kumwacha Willy ameshikwa na butwaa. Alipoingia ndani ya gari Nyaso

alimrushia busu Willy ambaye alisikia kama vile moyo wake umekosa pigo moja. Nyaso alipopotea ndipo Willy alipokumbuka safari yake ya kwenda kwenye ofisi ya Chris Tondo, ambayo ilikuwa karibu na hapo alipokuwa. Vile vile ndipo alipogundua kwamba Nyaso alikuwa anatokea kwenye ofisi ile ile wakati alipovamiwa.

Chris Tondo alikuwa katika pilika pilika humo ofisini kwake. Alikuwa akikusanya makaratasi na kutatunza kwenye visanduku. Alifanya shughuli hii haraka ili atoke ofisini. Alikuwa ameambiwa na F.K kufanya hivyo ili Willy asije kumkuta.

Wakati huo huo Willy alifika kwenye ofisi za Nyoka Tours and Safaris.

"Habari za leo", Willy alimsalimia kijana mmoja aliyekuwa kwenye ofisi ya nje.

"Nzuri, mzee. Nikusaidie nini?".

"Naomba kumwona ndugu Chris Tondo".

"Una miadi naye".

"Yupo?", Willy aliuliza.

"Ndiyo yupo, lakini huwezi kumwona huna miadi", kijana alisema

"Mimi ni rafiki yake. Ukinirudisha bila kumwona halafu akasikia umefanya hivyo ujuwe wewe huna kazi", Willy alitishia huku akielekea kwenye ofisi iliyoandikwa Meneja Mkuu.

Aliwaacha wafanyakazi wote kwenye ofisi ile wakimwangalia wasijue la kufanya. Alifungua mlango na karibu wagongane na Chris Tondo ambaye pia alikuwa anafungua mlango huo ili atoke nje.

"Oh, pole sana", Willy alisema.

Tondo alipogundua huyo alikuwa Willy, alisikia moyo wake unapiga haraka na akashindwa kupumua sawasawa.

"Karibu", Tondo alijikuta amebabaika.

"Ahsante", Willy aliitika huku akifunga mlango nyuma yake.

"Hawa vijana hawakunieleza kuna mgeni", Tondo alisema huku akionyesha kukasirika.

"Samahani, kwa kweli wao hawana kosa kwani ni mie ambaye sikuwasikiliza", Willy alijibu.

"Ehe, nikusaidie nini ndugu...?".

"Willy Gamba", Willy alimalizia.

Tondo alishangaa kumsikia Willy akijitambulisha kwa jina lake la kweli kwani alifikiri angejificha. Hii ilimtia hofu zaidi.

"Ya, nikusaidie nini ndugu Gamba?".

"Natumaini wewe ni ndugu Tondo. Meneja Mkuu wa Kampuni hii?", Willy alimwuliza huku akimtazama machoni.

Moyoni Tondo alijua mambo yameanza kutibuka. Alijisikia kujuta kwani alifahamu jinsi gani Willy aliweza kusoma mawazo ya mtu aliyezungumza naye. Kitu hicho ndicho kilichomfanya Willy kufanikiwa katika kazi yake ya upelelezi. Tondo alitafakari alipoulizwa vile.

"Ndio", Tondo alitumia uzoefu wake wa kipolisi kujibu swali hilo. Kwani alifahamu majibu mafupi yalikuwa mazuri kwa mtu anayehojiwa.

"Mimi ni afisa usalama kutoka Dar es Salaam. Nimefika hapa kwa shughuli za kiserikali. Nimeshawishika kuzungumza na wewe niliposikia uliwahi kuwa afisa wa cheo cha juu katika idara ya polisi".

"Vizuri", Tondo alijibu huku akishangaa kuona jinsi Willy alivyokuwa akijieleza.

"Sijui uliwahi kufika kwenye uwanja wa ndege jana usiku?", Willy aliuliza.

Mate yalimkauka Tondo alipofikiri juu ya uwezekano kwa kwamba Willy alikuwa amemwona wakati anatoa upepo ndani ya gari. Tondo alijuwa watu kama hawa walikuwa hatari.

Baada ya kusita kidogo, alijibu kwa sauti hafifu. "Hapana!".

"Nasikia gari nambari ARKK 567 ni lenu?", Willy alimpachika swali Tondo.

"Ndio"

"Nani huwa analiendesha mara kwa mara?".

"Unajua sisi tunafanya kazi ya kuhudumia watalii. Hivyo tunayo magari mengi na madereva wengi. Hatuna dereva maalum kwa gari fulani", Tondo alijibu.

"Nani alikuwa anaendesha gari hilo jana?".

Tondo alisita kujibu kwani alijua jibu la swali hili lilikuwa muhimu sana kwa Willy.

"Jana halikutoka", Tondo hatimaye alijibu.

Willy alijua alikuwa ameongopa tena.

"Kwa nini, lilikuwa bovu?".

"Wakati tunapokuwa hatuna kazi nyingi, magari yetu hufungiwa tu katika gereji".

"Gereji yenu iko wapi?".

"Iko nyuma tu ya ofisi hii", Tondo alijibu.

"Kwa hiyo gari haliwezi kutoka bila ruhusa kamili", Willy alipendekeza.

"Kabisa".

"Oke, ndugu Tondo, vizuri. Samahani kwa kuchukua muda wako", Willy alisema huku akiwa amesimama tayari kuondoka.

"Hivi kuna jambo gani kuhusu hilo gari? Naona sina budi niulize", Tondo aliuliza.

"Wewe umekuwa afisa wa polisi kwa muda mrefu, kwa hiyo ni lazima unaelewa mambo haya", Willy alimjibu. "Wakati mwingine tunapata habari fulani fulani. Inatubidi kuchunguza na kuthibitisha, vinginevyo watu wanaweza wakaumia bure".

"Ni kweli", Tondo alijibu.

"Oke, kwaheri".

"Karibu tena, ndugu Gamba".

"Willy alifungua mlango na kutoka ofisi ya nje. Aliwaaga wale wafanyakazi wa ofisi ile.

Tondo alirudi akaa kitako kitini mwake na kuanza kufikiri.

Willy alipotoka tu nje alitembea haraka sana na kuzunguka nyuma ya ile ofisi. Huko aliona lango la kuingilia katika gereji. Alibisha hodi maana lilikuwa limefungwa. Mara mlinzi alifungua.

"Tukusaidie nini, mzee", aliuliza yule mlinzi.

"Jana nilipewa lifti na ndugu Tondo. Lakini kwa bahati mbaya nilisahau miwani yangu ndani ya gari lake. Sasa amenishauri nije nikaangalie kama bado imo iwapo gari hilo halijatoka", Willy alijibu.

"Ahaa, gari alilokuwa anaendesha jana. Si ni lile ARKK 567?".

"Nafikiri", Willy alijibu.

"Basi, limetoka kwenda kujaza mafuta kwenye kituo chetu", alijibu mlinzi.

"Siyo kitu, nitamwambia yeye anitazamie miwani hiyo wakati gari likirudi".

"Haya, kwaheri", mlinzi alijibu huku akirudisha lango.

"Kwaheri", Willy alijibu huku akimwemwesa.

Ilikuwa saa saba na nusu za mchana. Willy, Bon na Rocky walikuwa wakila chakula pale pale New Arusha Hoteli. Ilikuja simu ambayo ilimhitaji Willy.

"Wewe mzee ndiye Willy Gamba?", mhudumu mmoja alimwuliza Willy.

"Ndio".

"Kuna simu yako".

"Sawasawa", Willy alisema huku akiweka kisu na uma kwenye sahani.

Alikwenda kusikiliza simu.

"Hallo, Willy hapa", Willy alisema baada ya kuunyakua mkono wa simu na kuupachika katika sikio lake la kushoto.

"Hapa ni mapokezi. Kuna mgeni wako ngoja uzungumze naye".

Hallo, Mike Maina", sauti ilisikika.

"Wewe unafanya nini hapa", Willy aliuliza kwa mshangao kwani alikuwa hakumtegemea.

"Nimekuja kukutafuta. Kwani wewe unafanya nini hapa", Maina aliuliza.

Willy alifahamu kwa nini Chifu alikuwa amemtafuta; Maina alikuwa ameletwa ili kuongeza nguvu.

"Njoo kwenye ukumbi wa maakuli. Utatukuta kwani nafikiri una njaa", Willy alimwambia.

"Nitakuja kwa haraka kama jeti", Maina alijibu.

Maina alimkuta Willy na wenzake wakiendelea kula chakula.

"Hallo Maina, karibu", Willy alimkaribisha Maina huku wenzake wakisimama.

"Ahsante Willy, mambo?", Maina aliuliza.

"Mambo ni segemnege", Willy alijibu huku akivuta kiti na wote wakakaa.

"Hebu nikujulishe kwa hawa ndugu zetu hapa. Naamini hamfahamiani", Willy alisema. "Huyu ni Bon Sipele wa wapigania uhuru na huyu ni Rocky Malele wa Zimbabwe".

Kisha Willy alimgeukia Maina na kusema. "Na huyu jamani ni Mike Maina kutoka Kenya".

Wote walisalimiana.

"Nilipata habari zake Angola alipokuwa naye. Mlifunga kazi takatifu", Bon alisifia.

"Basi, huyu ndiye Mike Maina", Willy alisisitiza.

Mhudumu alifika mezani na Maina akaagiza chakula.

Wakati huo Willy, kwa sauti ya chini, alikuwa anaeleza sifa za kipelelezi za kila mmoja.

"Basi mambo yanazidi kujipa", Rocky alisema.

"Sasa Mike, tupe habari za huko Nairobi. Nikisoma sura yako nahisi kuna mambo", Willy alichokoza.

"Haya, nisikilize kwa makini halafu na nyinyi baadaye mnijulishe mambo ya hapa", Mike alisema.

Mike aliwaeleza yaliyotokea Nairobi huku akiendelea kula chakula. "Nilipopita mpakani leo nilishangaa. Nilikuta rafiki yangu Peter Gerrit kaishapita. Alitumia jina la Peter Anderson na kudai yeye alikuwa ni Askofu kutoka Zimbabwe akija kuhudhuria mkutano wa wapigania uhuru. Kwa sababu hiyo maafisa usalama na uhamiaji wakampitisha haraka. Hivyo yuko hapa na mnaweza kuona wenyewe hali ya mambo".

"Kwa hiyo rafiki zangu", Willy alimalizia. "Mji huu umeingiliwa na balaa. Bila shaka damu itamwagika. Tuwe tayari kujitoa mhanga ili wale watakaobaki wawezi kufaidi matunda ya uhuru. Uhuru ni kitu muhuimu kwetu na kwa vizazi vijavyo".

Bon alisema. "Na sisi watu wa Afrika Kusini tunaamini kwamba kabla ubaguzi wa rangi haujatokomezwa ni lazima damu ya wazalendo itamwagika. Tuko tayari kwa yote hayo. Kama mnavyosikia, hata vijana wadogo wameamua kujitoa mhanga ili kutokomeza utawala wa Makaburu kwa faida ya walio wengi. Kwa hiyo Willy, mimi niko tayari kufa kwa ajili ya nchi yangu. Lakini kabla sijafa, nitahakikisha nao wanakiona cha mtema kuni".

"Kwa sasa hivi mipango gani?", Mike aliuliza.

"Kwanza kabisa nimempigia simu mtu wetu hapa, ambaye ni Mkuu wa Upelelezi Mkoa, Ndugu Hamisi", Willy alieleza. "Ameweka vijana wa kumfuatilia Chris Tondo. Ninayo imani kuwa yeye anaweza kutufikishia walipo hawa majasusi. Sina shaka mtu huyu anahusika nao kwa namna fulani".

"Kama inao uhakika", Mike alishauri. "Kwanini tusimufuate sisi wenyewe, ikibidi tumsakame mpaka atueleze tu? Wewe mwenyewe unajua kuwa tuna uwezo wa kumfanya mtu hata mwenye kichwa ngumu kama, atatapika maneno".

"Hapana, tusifanye haraka, maana watu kama hawa wanazo mbinu nyingi", Willy alieleza. "Lakini hata sisi tunazo mbinu zetu. Tunaweza kumfanya akatueleza mahali walipo bila kutumia nguvu zetu nyingi. Unajuwa bado tunahitaji nguvu zetu hasa kwa kupambana na hawa majahili", alieleza Willy, halafu akaanza kuwapa mipango kwa ajili ya usiku ule".

"Sisi tutasimama badala ya hawa viongozi wa wapigania uhuru. Sisi pamoja na wao ndiyo wanaowindwa. Hivyo kuanzia saa tatu tutajipoteza maana watu hawa watakuwa wanatuvinjari".

"Tumekuelewa barabara", Rocky alidakia.

"Na ninaamini mipango yako ni sawasawa kabisa".

"Mike, kula", Willy alishauri mara mhudumu alipoleta chakula. Mhudumu alipoondoka. Willy na wenzake waliendelea na mazungumzo yao.

# SURA YA TISA

**ILIKUWA** saa nane za mchana wakati F.K aliporudi. Alikuta wenzake wamelala. Walihitaji usingizi kwani usiku huo walitarajia kuwa macho. Alienda moja kwa moja kwenye chumba ambamo Peter Gerrit, George na Dave walikuwa wamepumzika.

"Karibu, F.K", George alimkaribisha. Yeye tu ndiye aliyekuwa hajalala.

"Una mapya yapi?".

"Ninayo mengi", F.K alijibu. Wakati huo huo Peter na Dave wakazinduka kutoka usingizini.

"Kwanza Tondo nimemkuta ofisini?", F.K aliuliza.

"Anasema kuwa Hamisi alimpigia simu na kumweleza kuwa Willy alimshauri aweke vijana wa usalama kumfuatilia na kuripoti mienendo yake yote. Hivyo nimemshauri akitoka ofisini aende moja kwa moja nyumbani kwake na asitoke".

Aliposikua hivyo George aliinuka kitandani.

"Hapana F.K", George alisema na kuinuka kitandani.

"Tondo lazima auawe".

"Auawe? Hapana, mtu huyu ametusaidia sana", F.K alimtetea Tondo. "Lazima aishi ili naye aweze kufurahia ushindi. Bila yeye mimi nisingeweza kufanya yote niliyofanya hapa nchini. Taarifa zote za kijasusi nilizoleta ni kutokana na msaada wake, kwani yeye alikuwa afisa wa cheo cha juu katika jeshi la polisi. Hapana, George, Chris Tondo lazima aishi ili afaidi matunda ya ushindi wetu. Vile vile nimeamua kwenda naye Afrika Kusini baada ya kazi ya hapa".

Wale majasusi wengine walimwangalia kwa macho makali yenye kutoa onyo.

"Nafikiri litakuwa jambo la busara kwako kufanya hivyo", P.G. alimwasa F.K.

Wakati wenzake walipokuwa wamepumzika, mnamo saa kumi za mchana, Willy alimpigia simu ndugu Mbeki. Mbeki alikuwa Mwenyekiti wa kamati ya kutayarisha mkutano. Alikuwa amefikia Mount Meru Hoteli.

"Hallo. Mount Meru hapa", mpokeaji simu alisikika akisema.

"Nipe chumba 321", Willy alisema.

"Subiri".

"Hallo, Mbeki hapa".

"Aha, nimepata habari kuwa unanitafuta".

"Sawasawa, naomba uje tuonane hapo kwenye klabu ya Kituo cha mikutano ya Kimataifa. Unaifahamu?", Willy aliuliza.

"Basi, jitahidi uwe pale katika muda wa dakika kumi zijazo".

"Haya".

Willy aliweka simu chini na kuteremka chini.

Alichukua teksi na kuelekea AICC Klabu.

Alipofika alisubiri kidogo na Mbeki akawasili. Willy alikuwa anajulikana sana mahali hapo. Aliongozana na Mbeki mpaka kwenye kibanda kimoja, halafu wakaagiza vinywaji.

"Tumekuwa na wasiwasi sana baada ya matukio makubwa ya jana", Mbeki alianza.

"Hiyo ndiyo sababu imetuleta hapa", Willy alijibu.

"Ulinzi wa Polisi unaonekana ni dhaifu sana", Mbeki alisema. "Viongozi wote wanawasili leo jioni, tayari kwa mkutano wa kesho. Sasa mimi ninao wasiwasi. Kuna mtu ambaye anatoa habari zetu nje, lakini hatujui ni nani".

"Mimi nashauri kuanzia sasa mtoe habari kwa mtu yeyote. Ikibidi punguzeni watu hata kwenye kamati ya matayarisho. Bakizeni watu tunaowafahamu fika. Sasa nisikilize kwa makini. Nataka ufanye kama nitakavyokueleza. Usikose hata chembe, kwani ukikosea, kutatokea balaa isiyoelezeka", Willy alitahadharisha.

Alianza kumweleza Mbeki juu ya mipango yote ya usalama wa mkutano kuanzia dakika ile mpaka mwisho wa mkutano. Alimweleza mipango ya ulinzi wa wajumbe, na viongozi mashuhuri wa wapigania uhuru.

NYASO

Ilikuwa saa kumi na mbili juu ya alama, Nyaso alipoegesha gari lake hapo New Arusha Hoteli. Willy alikuwa anaranda pale nje ya hoteli akimsubiri.

"Nimeamini kuwa unajuwa kuweka ahadi mtoto we, Wasichana wengi wa Kiafrika hawaweki muda maanani", Willy alisema huku akifungua mlango wa gari na kuingia ndani.

"Wacha kutuonea, siku hizi tumebadilika, hujui kuwa wakati huu unajulikana miaka ya elekttroniki! Watu lazima kwenda kwa wakati", Nyaso alijibu huku akiondoa gari.

"Unanipeleka wapi?", Willy aliuliza.

"Nilipiga simu 'Kambi ya Fisi' na kuomba watuwekee nyama ya kuchoma", Nyaso alijibu.

"Hiyo ni maridadi", Willy aliitikia aliitikia halafu akaendela.

"Vipi maisha hapa".

"Mwenyezi Mungu anatusaidia".

"Umeishi hapa Arusha kwa muda mrefu?".

"Miaka mitano hivi".

"Mimi nakuja hapa mara kwa mara lakini sijawahi kukuona, sijui huwa unajificha wapi?".

"Mbona maswali mengi? Unajuaje, huenda mwenzio nimewekwa kinyumba?", Nyaso alimtolewa Willy jicho la kiwiziwizi.

"Unasema kweli, hebu nisiulize maswali mengi kwani ninaweza kujiumiza roho bure".

"Pole sana".

Waliendelea na safari mpaka 'Kambi ya Fisi'.

Walipowasili Willy aligundua kuwa wahudumu wa pale walikuwa wanamfahamu sana Nyaso. Hiyo ilitokana na kwamba walipowasili Willy aliona wahudumu wakimkimbilia Nyaso na kuwapa mahali pazuri pa kukaa.

"Nyama uliyoagiza karibu itakuwa tayari", mhudumu alisema.

"Utasubiri kidogo tu".

"Hakuna tabu", Nyaso alijibu wakati wakikaa kwenye viti.

Watu wengi walikuwa pale ambapo pia walikuwa wamekuja kuchoma nyama.

"He, leo ni maajabu! Umemwona Nyaso kaja na mwanaume! Siyo maajabu haya?", kijana mmoja aliwauliza vijana wenzake wapatao watano.

"Huenda ni kaka yake", kijana mwingine alisema. "Huoni kuwa hata kijana mwenyewe anayo sura nzuri".

"Watu wanasema eti Nyaso hana ndugu, sasa huyo kaka katoka wapi", kijana wa kwanza alidadisi.

"Ya nini kuingilia maisha ya watu? Ndio sababu nyinyi waswahili hamwendelei. Mnapenda kuchunguza maisha ya wengine huku yale ya kwenu yanawashinda. Kama huyo kijana kaka yake au bwana yake nyinyi inawahusu nini? Iwapo mtu anavutiwa si heri akatafute nafasi yake halafu abahatishe tu? Vinginevyo kama Nyaso kapata bwana mwingine na kumwacha F.K hicho ni kilio chake F.K", kijana mwingine aliyeonekana kuwa mkubwa kidogo kuliko wengine aliwaasa wenzake. Hivyo iliwabidi kujali yaliyowaleta.

"Unafanya kazi wapi?", Willy alimwuliza Nyaso wakati wakinywa vinywaji baridi.

"Sasa hivi sifanyi kazi yoyote, ila naandaa kitabu".

"Eh, kitabu kuhusu nini?".

"Kinahusu uchumi wa nchi yetu".

"Wewe ni mtaalam wa mambo ya uchumi?".

"Ndiyo. Ninayo shahada ya kwanza katika uchumi".

"Ahaa vizuri sana. Hata mimi ni hivyo hivyo".

"Na wewe unafanya kazi gani?".

"Mimi niko Dar es Salaam ambako ninafanya biashara".

"Na hapa Arusha umekuja kufanya nini?".

"Mimi ni shabiki wa siasa, hivyo nimekuja kusikiliza mkutano wa hawa wapigania uhuru".

Nyaso alimwangalia bila kuamini masikio yake.

"Mkutano kama huu utakusaidia nini na wewe ni mfanya biashara?" Nyaso aliuliza.

"Nimekwambia kuwa mimi ni shabiki wa siasa. Madhumuni ya shabiki wa kitu chochote siyo kupata faida ya mali, bali kufanya mioyo yao ifurahi".

"Lakini wewe huelekei kuwa mtu wa kushabikia kitu hivi hivi tu".

"Sijui sasa", Willy alijibu kisha akaendelea.

"Mimi nilifikiri unafanya kazi Nyoka Tours and Safaris maana kabla hujavamiwa na yule jambazi nilikuona unatoka kwenye ofisi zao".

"Hapana, mwenye kampuni hiyo ndiye bwana yangu", Nyaso alijibu huku akiangalia chini.

Willy alisikia damu inamsisimka.

"Una maana ya F.K au Chris?", Willy aliuliza.

"Ni nani katika nchi hii ambaye hamjui F.K? Yule ni mtu maarufu sana".

"Basi, ni huyo F.K".

"Hongera, Nyaso kwani kwa mara ya kwanza nimeona msichana wa Kiafrika ambaye ni binti wa mvulana wa Kihindi kiwaziwazi bila kujificha".

"Nimekwambia Willy dunia inageuka.

Willy aliisifu tena nyota yake, kwani kama kweli msichana huyu alikuwa bibi yake F.K, basi bila shaka alimfahamu sana Chris Tondo. Ilikuwa ni bahati kwamba Willy, kama alivyofikiri, angejua mengi kutoka kwa Nyaso.

"Bahati yangu mbaya. Mimi nilifikiri nimepata mchumba kumbe wameisha niwahi", Willy alinung'unika.

Nyaso alimwangalia Willy na kumhusudu. Alifikiri ingekuwa furaha iliyoje kama angeolewa na kijana mzuri kama yule. Akimlinganisha Willy na F.K, Nyaso alijilaumu. Alijua alikuwa anaishi na F.K kwa sababu ni yeye tu ambaye aliweza kumtimizia mahitaji yake kipesa, hakuwa na mapenzi yoyote juu ya F.K. Lakini sasa matayarisho ya mpango wake yalikuwa yanakaribia kukamilika. Nyaso alikuwa na nyumba tayari. Alikuwa na gari na pesa pia. Hivyo angeweza kuanza opereshani wakati wowote. Alipofikiri hayo, Nyaso alijisikia machozi yanamlengalenga.

"Nini sasa, dada umekuwa nini?", Willy aliuliza alipomwona msichana huyu akitokwa na chozi la hudhuni. Na ilikuwa ajabu kwamba Nyaso alipotokwa na machozi ndiyo alivyozidi kupendeza.

"Usijali, kila mtu huwa na matatizo yake. Nimekumbuka jambo ambalo limenigusa moyoni, lakini siyo kutokana na wewe".

"Basi, pole".

"Ahsante".

Kutokana na uzoefu wake wa siku nyingi kuhusu wasichana, Willy aligudua kwamba Nyaso hakuwa na furaha katika uhusiano wake na bwana yake. Hivyo aliamua kutumia nafasi hiyo ili aweze kujua mengi zaidi juu ya Chris Tondo na F.K.

"Wewe na F.K mnakaa pamoja", Willy aliuliza.

"Hapana".

"Wewe unakaa wapi?".

"F.K alininunulia nyumba huko Kijenge, na yeye anaishi kwenye jumba lake huko Themi Hill".

"Anasubiri nini asikuoe msichana mrembo hivi. Anafikiri watu wengine hawakuoni?", Willy alimtolea Nyaso tabasamu la kumlainisha.

"Hiyo ni shauri yake".

"Au ni kwamba wazazi wako hawataki wewe uolewe na Mhindi?", Willy aliongeza. Mara aliona machozi yanamlengalenga Nyaso mara ya pili.

"Hapana", Nyaso alijibu.

Willy alihisi wazo fulani lilimjia akilini mwake.

"Nyaso, wazazi wako wako wapi?".

Nyaso hakumjibu Willy. Wote wawili walikaa kimya kwa muda mpaka nyama ilipoletwa.

"Basi, sahau yote hayo unayofikiria ili tule nyama na kufurahi", Willy alimshauri Nyaso.

"Uliniambia jina lako ni Willy nani?", Nyaso aliuliza kwa unyonge.

"Willy Gamba".

"Nimewahi kusikia jina kama hilo mahali fulani", Nyaso alisema.

"Kama siyo redioni, basi ni kwenye magazeti".

"Sijui, labda ni mtu mwingine. Kama ujuavyo, baadhi ya watu wanayo majina yanayofanana".

"Willy sijui nianzie wapi", Nyaso alisema halafu akasita.

"Naona kama kuna kitu kinakukera rohoni", Willy alisema. "Nakushauri ukiseme tu. Mimi ni kijana mwenzako. Unajua Nyaso, kama kuna jambo linalokukera moyoni, dawa ya kuleta nafuu ni kumwambia mtu. Ni vizuri zaidi ukamwambia mtu kama mimi ambaye hatufahamiani. Hivyo itasaidia sana kwani huwezi kuwa na wasiwasi kwamba nitawaambia watu wengine. Mimi sijui marafiki zako na wewe hujui marafiki zangu".

"Willy, nitakupa siri yangu ya maisha ambayo hakuna mtu mwingine anayeijua isipokuwa mimi mwenyewe. Pamoja na mwito wako wa kutaka nikueleze, huenda nisingekueleza. Lakini kwa kuwa wakati wa kutekeleza mpango umekaribia, nitakueleza tangu mwanzo.

Mara mhudumu alifika kwenye meza yao.

"Nyama ya hapa ni safi sana", Willy alinena.

"Ndiyo sababu ilinifanya nikulete hapa hapa", Nyaso alidakia.

"Msee, hapa nyama ni safi kabisa kabisa", mhudumu aliongeza.

"Wewe ni Mchagga?", Willy aliuliza.

"Ndiyo".

"Biashara kweli mnaijua", Willy alimsifia.

"Utafanya nini, babangu?", mhudumu aliitikia halafu akaondoka zake.

"Hebu endelea", Willy alimkumbusha Nyaso.

"Mimi nilizaliwa miaka ishirini na sita iliyopita nikiwa ni mtoto wa tatu wa Dk. Soni", Nyaso aliendelea. Baba yangu alikuwa daktari wa mifugo na mama yangu alikuwa muuguzi. Miaka saba baada ya mimi kuzaliwa tulivamia na majambazi wakati wa usiku, huko nyumbani Moshi. Majambazi hayo yalivunja nyumba na kuua watu wote wa familia yangu isipokuwa mimi tu. Mtumishi wetu wa

nyumbani, akiwemo mlinzi wetu waliuawa pia. Hata mimi nilidhaniwa kuwa niliuawa. Majambazo yalipompiga mapanga dada yangu mkubwa aliniangukia na sote wawili tulianguka chini. Majambazi walifikiri kuwa nami nilikuwa tayari nimekufa".

Aliposema hayo, Nyaso alinyamaza kidogo huku machozi yakimtoka.

Willy ambaye alikuwa akimsikiliza Nyaso kwa makini na mshangao alimshauri asilie.

"Unajuwa kuwa hapa tuko hadharani, hivyo nakuomba usilie".

"Sawa", Nyaso alijibu, halafu akaendelea. "Walipoamini kuwa wameua kila mtu, ndipo alipotokea yule mtu ambaye alikua amekodi majambazi. Lengo lake lilikuwa kuhakikisha kwamba kazi aliyowatuma ilikuwa imetekelezwa ndipo awalipe ujira wao. Mtu huyo nilimwona na kumtambua. Halafu nafikiri nilizirai, kwani nilipopata fahamu nilijikuta hospitali huku nimezungukwa na wauguzi pamoja na askari polisi. Baada ya siku mbili niliruhusiwa kutoka hospitali. Nilichukuliwa na polisi kisha niliulizwa maswali mengi. Ni ajabu kwamba sikuweza kukumbuka jambo lolote. Mwisho wake waliniachia kisha nikachukuliwa na Masista wa madhehebu ya Kikatoliki. Wao ndio walionitunza na kunipekeka shule hadi nilipomaliza kidato cha sita".

Nyaso alinyamaza ili kumeza mate ya kulainisha koo.

"Ulisema huyo mtu ulimwona na kumtambua, lakini ulipopata fahamu ukawa hospitali hukuwa na kumbukumbu tena?", Willy aliuliza.

"Ndiyo, lakini hebu nikwambie jambo nililotaka ulisikie: Kwa sababu hiyo, mimi sina baba wala mama, sina hata ndugu yeyote. Ndugu wa pande mbili za wazazi wangu walikaa kimya. Hakuna hata mmoja wao aliyejitokeza kunichukua kutoka kwa masista ili anitunze. Ufahamu Willy kwamba mimi nilikuwa mdogo hivyo sikujua mambo mengi. Ndio sababu naitwa Nyaso tu, basi!".

# SURA YA KUMI

**NYASO** alinyamza kidogo na kisha akaendelea. "Maisha yangu ya utoto yalikuwa ya ukiwa ingawaje wafadhili wangu walinipa kila kitu nilichohitaji. Sasa jambo la ajabu ni kwamba, nilipokuwa nasoma Kidato cha Sita, wanafunzi wa shule ya sekondari ya Kibosho tulipatwa na ajali. Baada ya kumaliza muhula wa kwanza shule ilifungwa. Tulikodishiwa gari litupeleke mjini Moshi tayari kwa safari ya kwenda likizo. Lakini humo njiani, kabla ya kufika mjini, gari lilipinduka. Mimi nilikuwa mmoja wa wanafunzi waliopata majeraha kichwani, hivyo nikalazwa K.C.M.C.

Nilipokuwa nimelazwa niliota ndoto kuhusu siku ile ya mauaji ya familia yetu. Ndoto hiyo ilinionyesha mambo yote yaliyokuwa yametokea siku hiyo; mpaka mtu yule aliyekodi majambazi yaliyoteketeza familia yangu. Niligutuka toka usingizini na kujikuta nimezungukwa na madaktari na huku jasho likinitoka mwili mzima".

"Nilipoulizwa na madaktari nilikuwa najisikia vipi, niliwajibu kuwa nilikuwa najisikia salama wote walishangaa! Hapo hapo muuguzi mmoja alinieleza kwamba wakati nikiwa usingizini nilikuwa napiga kelele na kuhangaika. Alisema kwamba hata wao walikuwa na wasiwasi kuwa huenda nilikuwa karibu kukata roho".

"Ina maana njozi ile njozi hiyo ilikufanya umkumbuke yule mtu aliyekodi majambazi", Willy aliuliza kwa shauku kubwa.

"Ndiyo, na siku hiyo hiyo niliruhusiwa nikatoka hospitali nikiwa mzima kabisa. Mtu yule nilikuwa namfahamu tangu nikiwa mtoto, kwanza alikuwa rafiki yake marehemu baba yangu", Nyaso alisema na kuanza kulia tena.

"Jikaze ili uweze kunimalizia kisa hiki", alidakia Willy.

"Je, ukimwona sasa unaweza kumtambua".

"Ndiyo, kwani mara nilipotoka usingizini nilimkubuka barabara. Zaidi ya hayo, mtu huyo anaishi hapa hapa Arusha na ni mtu mkubwa sana. Wakati huo nilipata wazo la kwenda polisi kueleza kisa hicho, lakini nilijuwa hakuna hata mtu mmoja ambaye angeniamini. Kwanza miaka mingi ilikuwa imepita, na pili, mtu huyo alikuwa tayari kizito. Watu wangefikiri mimi nimekuwa kichaa kwa sababu ya ajali".

"Wewe uliamua kufanya nini", Willy aliuliza.

"Nilifikiri sana juu ya hali hii, halafu nikaamua kulipiza kisasi".

"Niliamua kuchukua hatua mimi mwenyewe, kwani Serikali ilishindwa kuwakamata na kuwaadhibu wauaji hao. Niliona ni bora kuendelea na masomo kwanza, kitu ambacho nimefanya mpaka nikahitimu elimu ya Chuo Kikuu. Baada ya masomo niliwaomba ruhusa masista ambao walinitunza ili niweze kufanya kazi serikalini. Waliniruhusu na kunitakia kila la heri. Lakini mpaka sasa huwa ninakwenda kuwajulia hali kwa sababu nawaona kama wazazi wangu. Unaelewa, wakati nikiwa shuleni nilikuwa naitwa Nyaso wa masista".

"Sasa wewe umeamua kulipiza kisasi kwa njia gani?", Willy aliendelea kuuliza.

"Usiniulize swali hilo. Tangu nimeota ndoto ile sasa yapata miaka minane. Kwa muda huo nilikuwa nikipanga na kupangua. Sasa naamini nimefikia uamzi sahihi juu ya namna gani nitalipiza kisasi. Jukumu hili ni langu mwenyewe. Willy. Najua nitafanya nini. Kulipiza kisasi ni lazima".

"Nilipohitimu masomo ya Chuo Kikuu nilipangwa kufanya kazi katika Wizara ya Uchumi na Mipango. Niliomba kituo changu cha kazi kiwe Arusha, kwani hapo ndipo alipo mbaya wangu".

"Je, mtu huyo anajuwa kuwa wewe ni mtoto wa Dk. Soni?".

"Hapana. Hawezi kujua kwa sababu mimi situmii jina hilo. Najulikana kama Nyaso wa masista, basi. Na hii imeweza kunisaidia sana, kwani huyu mtu naonana naye mara nyingi, lakini hawezi kunitambua. Yeye ni mtu maarufu hapa, hivyo ni rafiki wa watu maarufu kama akina F.K".

"Ahaa, kwa hiyo urafiki wako na F.K una uhusiano na mtu huyo?".

"Siyo hivyo. Urafiki wangu na F.K ulitokana na sababu tofauti kidogo".

"Kuhusu mpango wangu wa kulipiza kisasi, mimi nilihitaji uwezo mkubwa kipesa. Ilinibidi nifanye kila liwezekanalo ili nipate mtu anayeweza kunipa uwezo huo. F.K ndiye aliyeonekana kuwa mtu wa kukidhi haja yangu. Hivyo nilitupa ndoano yangu, na F.K akanasa. Kwa hiyo lengo langu limetimizwa; fedha za kuendeshea operesheni yangu sasa ninazo. Ninaweza kuanza pole pole kutekeleza mpango wangu. Sasa najisikia nafuu kwani nimemweleza mtu historia yangu".

Willy alimwangalia Nyaso kwa makini na mshangao vilevile. Mara alikumbuka maneno aliyoambiwa na mama yake mzazi: Mwanangu Willy kila mara jihadhari na wasichana warembo kwani wana mambo.

"Loh, kumbe Nyaso umeishi maisha ya taabu sana, lakini napenda nikushauri kuwa siyo vizuri kulipiza kisasi kwani matokeo yake yanaweza kuwa mabaya zaidi; janga linazua janga. Hivyo ninaku....".

"Ngoja ngoja, Willy", Nyaso alimkata kilimilimi. "Mahali nilikofikia siyo pa kurudi nyuma. Janga gani linaweza kunitokea mimi zaidi ya kufa? Mie siogopi kufa. Unajua kwa nini familia yangu ilipouawa Mungu alininusuru? Alifanya hivyo ili niweze kulipiza damu ya familia yangu ambayo ilimwagika bila makosa".

"Je, unajua kwanini mtu huyu alipanga familia yako iangamizwe?".

"Ndiyo, najua lakini siwezi kukwambia. Nimekwambia mambo mengi ambayo nafikiri yanakutosha. Najua wasiwasi wako unatokana na kuwaza kwamba nikauawa pia. Mimi niko tayari kufa ili niungane na familia yangu huko peponi. Kula nyama uondoke wala usiniangalie kwa masikitiko hivyo".

Palepale Willy alijuwa kuwa Nyaso alikuwa amepania kutekeleza matakwa yake. Lakini alimsikitikia sana msichana yule kwani alijua kwamba alikuwa mgeni katika mambo kama hayo. Hivyo alijua kwa vyovyote Nyaso angekuwa na mwisho mbaya, hata kama mipango yake ilikuwa mizuri. Hata hivyo Willy alimwona Nyaso alikuwa msichana jasiri na kwa sababu hiyo alimheshimu sana. Kutokana na hali hiyo, Willy aliamua kumpasha mambo ambayo yangemfanya msichana huyu awe tayari kusaidiana naye, hasa kuhusu Chris Tondo na F.K.

"Sikiliza Nyaso", Willy alisema. "Tangu nilipokuona mara ya kwanza nilijua wewe ni mtu wa aina gani. Wewe ni msichana mwenye sura nzuri sana. Ninathubutu kusema umependelewa sana jinsi ulivyoumbika. Vile vile wewe una akili nyingi sana na usafiri kinyume cha wasichana wengi. Unao uwezo wa kumudu mapambano".

"Hebu wacha kunipamba na sifa nyingi". Nyaso alimkatiza. "Mimi nimeshasikia nikipewa sifa za kila aina".

"Sikiliza, Nyaso. Sifa ambazo umezisikia ni kutoka kwa wanaume walaghai wenye kukutaka mapenzi. Nia yangu siyo hiyo, la hasha. Kama hali ya mapenzi ikitokea kati yangu na wewe, basi itakuwa katika hali ya kawaida na siyo kwa kughilibu. Kitu ninachotaka kusema ni kwamba nilikuwa sijaona msichana aliyebarikiwa kama wewe mpaka akawa na akili nyingi, sura nzuri isiyoelezeka na pia hekima na ujasiri. Kwa sababu ya yote hayo. nimekuheshimu. Ndiyo sababu nami nimeamua kukueleza juu ya maisha yangu mwenyewe na kwanini niko hapa".

Willy alimtolea Nyaso jicho la mahaba.

"Usiniangalie hivyo na kuniumiza roho", Nyaso alilalamika. "Sema tu unavyotaka kusema".

"Kama nilivyokwambia hapo awali", Willy alisema. "Mimi naitwa Willy Gamba. Watu wengi wananijua kama mfanyabiashara. Lakini ukweli ni kwamba mimi ni mpelelezi katika Idara ya Upelelezi Tanzania".

"Kweli", Willy alimthibitishia.

"Nimewahi kusikia tetesi kama hizo", Nyaso alidakia. "Ndiyo sababu nikakwambia nimewahi kusikia jina lako. Lakini watu wengine husema kuwa habari zote kuhusu jina hilo huwa ni hadithi tu na wala hakuna mtu wa namna hiyo ambaye anaishi hapa duniani. Lakini tangu nilipokuona kwa mara ya kwanza, niliona vitendo vyako vinafafana na vile vya huyo Willy anayesifika. Sasa naamini kwamba ni wewe hasa. Nafikiri ninayo bahati kubwa kukufahamu. Sina shaka wewe utakuwa mwali wangu katika operesheni ninayotarajia kuendesha ili kullipiza kisasi".

"Usijali, ngoja kwanza nikueleze kilichonileta hapa", Willy alimwambia Nyaso.

"Baadaye utaona kwamba mambo mengine pamoja na hayo ya kwako ni kama mchezo".

"Sawa, Willy, ninakusikiliza".

"Basi tega masikio nikueleze toka mwanzo hadi mwisho".

Willy alimweleza Nyaso yote yaliyokuwa yametokea, kwanini alikuwa Arusha na tuhuma zake dhidi ya Chris Tondo na huenda F.K vile vile.

"Kwa hiyo Nyaso", Willy alimaliza. "Ninakuomba unisaidie kwa kunipa habari ambazo zinaweza kunisaidia katika mapambano dhidi ya majasusi wa Afrika Kusini. Ushindi wetu ni wako vile vile".

Nyaso aliyekuwa anamsikiliza Willy kwa makini, alimtolea tabasamu la mwaka kisha akasema. "Usiwe na wasiwasi, Willy. Mtu kama wewe ndiye nilikuwa natafuta tokea siku nyingi. Tangu sasa hivi mimi niko mikononi mwako. Msaada wowote utakaohitaji kutoka kwangu hesabu kuwa umepata".

Willy alijisikia joto la mwili likipanda, lakini akaamua kutoruhusu hali hiyo iendelee mpaka hapo kazi iliyokuwa mbele yao itakapokuwa imemalizika.

"Nyaso", Willy alisema. "Ninakuomba unieleze yote kuhusu maisha ya F.K pamoja na shughuli zake kibiashara. Yale yanayohusu maisha yenu kama bibi na bwana unaweza kuyaacha".

Nyaso alimweleza Willy yote anayojuwa kuhusu F.K., Chris Tondo pamoja na shughuli za Nyoka Tours and Safaris.

"Kama unahisi hapa majasusi wamejificha mahali, basi ni nyumbani kwa F.K", Nyaso alisema. "Kama nilivyokueleza mimi na F.K tumekuwa marafiki kwa muda mrefu. Lakini nimefika nyumbani kwake mara chache. Nyumba yenyewe imejengwa kinamna, kwani White House ni Wihite house hasa. Ni kama Ikulu; hata sijui unaweza vipi kuingia ndani ya jumba hilo".

"Je, F.K hajawahi kukueleza kitu chochote ambacho kinaweza kunisaidia kuingia ndani ya jumba hilo?".

"Kitu ninachokumbuka ni kwamba, wakati penzi letu lilipokuwa bado moto moto, F.K alinichukua ili nikalale kwake. Hii ilikuwa moja ya safari tatu tu ambazo nimewahi kulala kwake. Wakati tulipokuwa tunazungumza, nilionyesha wasiwasi wangu kuhusu yeye kuishi peke yake katika jumba kubwa vile. Nilimweleza kuwa angeweza kushambuliwa na majambazi kwani alijulikana kuwa ni mtu tajiri sana. Lakini yeye alinihakikishia nisiwe na wasiwasi kwani jumba lake lilikuwa limejengwa kwa namna yake. Aliongeza kusema kuwa kama angevamiwa, angweza kutumia njia za siri ambazo ziko chini kwa chini mpaka akatokea nje ya seng'enge, ili akawajulishe polisi. Kwanza nilifikiri alikuwa anajigamba tu. Unajuwa wanaume wengi hupendelea kujionyesha mbele ya wanawake kwamba wao ndio wenyewe. Lakini baada ya kusikia tuhuma dhidi yake, naamini alikuwa anasema kweli".

"Sehemu yake ina eneo gani?", Willy aliuliza.

"Ekari kumi na mbili", Nyaso alijibu.

Willy aliangalia saa yake na kuona ilikuwa saa mbini na nusu usiku.

"Nyaso", Willy aliomba. "Hebu twende ukanionyeshe kwa Chris Tondo. Ningependa nizungumze naye kidogo".

"Sawa Willy, lakini huenda tusitumie gari langu kwani linajulikana sana. Hapo nyumbani kwangu kuna gari la rafiki yangu kutoka Nairobi, aliliacha pale halafu alipanda ndege kwenye Dar es Salaam. Heri tukatumie gari hilo".

"Mawazo yako ni sahihi. Je, lina namba za Kenya?".

"Ndio".

"Haya twende. Si wewe mwenyewe unataka pilika pilika? Sasa basi zimeanza", Willy alimtania Nyaso.

Waliunuka toka vitini na kuondoka.

Chris Tondo alikuwa anaishi sehemu inayojulikana kama 'Corridor Area! Wakati Willy na Nyaso walikuwa wanaelekea huko kupitia barabara ya Haile Sellasie, walipishana gari dogo aina ya Datsun.

"Gari hilo ni la F.K. na anaendesha mwenyewe. Kwa kawaida huwa haliendeshi gari hilo. Mara nyingi huwaachia watumishi wake na yeye anatumia ile Benz yake, kwani anazo gari tatu hapo nyumbani kweke", Nyaso alimwambia Willy mara walipopishana na ile Datsun.

F.K. alikuwa hakuwatambua.

"Huenda amechoka kuendesha magari makubwa", Willy alisema.

"Nyumba ya Chris Tondo ni ya nne kutoka nyumba hiyo hapo".

"Basi, egesha mahali pazuri na mimi nitatoka kwa muda wa robo saa", Willy alimwambia Nyaso.

"Mimi nitaingia katika nyumba hii kumwona rafiki yangu", Nyaso alisema

"Nitatoka baada ya robo saa ambapo wewe pia utakuwa tayari. Tafadhali Willy, kama watu hawa ni hivyo unavyohisi, basi ni watu wabaya, ni vizuri kuchukua tahadhari wasije wakakudhuru".

"Usijali, tutaonana baada ya dakika hizo", Willy alisema huku akitokomea gizani.

Nyaso aliyekuwa anamwangalia Willy huku akimwemwesa alijikuta anajisemea kimoyomoyo. "Jinsi nilivyomzoea! Utafikiri tumeishi naye miaka mingi. Hivi sasa ninavyojisikia ovyo kumkosa hiyo robo saa".

Nyaso aliondoka akaenda kubisha hodi mlangoni kwa rafiki yake.

Willy aliambaa kwenye nyufa za nyumba jirani na ile ya Chris Tondo. Aliwaona vijana wawili kwa mbali wakipotea kwenye giza la michongoma ya nyumba iliyotazamana na ile ya Chris Tondo. Mara alitambua wale walikuwa vijana wa Hamisi. Kwa kuwa hakutaka wamwone, Willy alijipeneyza kwenye sehemu ya

kushoto ya ua. Kwa ustadi kama wa paka Willy alipanda ukuta na kudondoka uwani bila kishindo.

Aliangaza huku na kule na kwa bahati nzuri aliona dirisha kwa upande huo liko wazi. Aliona taa ilikuwa inawaka kwenye chumba upande wa sebule. Willy alihisi kilikuwa chumba cha kulala cha Chris. Basi alijinyanyua, akakwea hadi ndani ya nyumba kupitia dirishani. Huku bastola ikiwa mkononi mwake. Willy alijikuta kadondoka bafuni. Alipofungua mlango taratibu alijikuta yuko kwenye njia nyembamba iliyokuwa inatenganisha vyumba. Aliamua kwenda sebuleni ambako alihisi Chris angekuwepo.

Willy alifungua mlango kwa ghafla ili asimpe nafasi Chris ya kuwa tayari kujihami. Lakini alishangaa kukuta chumba kile kilikuwa kitupu. Taa ya mle chumbani ilikuwa inawaka na Willy aliona jinsi chumba kile kilivyokuwa cha fahari isiyo kifani. Alijongea na kuelekea kwenye chumba kingine ambacho kilikuwa kinawaka taa pia. Hata hivyo, Willy alishangazwa na ukimya uliokuwa ndani ya jumba hilo.

Alifikiri labda walipopishana na gari la F.K. Nyaso alikuwa hakuona vizuri kwani huenda hata Chris alikuwa kwenye gari lile lile. Wakati anafikiri yote hayo, aliamua kuendelea na mpango wake. Kwa kasi kama umeme Willy alifungua mlango wa chumba hicho. Kumbe loo mle ndani alikuta maiti tatu! Baada ya kuangalia vizuri aligundua kuwa watu watatu hao waliuawa kwa kupigwa risasi. Walikuwa ni Chris Tondo, msichana mmoja mrembo sana ambaye Willy alihisi kuwa alikuwa binti yake Chris pamoja na mlinzi mmoja kutokana na mavazi yake..

"Bila shaka kazi hii ni ya F.K.; ameniwahi", Willy alijisemea kwa uchungu.

Bila kupoteza muda, alitoka nje kwa kupitia njia aliyokuwa ameingilia. Alipokuwa nje alimwona Nyaso naye anatokea kwenye lango la nyumba ya rafiki yake, walipoingia ndani ya gari, Willy alimwambia Nyaso.

"Hebu endesha gari haraka ili tutoke kwenye sehemu hii. Chris, mlinzi wake pamoja na binti yake wameuawa. Nipeleke hotelini kwangu kwani sasa kazi imeanza", Willy alimwambia Nyaso.

"Huyo ni F.K. Willy, ndiyo sababu tulikutana naye akitoka huku", Nyaso alisema.

"Bila shaka", Willy alikubaliana na Nyaso.

"Masikini Betty kauawa bure mtoto wa watu. Mimi ndiye niliyemfahamisha kwa Chris, oh Betty! Willy uliyohisi ni kweli. F.K. utakiona ", Nyaso alisema kwa

uchungu. Aliendesha kuelekea New Arusha Hoteli. Willy alipoangalia saa ilikuwa saa tatu na robo. Alikuwa amechelewa robo saa lakini alikuwa amejua mengi.

# SURA YA KUMI NA MOJA

## KABLA YA USIKU WA MANANE

Wakati Willy na Nyaso walipokuwa wanaelekea New Arusha Hoteli. F.K. alikuwa amewasili nyumbani kwake. Alikuwa akiwaeleza wenzake kazi aliyokuwa ameifanya.

"Kazi mliyonituma nimeimaliza tayari", F.K alisema.

"Vema", George alijibu.

"Sasa ni saa tatu na dakika kumi, mipango yetu itaanza saa ngapi?", P.G aliuliza.

"Hebu nisikilize kwa makini", George alieleza. "Nilikuwa kwenye chumba cha habari na nimewasiliana na Kamanda wa KULFUT huko Afrika ya Kusini. Nilipompa habari kuwa tayari tumepoteza watu wawili alikasirika sana na kuniambia kwamba asingependa kusikia kitu kama kile tena. Alisema jambo hilo lilikuwa kinyume cha nia ya matakwa ya Serikali ya Afrika Kusini ambayo ni kuleta 'hofu' isiyoelezeka dhidi ya wapigania uhuru, nchi zilizokuwa mstari wa mbele na Afrika huru kwa ujumla.

"Ameongeza kuwa usiku wa leo lazima uwe usiku wa kazi. Hapo kesho Kamanda anataka kusikia habari za kilio kutoka Tanzania na Afrika nzima. Kama mjuavyo mkutano wa wapigania uhuru umepangwa kuanza kesho saa tatu. Lakini amri tuliyopewa ni kwamba mkutano huo usiwepo, na badala yake kuwe na vilio. Wale watakaokuwa wamesalimika watakuwa wanaikimbia Tanzania bila mpangilio wowote. Wakati dunia nzima itakapokuwa inalaani kipigo tutakachokitoa kwa Tanzania, majeshi yetu ya Serikali ya Afrika Kusini yatavamia Msumbiji, Botswana, Zambia, Zimbabwe na Angola hapo kesho. Watu wa nchi hizo watabaki wamechanganyikiwa. Wakati dunia nzima inagwaya, jeshi letu la polisi litafyekelea mbali watu weusi wenye kuleta ghasia ndani ya Afrika Kusini. Tutawachinja kama kuku na hivyo kuzima kabisa maasi wanayoita ukombozi".

"Ndio mnaona umuhimu wa kushinda katika mapambano yetu. Kamanda wetu amenipa majina ya viongozi wanne wa wapigania uhuru. Ameongeza kwamba hao wakiuawa wote kwa siku moja, itakuwa ni kipigo cha kutosha hata kuzima vugu vugu la maasi katika Afrika kwa muda mrefu. Majina ya viongozi hao ni Mbeki, Jamana, Ntamazi na Basweka. Je, F.K una habari kuwa watu hawa wamewasili?".

"Ndiyo, wote hawa wamefikia Mount Meru Hoteli na namba za vyumba vyao ni hizi hapa", F.K alisema huku akimpa kijikaratasi chenye maelezo kamili juu ya viongozi wake.

"Umefanya kazi nzuri, F.K", George alimpongeza F.K.

"Ahsante, kazi nzuri lazima ifanyike George ili lengo letu liweze kutimizwa", F.K alisema.

"Sina shaka", George alisema. "Viongozi hawa wanalindwa sana. Askari polisi, maafisa usalama na hao wapelelezi mashuhuri watatu wamewazunguka viongozi hao, hasa kutokana na mambo yaliyotokea jana. Tumshukuru F.K kwa kuhakikisha usalama wetu na kukaa bila adui kujua tuko wapi huku tukipata habari bila matatizo".

"Hayo yote ni matunda ya mafunzo yako thabiti, kama Mwalimu wangu", F.K alijibu kwa unyenyekevu.

"Hivyo", George alieleza. "Mpango ni kama ifuatavyo; kwanza kabila lazima tuwakorofishe hawa wapelelezi watatu. Bila kufanya hivyo, kazi yetu ya kuwafyekelea mbali viongozi hawa itakuwa ngumu. Kwa hiyo, mimi nimepanga kwamba ni lazima Willy Gamba auawe leo kabla ya usiku wa manane, inaonekana huyu ndiye ngao ya wengine waliobaki. Yeye akiuawa wenzake watabaki wamegwaya na kuchanganyikiwa wasijue la kufanya. Hawataweza kuchukua hatua yoyote kwa leo kwani watahitaji muda mrefu kutayarisha mpango mpya, bila kuwa na Willy Gamba. Hii itatupatia muda sisi kufunga kazi, Kabla ya jua kuchomoza, kazi yetu itakuwa imekamilika".

"Mtu huyu atauawa vipi", P.G aliuliza.

"Mpango wa kumuua Willy utakuwa kama ifuatavyo, F.K na vijana watatu watakwenda nyumbani kwa mzee Hamisi. F.K alieleza kwamba familia ya mzee Hamisi iko likizo, hivyo yeye anakaa peke yake kwa wakati huu. Vile vile tunafahamu kuwa Willy na mzee Hamisi wanafanya kazi bega kwa bega, kwani habari zote kutoka kwa bosi wa Willy zinapitia ofisini kwa mzee Hamisi. Hivyo F.K na wenzake watamlazimisha mzee Hamisi amwite Willy Gamba kwa simu toka hapo hotelini kwake. Mzee Hamisi atalazimishwa kumwambia Willy aje nyumbani kwake ili ampe habari muhimu sana kutoka kwa bosi wake. Bila shaka Willy atakuja na mtego wetu utamnasa. Atauawa tu", George alisema huku akitabasamu alipoona nyusa za wenzake zimejaa furaha baada ya kusikia mpango wake.

"Kweli naamini unastahili kuwa kiongozi wetu", Dave alisema. "Kwenye mtego kama huu hata mimi ningenasa tu".

"Lakini vijana watatu hawatoshi, mtu huyu ni mbaya sana", F.K alisema kwa sauti ya woga.

"Oke, nitakwenda nao mimi mwenyewe", Dave alijigamba.

"Hapana", George aliingilia kati. "F.K atakwenda na hao vijana, bali tu tutamwongeza mmoja zaidi ili wawe wanne. Wewe mwenyewe Dave unajuwa kwamba vijana wetu wanao ujuzi mkubwa. Vile vile mfahamu kuwa wakati Willy akiitwa kwa mzee Hamisi hatachukua tahadhari kubwa, kwani hatahisi kitu chochote kibaya. Hivyo kazi yao itakuwa rahisi kama mtelemko. Mara tu baada ya mzee Hamisi kumwita Willy, naye lazima auawe. Baada kumuua Willy vijana wetu watarudi huku haraka kwa kazi nyingine ya baada ya usiku wa manane. Mimi, P.G na vijana wawili tutakwenda kukagua mazingira Mount Meru Hoteli na vile vile jumba la Kimataifa ambamo mkutano unatarajiwa kufanyika. Tunataka kutega mabomu ya masaa kwenye sehemu hiyo. "Kwa hiyo F.K, baada ya kumwita Willy na kumuua Hamisi, kazi nyingine utawaachia vijana. Wewe utachukua gari la Hamisi kwani litahakikisha usalama zaidi, halafu utufuate Mount Meru Hoteli ili utuonyeshe chumba cha mikutano ambamo tunatarajia kutega mabomu. Baada ya kumuua Willy. Vijana warudi huku haraka kwa gari lako. Wewe Dave utabaki hapa na vijana watatu mkisubiri kazi yenyewe ya usiku wa manane. Mipango zaidi nitawajulisha saa tano usiku wakati tukijitayarisha kwenda kwenye mapambano yenyewe. Naamini nyote mmenielewa?".

"Mpango ni barabara kabisa", Dave alisema huku akijinyoosha nyoosha.

"Hivi ni kwanini mnataka kutega mabomu? Si hawa watu tutawaangamiza usiku huu ili mkutano usifanyike kesho?", P.G aliuliza.

"Katika kazi hii hakuna kuacha mwana hata kidogo, kama hatukufanikiwa kuwauwa wote kwa leo, basi wale watakaodiriki kuendelea na mkutano kesho, nao watauawa vile vile", George alijibu huku akitabasamu.

"Baada ya kufunga kazi sisi tutaondoka vipi hapa?", Dave aliuliza.

"Usiwe na wasiwasi", George alijibu. "Mipango yote imeshakamilishwa na F.K; ukipata muda ingia chumba namba kumi".

"Haya, twende kazini vijana. Mungu atusaidie", P.G alisema.

"Amin!", wengine walijibu kwa pamoja huku wakiinuka na kujitayarisha kuondoka.

Ilikuwa yapata muda wa saa tatu na nusu usiku, Willy na Nyaso walibisha hodi kwenye chumba cha Willy baada ya kujua kwamba wenzake walikuwa wanamsubiri ndani. Willy na Nyaso walikuwa wamefika pale chumbani kwa kupitia njia tofauti kama walikuwa hawafahamiani. Willy alikuwa amepanda kwa kutumia ngazi, wakati Nyaso alitumia lifti.

"Nani", Bon aliita kwa sauti.

"Willy".

Bon alifungua mlango huku akiwa na bastola mkononi. Alipomuona msichana Bon alirudisha mlango haraka haraka.

"Na wewe woga umezidi, karibu ndani Nyaso", Willy alimkaribisha huku akirudisha mlango baada ya Nyaso kuingia ndani.

"Maama", Mike alisema kwa mshangao.

"Nini?", Willy aliuliza kwa kebehi.

"Wewe huwa unawatoa wapi hawa?".

"Malaika huyu ama mwanadamu?", Mike aliendelea kushangaa.

"Wewe unafikiri vipi?", Willy alimuuliza.

"Malaika", Mike alijibu huku wote chumbani wakimwemwesa.

"Subiri sasa niwafahamishe kwa huyu 'malaika'. Mtoto huyu anaitwa Nyaso. Ni Nyaso tu. Msiulize zaidi. Nyaso hawa ndiyo rafiki zangu niliokuwa nikikueleza. Yule maneno mengi ni 'Kikuyu' toka Kenya. Huyu ni Bon toka Afrika Kusini na yule pale anayejifanya mkimya ni Rocky kutoka Zimbabwe", Willy alisema.

"Nashukuru kuwafahamu", Nyaso alijibu.

"Sisi ndiyo tunapaswa kushukuru kwani kumfahamu mtoto mzuri kama wewe ni fahari ati", Mike alisema.

"Willy kweli watanzania mnatoa watoto, mimi sina hata maneno. Hivi vijana wa hapa mtaweza kujenga?, Mtoto kama huyu akisema umpe mshahara wako wote wa mwezi unaweza kukataa? La hasha rocky alisema.

"Ahsante kwa sifa ulizonipa", Nyaso aliitika.

"Sikia sauti yake nyororo", Bon aliongeza.

"Wacha sauti na sura, Nyaso anayo mengi zaidi", Willy aliasa.

"Haya Willy, umemleta huyu mrembo ili tukusifu ama unayo mengine zaidi?". Mike aliuliza.

"Wacha maneno mengi, nyinyi wakenya mkijua kiswahili kadiri, sisi watanzania huwa watufui dafu", Willy alisema.

"Hayo ndio maendeleo", Mike aliongeza.

"Hebu jamani, nisikilize kwa makini. Sikuja na msichana huyu ili kuwakoga. Kusema kweli mambo yamepamba moto tayari na ni lazima na sisi tuwemo kazini", Willy alisema halafu aliwaeleza juu ya mazungumzo yake na Nyaso, juu ya F.K na mwisho jinsi walivyokwenda kwa Chris na kukuta ameuawa.

"Tunao uhakika kuwa F.K ndiye aliyefanya mauaji hayo. Mimi ninahisi amekuwa na wasiwasi baada ya kusikia kwamba mimi nimemhoji sana Chris. Kwa hiyo aliamua kutumia mbinu zile zile za siku zote: Yaani maiti hawana maneno. Hii ina maana kwamba fumbo limefumbuliwa tayari. Majasusi tunaowatafuta wamejificha kwa F,K. Kutokana na maelezo ya Nyaso kuhusu jumba la F.K. lilivyo ni dhahili kwamba majasusi hao wako mle ndani, hivyo kazi imebaki kwetu", Willy alisema.

"Sasa mipango iko vipi bosi?", Bon alimwuliza Willy.

"Kwanza kabisa mimi na Nyaso tutakwenda kufanya uchunguzi kwenye jumba la F.K. kama nilivyowaeleza, jumba hilo linazo njia za chini kwa chini. Na kama hivyo ndivyo, basi mle kuna sehemu nyingi ambazi ni za siri. Kwa sababu hiyo mimi naona ni bora niende na Nyaso ambaye atanionyesha mahali jumba hilo lilipo. Baada ya kufanya utafiti, nitarudi hapa ili tujadili jinsi gani ya kuwakabiri hao majasusi usiku huu, ama mnasemaje?", Willy aliuliza.

"Hisia zetu ni sahihi. Sasa kwa nini sisi sote tusivamie jumba hilo mara moja na kufunga kazi", Mike alipendekeza.

"Hapana Mike, huenda kazi yenyewe isiwe rahisi kama unavyofikiri. Haitakuwa vizuri sisi sote kujitumbukiza bila kufanya uchunguzi. Uwezekano wa kuangamia sisi sote upo, na hilo litakuwa pigo kubwa kwa Afrika huru na kwa wapigania uhuru wa Afrika Kusini. Hivyo utakuwa ushindi kwa makaburu. Amini usiamini, mapambano yanayoendelea huko Afrika Kusini, kwa kiwango kikubwa, yanategemea ushindi wetu", Willy alijibu.

"Mimi nakubaliana na wewe kabisa", Bon alisema halafu akaendelea, "Kusema kweli, vita kamili vimeanza ndani ya Afrika Kusini. Ushindi wetu hapa utawatia hamasa vijana wa kizalendo ambao wanapambana na askari wa makaburu. Nia ya makaburi ni kutuvuruga sisi huku na kufanya wana-ukombozi walio ndani na nje ya Afrika Kusini kuchanganyikiwa. Vita vya Ukombozi tayari vimevuka hatua ya kutumia mawe na marungu. Awamu hii ni ya kutumia silaha za moto. Hivyo, na sisi tuwe tayari kujitoa muhanga ili matunda ya uhuru yapatikane kwa watu wetu", Bon alisema.

Willy alikuwa karibu kuzungumza jambo fulani, mara simu ililia. Wote waliangaliana halafu Willy aliamua kusikiliza simu.

"Hallo", Willy aliitikia.

"Mimi ni mzee Hamisi, naomba kuzungumza na Willy", sauti ya mzee Hamisi ilisikika.

"Mwenyewe nazungumza, habari za saa hizi mzee", Willy alijibu.

"Habari ni nzuri, Willy nakuhitaji uje hapa nyumbani kwangu haraka kwani nina habari muhimu sana", Hamisi alisema, Willy alisita kidogo halafu akamjibu.

"Sawa, nakuja", halafu alikata simu bila kusema maneno zaidi.

"Huyo ni nani?", Mike aliuliza.

"Ni mzee Hamisi, anasema ni lazima niende nyumbani kwake kwani ana habari muhimu", Willy alibu.

"Hivi sasa itabidi mimi, Rocky na Nyaso tuandamane mpaka kwenye jumba la F.K. Sisi tutafanya utafiti halafu turudi hapa", Bon alishauri.

"Hiyo ni sawa, wewe Mike huna budi kubaki hapa. Kama kuna habari zozote, tutawasiliana. Bon na Rocky ni lazima kuchukua tahadhari kubwa kwani katika mazingira ya jumba kama lile, kunaweza kukatokea jambo lolote", Willy aliasa.

"Huyu Hamisi anakaa wapi?", Nyaso aliuliza.

"Anakaa kwenye nyumba za maafia huko Kijenge, karibu na barabara iendayo Themi Hill. Kwa hiyo tutaondoka wote halafu nyinyi mtaniacha barabarani. Baada ya kuzungumza na mzee Hamisi, mimi nitatafuta njia yangu mwenyewe ya kurudi ili tukutane hapa tena. Sasa Nyaso, wewe telemka chini na kutusubiri kwenye gari", Willy alielekeza.

Wote watatu walichukua silaha ambazo walifikiri wangezihitaji. Willy pia, ingawa alikuwa anakwenda kwa mzee Hamisi, alichukua silaha akiwa tayari kwa lolote. Wanaume walishajuwa kwamba walikuwa wanawinda na huku wakiwindwa. Mike ambaye alikuwa na jukumu la kubaki pale hotelini, naye alikaa tayari na silaha zake. Walipokuwa tayari, walielekea kwenye gari huku kila mmoja akitumia njia tofauti na wenzake.

"Ahsante". F.K. alimwambia mzee Hamisi baada ya kuzungumza na Willy.

"Hebu ondoa huo mtutu wa bunduki kwenye kichwa changu. Unajua mimi ni mzee sana na kuniweka katika hali hii kunaweza kunisababisha nipate ugonjwa wa moyo. Kazi uliyotaka nimekufanyia, zaidi unataka nini", mzee Hamisi aliuliza.

"Ha ha", F.K. aliangua kicheko kwa jeuri halafu akaendelea, "Mzee Hamisi sina budi nikushukuru kwa yote uliyonifanyia, maana bila kupata habari ulizonipa mipango yangu isingefikia hatua hii. Wewe ni mtu mwenye ujuzi na uzoefu katika shughuli za usalama. Sina shaka umeshahisi kitu gani kinatendeka baada ya kuona unavamiwa na kundi la Wazungu. Hawa ni askari kutoka Afrika Kusini. Ufahamu fika kwamba wewe ni msaliti wa nchi yako. Hii imetokana na nyinyi watu wenye vyeo Serikalini kupenda pesa. Pesa nilizokupa zilikufanya uisaliti nchi yako. Ha ha! Uchu wa pesa utaimaliza Afrika. Je, unajua adhabu ya usaliti ni nini", F.K. aliuliza kwa kebehi.

"Usiniue F.K. kwani hata ukiniua, Willy atakumaliza...", Hamisi alisema huku akipapatika.

"Stumke, fanya kazi yako", F.K. aliamrisha, mzee Hamisi aliinuka na kabla hajachukua bastola yake kutoka kwenye koti, alipigwa risisa ya paja na kichwani na kufa papo hapo.

"Sasa msubiri Willy. Nina imani kazi yenu itakuwa rahisi", F.K. alisema huku akimpa Stumke swichi ya gari lake. Stumke alikuwa kiongozi wa yale majasusi yaliyomvamia mzee Hamisi, na ambayo sasa yalikuwa yakimsubiri Willy. Baadaye F.K. alichukua funguo za marehemu Hamisi kutoka mezani kwake na kuaga.

"Stumke, tuonane nyumbani. Lakini nawashauri mkae macho sana. Ingawaje Willy atakuja bila tahadhari, ni mtu hodari kupindukia. Msimpe mwanya bali mtumie mbinu zote mnazozifahamu", F.K. alionya.

"Usiwe na wasiwas, F.K. mimi nilikwisha ongoza kundi hili hili na kuteketeza kikosi kizima huko Namibia. Itakuwaje tushindwe mtu mmoja?, Huyo mfute kutoka kwenye orodha ya adui walio hai. Labda asitokee!", Stumke alijigamba.

Willy na wenzake walikuwa wanaingia kwenye barabara kuu iendayo Themi Hill. walipishana na F.K. ambaye alikuwa akiendesha gari la Hamisi na kuelekea mjini. Si F.K. wala Nyaso ambaye alimtambua mwenzake kwani wote walikuwa wanaendesha magari ambayo hayakuwa yao. Lakini Willy aligeuka na kuliangalia gari hilo ambalo lilikuwa linakwenda kasi na kupotea gizani.

Hilo ni kama gari la mzee Hamisi", Willy alisema baada ya kugutuka.

"Itakuwaje akuite halafu atoke", Bon aliuliza kwa mshangao.

"Hapo sasa", Willy aliitikia.

"Kama una hakika ni lenyewe, basi hilo siyo jambo la kawaida", Rocky alisema.

"Huenda ameona nimechelewa hivyo akaamua anifuate", Willy alijibu.

"Lakini hatujachelewa hata kidogo", Rocky alijibu.

Wakati huo walikuwa wamekaribia sehemu ya Kijenge ambako Hamisi alikuwa anakaa.

"Nyaso! Simama hapo pembeni", Willy alisema, Nyaso alijisikia raha kwani alijua yeye alikuwa msichana peke yake aliyepata fursa ya kuwaendesha wapelelezi mashuhuri wa Afrika, hasa wakiwa katika harakati za mapambano. Alisimamisha gari pembeni mwa barabara na Willy akatelemka.

"Haya nendeni lakini jihadharini sana. Huko mwendako panaweza kuwa moto. Nawatakia kila la kheri", Willy alisema.

"Ahsante", Bon na Rocky walijibu kwa pamoja.

Nyaso aliendesha kuelekea Themi Hill baada ya kumwacha Willy. Willy naye taratibu aliambaa kwa kufuata ua wa sehemu hii kuelekea nyumbani kwa Hamisi. Nyumbani kwa marehemu mzee Hamisi Stumke alikuwa amepanga watu wake tayari.

"Mtu huyu akiingia sharti auawe pale pale. Hakuna kusubiri. Yeyote atakayekuwa kwenye sehemu nzuri ya kumuua lazima afanye hivyo mara moja. Kama tulivyokwisha ambiwa, mtu huyu ni hatari sana. Kila mtu awe macho", Stumke aliwaonya wenzake.

Stumke alitokomea gizani. Aliambaa kwenye ua huku akielekeza macho na mawazo yake kwenye lango la nyumba. Majasusi wengine wawili walikuwa wamejibanza kwenye ua. Mmoja wao mwingine alikaa langoni kwani yeye ndiye ambaye angemfungulia Willy. Kila wakati waliposikia muungurumo wa gari, walijiweka tayari lakini hakuna gari lililojitokeza pale nyumbani. Gari la Nyaso liliposimama Stumke kutokana na uzoefu wa kazi yake, alihisi huenda mtu wao angeweza kuteremshwa njiani na kuingia pale kwa kutembea. Hivyo aliwashauri watu wake wawe macho kama mtu huyo angeingia kwa miguu.

Kengere ya ilani ilizidi kulia kichwani mwa Willy baada ya kila hatua aliyopiga kuelekea kwenye nyumba ya Hamisi. Ilikuwa kawaida yake kwamba kila hali hiyo ilipotokea, Willy alichukua tahadhari ya hali ya juu. Wakati huo huo Willy alimua kupita mlango wa nyuma badala ya mbele ya nyumba ile. Alizunguka ua wa nyumba huku akinyatia kama nyani. Aliruka ua huo wa michongoma na kutua ndani kwa kishindo kidogo.

Jasusi aliyekuwa upande wa kulia aligutuka kidogo halafu akaamua kuja kuangalia kuna nini. Alikuja kwa mwendo wa kunyatia kiasi kwamba hakutoa sauti yoyote. Lakini kwa kuwa masikio ya Willy yalikuwa na uzoefu kama wa mnyama awindwaye porini, aliweza kusikia mtu anajongea. Willy aliinuka mara moja na kujibanza kwenye pembe ya kulia ya nyumba. Aliangalia kwa chati na kuona yule kaburu anasogea huku bastola ikiwa mkononi. Macho ya Willy kama ya wale majasusi yalishazoea giza. Hivyo aliweza kuona vizuri.

Willy alikuwa na bastola mkononi, mara akaamua kuirejesha mahali pake, akajitayarisha kumkabiri jasusi yule kwa mikono. Pale pale akijuwa kuwa kuitwa kwake kulikiwa ni mtego na kwa hiyo ilibidi awe tayari kwa mapambano.  Yule jasusi alisogea karibu kabisa na pale Willy alipokuwa amejibanza. Willy alimwacha afike kabisa kwenye usawa alipokuwa amesimama. Ndipo alipomrukia na kumkaba koo kiasi kwamba yule jasusi hakuwa na muda wa kuweza hata kukohoa. Willy alivunja shingo ya yule jasusi ambaye alikata roho bila kutoa sauti. Taratibu Willy aliilaza chini maiti yake.

Jasusi mwingine alipoona mwenzake anakawia kurudi, alitoa ishara kwa yule aliyekuwa kwenye lango. Alikuwa anamjulisha kuwa anaelekea nyuma ya nyumba. Wakati huo damu ya Willy ilikuwa tayari imechemka kwa hali ya vita. Mara alimwona jasusi mwingine anakuja mbio. Willy alimsubiri huku akimwemwesa kwani alikuwa anakwenda hovyo bila tahadhari yoyote. Lakini alipokaribia mahari Willy alipokuwa, yule jasusi alisimama kana kwamba alikuwa

amegutushwa na jambo fulani. Willy alijua kuwa kama angesubiri, bila shaka angeonekana. Kama risasi, Willy alifyatuka na kumrukia yule jasusi pale alipokuwa amesimama. Alimkata mkono wa karate na kumpasua kichwa. Wote walianguka chini.

Walianguka kwa kishindo ambacho kilimshitua Stumke na yule jasusi aliyekuwa kwenye lango. Wakiwa kama watu waliotiwa ufunguo walikimbia kuelekea mahali alipokuwa, mmoja akipitia kushoto na mwingine akipita kulia. Hapo hapo Willy aligundua kuwa jasusi yule alikuwa kafa, hivyo aliinuka haraka. Aliruka kama nyani na kukamata sehemu ya juu ya ukuta. Alijipinda na kupanda juu ya paa akajibanza. Mara tu baada ya kupanda juu ya paa ya nyumba, Stumke na mwenzake walifika sehemu ambayo Willy alikuwa amesimama muda kitambo. Walikuta wenzao wawili wamekufa. Waliingiwa na woga sana.

"Grande, mtafute haraka tumuue, unasikia", Stumke alimwamrisha mtu wake wasiwasi mwingi.

"Willy, uko wapi? njoo tuonane uso kwa uso kama kweli wewe ni mwanaume", Grande alisema kwa sauti. Willy ambaye alikuwa amelala juu ya paa alijisikia raha alipoona majasusi yale yanapaparika kwa woga. Mara aliinuka na kwa spidi kubwa Willy alijirusha katikati yao. Lakini wakati akiwa bado yuko hewani aliipiga teke bastola ambayo Grande alikuwa nayo mkononi. Silaha hiyo ilianguka upande wa pili wa ua. Stumke ambaye alikuwa ameangalia upande mwingine aligeuka na kufyatua risasi. Wakati ule ule Willy alijiviringisha chini na risasi zile zikampata Grande.

"Stumke, umeniua! Aibu", Grande alilalamika halafu akakata roho pale pale. Willy aliamka na kumwahi Stumke. Aliipiga teke bastola yake ambayo iliruka na kutua juu ya paa ya nyumba. Mara mapambano makali yakaanza.

Stumke alimpiga Willy teke la tumbo ambalo lilimpata barabara na kumwangusha chini. Kabla hajaweza kusimama, Stumke alimwongeza teke jingine la ubavuni. Halafu aliamua kumrukia ili ammalize kabisa. Kumbe Stumke alikuwa amefanya makosa. Wakati huo huo Willy alijiviringisha kidogo na Stumke akamkosa. Willy alijipinda na kusimama. Alikuwa amejisikia damu yake imeanza kwenda mbio kutokana na kupigo. Hasira zilikuwa zimempanda. Angeweza kummaliza Stume pale pale, lakini Willy alimpa nafasi naye ainuke. Jambo hilo lilimshangaza sana Stumke.

"Simama kaburu mshenzi, wee! Ulichokuja kutafuta leo utakipata. Kama mlifikiri mkutano hautafanyika mlijidanganya. Wakati ukiwa jehanamu mkutano utakuwa unaendelea", Willy alisema kwa hasira.

Stumke alikuwa bingwa wa karate katika jeshi la KULFUT. Hivyo alimsikitikia Willy kwani alifikiri angeweza kumamliza mara moja. Aliamini kwamba hakukuwepo mtu yeyote kutoka katika nchi za Afrika ambaye angediriki kupigana naye. Stumke alikuwa mwoga kila mapambano yalipokuwa sura ya kutumia silaha kama vile bastola. Lakini kama mtu alipambana naye kwa kutumi mbinu za karate, basi Stumke alimhesabu mtu huyo kuwa ni marehemu.

"Utajijutia leo", Stumke alisema. Mara alimrukia Willy na kutoa mapigo matatu ya karate ambayo hata Willy hakutarajia kamwe. Stumke alishangaa kwani Willy aliyazuia yote. Ni mara chache ambazo Stumke alikuwa ametumia mapigo ya namna hiyo wakati wa mapambano. Na kila alipoyatumia ni watu wachache ambao waliweza kuyazuia. Jambo ambalo alikuwa hajui Willy alikuwa Ninja.

Stumke alibadili mbinu na kutumia zile za hali ya juu kabisa. alitoa pigo la kwanza ambalo Willy alilikwepa. Alitoa pigo na pili na Willy alilizuia. Alipotoa pigo la tatu Willy alimkamata mkono ghafla. Aliukata kwa kiganja chake nao ukavunjika. Hata hivyo Stumke alijirusha na kumpiga Willy teka farasi ambalo lilimwangusha chini. Wakati huo huo Stumke aliguna kutokana na maumivu ya mkono wake uliovunjika. Alimtupita teke la mauti Willy lakini alikuta patupu! Willy alikuwa amejipinda kama swala na kuushika mguu wa Stumke akiwa bado hewani. Aliupinda na kufyatua mfupa wa goti.

Willy alimsukumiza Stumke kwenye ukuta ambapo aligonga kichwa chake na kuona nyota. Fahamu zilimpotea. Willy alimfuata kasi na kumkata karate iliyoacha mkono wake wa pili bila kuwa na kazi. Alimtingisha huku akisubiri fahamu zimrudie. Stumke alipopata fahamu, alijuwa kuwa ameshindwa. Hivyo kama lile jasusi Paul lilivyokuwa limefanya, Stumke alitoa ulimi wake nje na kuukata haraka kwa meno. Kwa haraka, Willy alimtia ngumi moja Stumke halafu akamwacha akate roho kwa kutokwa na damu.

"Ama kweli majasusi hawa ni watu wa ajabu. Kujiua kwa kujikata ulimi ni jambo geni kabisa", Willy alijisemea huku akielekea ndani ya nyumba. Mle ndani alikuta maiti ya mzee Hamisi. Hapo hapo akagudua kuwa mzee hamisi alikuwa amelazimishwa kumwita ili aje auawa kama yeye. Vile vile Willy aligundua kuwa kama majasusi hawa waliweza kuutumia uhusiano wake na Hamisi, basi tayari

walikuwa na habari nyingi juu yao. Willy alijipongeza, bahati yake nzuri kwani mtego waliokuwa wamemwekea ilikuwa bahati kuukwepa.

Mara wazo likamjia. Alifikiri jinsi F.K. alivyokuwa anaaminiwa hapo Arusha kuwa mtu mwaminifu kwa Serikali na Chama. Kama kweli anahusika, bila shaka ndiye anayetayarisha mpango mzima. Mzee Hamisi asingeweza kumhisi kitu F.K. Ndio sababu waliweza kumwingia kwa urahisi. Mzee Hamisi alikuwa anajulikana kama mtu matata. Isingekuwa rahisi kwake kuuawa 'kike' hivyo. Willy aliamua kurudi alipokuwa amelala Stumke. Alimkuta bado hajakata roho kabisa. Alimpapasa ili kuona kama angepata kielelezo chochote. Hakukuta kitu bali funguo za gari. Alizichukua na kuelekea sehemu ya mbele ya nyumba.

Alikuta gari aina ya Benz. Alichukua kalamu yake ambayo ilikuwa na tochi vile vile, na kumulika kwenye karatasi ya bima iliyokuwa imebandikwa katika kioo cha mbele cha gari. Bima hiyo ilikuwa imechukuliwa kwa jina la Feroz Kassam. Kwa kutumia funguo zile zile, Willy alifungua mlango wa gari na kuingia ndani. Aliwasha gari lile na kuondoka. Wakati akiendesha Willy alijikuta akisema.

"We gari, nipeleke nyumbani kwenu, na leo hii bwana yako atanitambua!".

"Jumba lenyewe ni lile pale", Nyaso aliwaonyesha mara walipofika kwa F.K.

"Seng'enge yote ile mnayoiona imezunguka eneo la jumba hilo", waliangalia eneo hilo kwa makini kwani kila sehemu ilikuwa inawaka taa.

"Hili ni jumba hasa", Rocky alisema.

"Wacha kulishangaa kwa nje. Ndani yake ni zaidi. Siku moja mimi nililala humo. Mara nilisikia mlio wa vitu fulani kutoka chini. Nilipomwuliza nini ilikuwa, F.K alijibu huku akiwa mwenye nusu usingizi.

"Hao ni watu wanafanya kazi huko chini, wewe lala usiwe na wasiwasi. Mambo haya hayakufai! Siku hiyo ndiyo nilijuwa jumba hilo lilikuwa na vyumba chini ya ardhi. Siku nyingine F.K alifurahi sana halafu akanieleza kwamba, kama lingetokea jambo la dharura, jumba lile lina njia mbili za kutokea nje kupitia chini kwa chini. Aliongeza kusema kwamba njia moja ilitokea Magharibi na nyingine ilitokea Kusini mashariki mwa jumba hilo. Alinieleza pia kwamba kwa nje mtu yeyote angefikiri labda sehemu ya nje ni mahali palipofunikwa tu. Aidha mfuniko wa njia ulionekana kama ule wa machafu", Nyaso alieleza huku akiendesha pole pole.

"Mimi naona usimame hapa. Sasa hivi ni saa nne kamili. Sijui utaegesha wapi halafu utasubiri, tusingependa waone gari lako", Bon alimwambia Nyaso.

"Itawachukua muda gani?", Nyaso aliuliza.

"Tupe nusu saa. Ukikuta hatujarudi, ujuwe mambo yameharibika. Hivyo utakwenda Hotelini na kumweleza Willy", Bon alijibu.

"Una maana gani?", Nyaso aliuliza.

"Usiniulize maswali, fanya kama nilivyokwambia kwani hiyo itakuwa rahisi kwako", Bon alijibu kwa sauti kali kidogo.

"Haya bwana, mimi nakwenda kwa rafiki yangu hapo juu kwenye nyumba za wasabato. Saa nne na nusu juu ya alama nitakuwa hapa", Nyaso alijibu.

"Sawa, tutakuwa tumejibanza kwenye mti ule pale", Bon alieleza na halafu wakatelemka. Nyaso aliondoka huku roho ikimdunda.

# SURA YA KUMI NA MBILI

**KUFUATANA** na maelezo ya Nyaso, jumba hili linazo njia mbili za kuingilia kwa chini. Moja iko magharibi na nyingine iko kusini mashariki, wewe utaingilia magharibi na mimi nitapita kusini mashariki. Kama hatukuonana ndani basi tukutane mahali petu kabla ya saa nne na nusu", Bon alimweleza Rocky.

Wote walitazamana kwa hisia zao zilizowajulisha kwamba walikuwa wanaingia mahali pa hatari. Huku wakiwa wamejidhatiti, walipeana mikono na kuingia kazini. Rocky alikuwa wa kwanza kuona mfuniko ulioziba mlango wa njia. Aliuinua taratibu na kuona ngazi za kutelemkia chini. Aliuweka kando mfuniko ule ili wakati wa kutoka nje usije ukampa tabu. Baada ya kufanya hivyo, alichukua tochi yake yenye saizi ya kalamu akamulika na kutelemka ngazi jambo ambalo Rocky hakufahamu ni kwamba wakati mfuniko ule ulipofunguliwa ulikuwa unapeleka miale ya ilani, ambayo ambayo ilionekana kwenye televisheni iliyokuwa chumbani, kwa ajili ya usalama.

Dave alikuwa ndani ya chumba cha kumi akiangalia helikopta ya namna yake ambayo ilikuwa chumbani tayari kwa ajili ya kuwachukua majasusi baada ya kufanya maovu yao. Mara alisikia jasusi mmoja kwa jina la Terre akimwita. Terre na wenzake wawili walikuwa wamejinyoosha kwa mapumziko. Aligutushwa na makelele kutoka kwenye televisheni pamoja na picha ya mtu aliyeonekana akiingia kwenye njia ya siri upande wa magharibi. Dave alipofika na kuona picha hiyo, aligundua mara moja kwamba yule alikuwa Rocky kutoka Zimbabwe. Dave aliweza kumtambua Rocky kwa sababu alikuwa ameonyeshwa picha za wapelelezi mashuhuri wa Afrika, majina yao na nchi walizotoka.

"Haya sasa, kazi imebaki kwenu. Huyu amejileta mwenyewe badala ya sisi kumtafuta. Terre na Gary nendeni kwenye mlango ule. Akifungua tu nataka mmalize mara moja. Sisi tunamwona lakini yeye hatuoni. Hivyo kazi yenu itakuwa rahisi. Hakuna haja yangu mimi kuhangaika. Nitakuwa nawaangalia kwenye televisheni. Sitaki mtumie bastola bali mikono yenu. Hapo ndipo watu hawa watatambua sisi ni nani", Dave aliamrisha huku furaha imemjaa. Dave na Howe walikaa tayari kushuhudia mapambano ambayo yangefuatia.

"Huyu ni chakula chetu", Terre alijibu huku akiondoka pamoja na Garry. Walikuwa wamepandwa na mori kwani walitaka kuonyesha uhodari wao, pia kuwa mtu wa kwanza kumuua mpelelezi mashuhuri wa Afrika. Bila kujua kuwa alikuwa

anaonekana kwenye televisheni, Rocky aliendelea taratibu kwa tahadhari kubwa sana. Alipomaliza ngazi za kwanza, aliufikia mlango. Upande wa pili wa mlango, Terre na Garry alikuwa wakisubiri tayari.

Ili wamsaidie kuingia kwenye mtego, walikuwa wamefungua mlango na kuuacha umerudishiwa tu. Rocky alipojaribu kufungua mlango alikuta umerudishiwa. Kutokana na uzoefu wake wa kazi wa muda mrefu. Rocky alifungua mlango ghafla na kwa nguvu. Terre na Garry walitarajia Rocky angefungua taratibu na kuendelea kutembea. Badala yake alijirusha chini kwenye njia. Alifanya kitu ambacho hakikutarajia mpaka wakashindwa kufanya yale waliyokuwa wamepanga. Alijiviringisha chini na kujipinda huku akichukua bastola yake. Alifyatua risasi mfululizo ambazo zilimpata Terre na Garry. Wote wawili walikufa pale pale.

Dave na Howe ambao walikuwa wanafuatilia mapambano kwenye televisheni, walishangazwa na kitendo hicho cha Rocky chenye kuonyesha ujuzi wa hali ya juu.

Howe, twende tukamkabiri kwani naona mtu huyu ni hatari sana. Chukua bastola na mimi nipatie moja", Dave alimwagiza Howe.

"Wewi ni Ninja, huyu atakuwa nini kwako?", Howe alimpambisha Howe moto.

"Unasema kweli, kama hujaniona basi leo utaniona", Dave alijigamba huku wanaelekea kwenye mlango katika njia ambayo Rocky alikuwa akitokea.

"Dave, nafikiri tusisogee kwenye mlango kwani mtu huyu anaweza kutufanya kama Terre na Garry. Heri tumsubiri hapa. Kwa kuwa chumba hiki ni kipana kiasi cha kutosha, hata kama akijirusha bila shaka ataimba tu", Howe alisema huku akijitayarisha na kumwangalia Rocky kwenye televisheni kwa mara ya mwisho. Rocky aliendelea kunyata na kuusogelea mlango wa chumba kile cha mapumziko.

Mlango wa sita wa maarifa ulimjulisha Rocky kwamba chumba alichokuwa akisogelea kilikuwa cha hatari zaidi. Hivyo alichukua tahadhari zaidi. Alikuwa tayari amepandwa na mori wa kupigana. Kwa hiyo alijiona kuwa alikuwa na uwezo wa kupabana katika hali yoyote ile. Dave ambaye alikuwa amesimama pembeni karibu na mlango ule, alitarajia Rocky angejirusha chini baada ya kufungua. Badala yake Rocky aliruka hewani na kuufungua mlango kwa kuupiga teke akitumia miguu yake miwili. Wakati bado akiwa hewani, Rocky alijipinda na kutua njiani nyuma yake. Howe aliyekuwa anasubiri Rocky kwa hamu alifyatua risasi tatu ambazo zote zilikosa Rocky. Kitendo cha sasa cha Rocky kilikuwa hakikutarajiwa pia.

Dave alimtolea ishara Howe ili amfuate Rocky. Howe alijiviringisha chini kwenye njia huku akifyatua risasi ambayo ilimpata Rocky kwenye mkono wa kushoto karibu na bega. Wakati huo huo Rocky aliachia risasi ambayo ilimpata Howe kwenye paji la uso. Alikata roho pale pale. Akiwa anasikia maumivu makali. Rocky alikimbia mpaka nyuma ya mlango kulikokuwa na maiti ya Terre na Garry. Alirudisha mlango huo. Alichana shati lake mwenyewe na kujifunga mkono ili kuzuia damu isitoke kwa wingi. Dave alijuwa Rocky alikuwa ameumia hivyo alimfuata na kufungua mlango ule. Rocky alikuwa ameweka bastola yake chini. Dave aliruka na kumkumba Rocky na wote wakajiviringika chini.

"Rocky! Unakufa sasa", Dave alisema kwa sauti ya juu. Rocky alikuwa anasikia maumivu makali lakini hali halisi ilimfanya asahau maumivu hayo. Aliinuka haraka akiwa tayari kukabiliana na jasusi hilo. Hapo mapambano makali yalianza. Dave alimshambulia Rocky kwa mapigo safi yapatayo saba lakini yote yalizuiwa. Hapo ndipo Dave alipogundua kuwa alikuwa anapambana na mtu mwenye ujuzi zaidi ya vile alivyotarajia. Hivyo aliamua kutumia mafunzo ya U-Ninja. Vile vile Rocky aligundua kuwa Dave alikuwa na ujuzi wa hali ya juu. Hivyo ilimbidi atumie mbinu kali kuweza kumshinda adui.

Dave alitupa ngumi lakini Rocky aliikwepa nayo ikagonga ukuta na kulitoa tofari moja lililoangukia upande wa pili. Wakati huo huo Rocky alichukua nafasi hiyo kumtia mapigo makali Dave ambayo yalimfanya aanguke chini. Hapo aliamua kuchukua bastola yake kwani aliamini kuwa mtu huyu hakuwa saizi yake. Hivyo alijirusha lakini kabla hajawahi kuichukua bastola yake iliyokuwa chini, Dave naye aliruka na kumwahi Rocky hewani alipompiga teke la kichwa. Rocky alipoteza fahamu na kuanguka chini kwa kishindo.

Bon alikuwa amenyatia toka chumba hadi chumba wakati alipofika kwenye chumba cha televisheni alimwona Dave anampiga Rocky teke la kichwa. Bon aligundua kwamba Rocky alipigwa teke la ki-Ninja ambalo asingeweza kulistahamili.

Bon alikimbia haraka kuelekea kwenye njia ambayo aliamini ndiko walikuwa wakipigania huku hasira na chuki zimemjaa. Rocky alikuwa anapigana kishujaa. Bon alipofungua mlango na kuingia kwenye chumba walichokuwa wanapigania, kumbe alikuwa amechelewa. Dave alikuwa amemrukia Rocky na kumpiga teke la moyoni ambalo lilimuua pale pale Rocky.

"Kufa mbwa mweusi, we!" Dave alitukana. Mara aliona mlango unafunguliwa ghafla na Bon akiingia ndani.

"Mbwa we, umemuua Rocky, nawe utaambatana naye mpaka peponi", Bon alisema kwa uchungu huku machozi yakimtoka. Bon alikuwa na bastola mkononi. Angeweza kumpiga risasi Dave. Lakini badala yake aliitupa kando. Dave alishangazwa na kitendo cha Bon. Vile vile alimwonea huruma kwani aliamini hakuna mtu mweusi ambaye angepambana naye kwani yeye alikuwa ni Ninja.

"Pole sana mbwa mweusi! Na wewe umejileta kwenye kaburi lenu", Dave alijibu kwa dharau. Bila kuchelewa Bon alimrukia Dave na kumpiga vipigo, moja baada ya kingine mpaka akaanguka chini. Lakini alijiviringisha na kuinuka haraka tayari kumkabiri Bon. Bon hakumpa nafasi kwani kabla hajasimama sawa sawa Dave alipewa vipigo kadhaa ambavyo vilimtatanisha. Pale pale alijuwa kwamba alikuwa anapambana na Ninja kama yeye mwenyewe, Bon aliruka na kumtia Dave teke la ubavuni na kumzidishia hasira.

Bon alimwahi Dave na kumpiga teke moja la shingoni na jingine la kichwani kwa wakati ule ule, ambayo yalimfanya Dave achanganyikiwe. Bon alipima hali ya Dave na kuona mbaya. Hivyo alichukua nafasi hiyo na kumtia pigo takatifu la kifuani ambalo lilikibomoa na kufanya damu ifumke na kutapakaa kila mahali. Kabla dave hajaanguka chini, Bon alimwonyesha kiganja na kama kusema. 'pigo linalofuata ni kisasi cha Rocky! Alimzibua tumbo na kuyatoa matumbo ya Dave nje'.

"Kufa Kaburu mshenzi, we!" Bon alisema kwa hasira. Dave alianguka chini akiwa maiti. Bon aliangalia saa yake. Ilikuwa saa tano kasoro dakika tano.

Ilikuwa yapata saa tano hivi wakati Willy alipokuwa anaegesha gari la F.K karibu na ofisi za mjini za mauzo ya General Tyre. Alikwenda haraka kwenye hoteli yake. Alibisha hodi kwenye chumba chake Mike akamfungulia.

"Vipi mwenzetu, mbona umenuna", Mike alimwuliza Willy.

"Hatari, akina Bon hawajarudi?", Willy aliuliza.

"Bado, mimi nina wasiwasi mkubwa", Mike alisema, "Je, umeonana na mzee Hamisi?".

"Mzee Hamisi ameuawa. Sasa hivi mtu wetu ni F.K. Hivi ninavyokueleza, nimeshaua makaburu wanne", Willy alisema na kisha alianza kumsimulia Mike yote yaliyotokea.

"Hivyo Mike, hapa mjini kuna kundi kubwa la makaburu wenye ujuzi mkubwa wa kupigana", Willy alimalizia.

"Kama ni hivyo, mimi napendekeza tulivamie jumba hilo kwani bila shaka majasusi wako humo. Nashauri kwamba kama ikibidi, tuombe msaada wa polisi ama jeshi", Mike alisema.

"Hapana Mike, kazi ya kupambana na majasusi haistahili kuhusisha polisi ama jeshi, kwani wao wanaweza kutumia mbinu za kijeshi tu na kusababisha maafa makubwa. Inatubidi sisi wenyewe tufunge vibwebwe na".... kabla hajamaliza sentensi, alisikia mtu anabisha hodi kwa kugonga mlango. Bastola za wanaume hawa zikawa tayari mikononi. Kwa tahadhari kubwa. Willy alifungua mlango huku bastola yake mkononi.

"Ni mimi....", Nyaso alisema kwa hofu alijikuta amekabiliana na mtutu wa bastola.

"Pole, usiwe na wasi wasi", Willy alisema huku akimvuta Nyaso ndani na kuurudisha mlango.

"Wenzako wako wapi?", Mike alimwuliza Nyaso huku akitweta.

"Waliniambia niwapitie saa nne na nusu. Nilipokwenda kwenye sehemu tuliyoagana, sikuwakuta. Hapo mwanzo walikuwa wamenieleza kwamba kama nisingewakuta basi ilibidi nije moja kwa moja huku ili niwaambie nyinyi", Nyaso alijibu huku machozi yakimlenga. Willy aliangalia saa yake na kuona kwamba ilikuwa saa tano na dakika kumi za usiku.

"Nyinyi subirini hapa. Mimi nitakwenda kuchunguza nini kimetokea, maana tukiondoka wote tunaweza kupishana nao, hivyo tutakuwa tumewachanganya. Nipeni mpaka saa sita na nusu, kama hamkuniona basi mjuwe mambo yameiva hivyo njooni", Willy aliwaambia.

"Hapana Willy, tuondoke wote. Nyaso atabaki hapa ili kama akina Bon wakirudi atawaambia watufuate", Mike alisisitiza.

"Hapana Mike, Willy halielewi sawa sawa lile jumba. Sharti nifuatane naye ili nimwelekeze", Nyaso alisema.

"Sawa Mike, utabaki hapa nami nitafuatana na Nyaso. Akisha nionyesha atarudi hapa. Kama ikifika saa sita na wewe hujaniona, basi nifuate", Willy alitamka.

"La hasha, mimi nitabaki huko na wewe....", Nyaso alisema na huku Willy akimkatisha.

"Nyamaza! Wewe unajuwa watu wale pamoja na bwana yako ni wauaji. Je, unataka kufa ama nini", Willy alisema kwa ukali.

"Hebu usiniambia kuwa bwana yangu ni muuaji! Kuna tofauti gani kati yake na wewe. Nyote wauaji tu. Kwani mimi nilifahamu kuwa yeye ni muuaji?", Nyaso alijibu kwa hasira. Willy alishikwa na hasira nusura ya kumnasa kibao Nyaso. Lakini Mike aliingilia kati.

"Basi basi, acheni hayo. Tunapoteza muda wetu. Wewe Nyaso usipende kugombana na wanaume. Utaumia. Mpeleke Willy kama alivyokwambia.

Nyaso alimtazama Willy kwa macho ya upendo. Alimkimbilia na kujilaza kifuani kwake huku akisema kwa sauti nyororo.

"Samahani Willy, sikuwa na maana hiyo. Nakupenda, tafadhali jihadhari", Willy alimvuta na wote wakatoka nje.

"Nawatakia kila la heri", Mike alisema.

"Ahsante!", Willy na Nyaso walijibu kwa pamoja wakati wakitoka nje.

## MAMBO BADO

Ilikuwa yapata saa sita kasoro dakika kumi wakati Bon alipobisha hodi kwenye chumba cha Willy, huku akiwa na bastola mkononi tayari. Mike alikwenda kufungua. Akiwa tayari kabisa, aliruka haraka upande.

"Lo! Mungu wangu vipi?", Mike aliuliza baada ya kumwona Bon".

"Willy yuko wapi?", Bon aliuliza kabla ya kujibu.

"Amewafuata", Mike alijibu.

"Kama nusu saa hivi. Nyaso amempeleka na atarudi si muda mrefu. Rocky yuko wapi?", Mike aliuliza.

"Mike. Rocky ameuawa", Bon alijibu.

"Hapana", Mike alisema bila kuamini.

"Ukweli ni kwamba watu hawa ni majasusi wa hali ya juu. Twende tumfuate Willy. Huko njiani nimeona gari likielekea nyumbani kwa F.K. likiwa limejaa watu. Iwapo Willy yuko peke yake, atapata matatizo. Heri tumfuate kwani hatuwezi kumpotenza na Willy pia. Mambo mengine nitakueleza njiani. Kwani hatuna muda. Nyaso akirudi anaweza akatusubiri hapa hapa", Bon alisema.

Bila kusema neno Mike alichukua zana zake na wanaume wakatelemka chini. Mbele ya hoteli walipungia taksi na kupanda.

"Tupeleke Themi Hill", Bon alimwamrisha dereva. wakaondoka.

Willy alipopata fahamu kidogo akajikuta ndani ya chumba kikubwa. Alikuwa amefungwa kwenye mti mfano wa msalaba uliokuwa katikati ya chumba. Ingawa Willy alikuwa amepata fahamu huku akiumwa sana na kichwa, hakuonyesha kama amepata fahamu. Alifanya hivyo 'kununu muda' Alishangaa kukuta majasusi walikuwa bado hawajamuua. Hapo hapo aligundua kuwa walikuwa na sababu ya kumweka hai. Kwa kutumia sababu hiyo aliweza kununua muda zaidi. Alijikuta amefungwa barabara kiasi kwamba asingeweza hata kujitingisha.

Mara alisikia mlango unafunguliwa na taa kali zaidi zinawashwa na kuelekeza mwanga wake kwake. Pale pale Willy alitambua kuwa chumba kile kilikuwa chumba cha mateso. Alikuwa amevuliwa nguo zake zote na kubaki na chupi tu.

"Hecke, bila shaka umempiga sana mtu huyu, nusura umwue. Unajuwa mtu huyu tunamhitaji sana angalau kwa muda wa dakika tano zaidi akiwa hai", F.K alisema. Willy aliyasikia maneno hayo.

"Mtu huyu ni hatari sana F.K. Hecke alichofanya ni sawa sawa", mtu mmoja alisema na Willy akamsikia.

"Sharti turudishe fahamu yake maana yule mwenzake anaweza kuwa anajongea kwa wakati huu", F.K. alisema.

*****

"P.G yuko nje tayari kumfungia kazi. Hecke na wewe nenda nje ukamsaidie P.G. kama ikibidi. Akidiliki kupitia njia ile ya chini kama alivyofanya mwanzo, huo ndio utakuwa mwisho wake, kwani nimemtegeshea bomu moja safi", George alijigamba.

"Hebu kwanza Hecke, nenda ukawashe ile swichi ya umeme ili umshitue mbwa huyu kwani amezirai muda mrefu", F.K. alimwamrisha Hecke. Willy akajiweka tayari huku akili yake ikifanya kazi haraka haraka. Hecke alikwenda akawasha swichi. Umeme ulimshitua Willy naye akajifanya kaupata fahamu tayari ili asiumizwe zaidi. Alipofungua macho alimwona F.K. amesimama mbele yake pamoja na George. Kule pembeni alimwona Hecke.

"Karibu kwetu Willy Gamba. Ni jambo lisilofurahisha kukukaribisha hapa nyumbani kwangu katika hali hii. Lakini umeyataka mwenyewe na kama ujuavyo msiba wa kujitakia hauna kilio. Haya, huyu hapa ni mwenzetu na kiongozi wetu Geoge ambaye anaongoza kikundi cha 'KULFUT' kilichotumwa kuja kuifundisha adabu Tanzania", F.K alisema akiwa anamtazama Willy. Baadaye alimgekia George.

"George, huyu ndiye Willy Gamba kama umewahi kumsikia. Ni bahati yake mbaya kwamba amekutana na wewe", F.K. alisema.

"Hata mimi nimefurahi kumwona, nimesikia habari zake nyingi. Nasikitika kumwona katika hali hii, hata anapokuwa amefikia mwisho wa maisha yake haya yote yametokana na nchi ya Tanzania kujiweka kimbelembele na kujiingiza kwenye mambo yasiyowahusu", George alijigamba.

Aliposikia hayo Willy alianza kuzungumza ilimradi aweze kusukuma wakati.

"F.K... ni lazima umweleze kaburu huyu swala la ukombozi Kusini mwa Afrika ni swala la Afrika huru nzima. Hivyo kwa watu kufa ili vizazi vilivyobaki viweze kuwa huru ni jambo takatifu. Kwa hiyo mimi sina wasiwasi na kufa".

"Hecke, hebu nenda huko nje ukamsaidie P.G. kumumaliza huyo mbwa mweusi mwingine kwani naona hawa wana vichwa vigumu kama vya paka", George alimrisha.

"Kitu kimoja ambacho unapaswa kuweka maanani Willy ni kwamba, mtu mweusi hawezi kujitawala. Sana sana atapata uhuru wa bendera lakini uchumi wenu utatawaliwa na mtu mweupe daima. Chukua mfano wa Tanzania ni nani anayefaidi matunda ya uhuru hapa kama siyo mzungu na mhindi?, Mhindi akiendesha Benz ni halali yake; thubutu mtu mweusi aendeshe Benz kama hakutiwa msukosuko. Sasa, kisa gani hata kupoteza maisha yenu kwa kupigania uhuru wa bendera ambao huna faida? kweli mtu mweusi hawezi...", F.K. alisema na kukatizwa.

"F.K. unazungumza maneno ya kitoto. Nchi huru za Afrika zinapigana dhidi ya ubaguzi kwa sababu hazitaki ubaguzi. Nyinyi wahindi mnaonekana kama watanzania machoni mwa watanzania. Mawazo yako katika kuhusu uhitilafiana kimapato ni jambo lililopo Ulimwenguni kote. Amini usiamini, kama usaliti wako utagunduliwa, hata kama mimi nitakuwa nimekufa, wahindi wenzako watakuwa wa kwanza kutamani kukurarua. Siyo wahindi wote wenye mawazo finyu kama yako", Willy alimwambia F.K.

"F.K. unamchelewesha huyu mtu. Hebu muulize atupe habari zetu halafu... Usiku unakwenda haraka sana", George alimwambia F.K.

"Kusema kweli Willy nilipenda kifo chako kije haraka. Hata hivyo huo ni uamzi wako. Kama utajibu swali langu, utakufa haraka bila kupata mateso. La hasha, utakufa pole pole na kwa uchungu mkubwa. Chumba hiki kina kila aina ya vifaa vya kutesea. Sina haja ya kukueleza kwani wewe mwenyewe ni mwenyekiti katika shughuli hii. Sasa jibu swali langu: Viongozi wa wapigania uhuru wamefichwa wapi?", F.K. aliuliza. Mara Willy aligundua kwamba mpango wa kuwaficha viongozi wa wapigania uhuru ulikuwa wa busara sana.

"Sijui. Kawatafute wewe mwenyewe. Kwani sisi tulipogundua hawa makaburu ulipowaficha ulituambia?", willy alijibu kwa kiburi. Jibu hilo liliwafanya wahamaki. George alimrukia Willy na kumtia makonde ya haraka haraka mpaka Willy akapoteza fahamu kwa muda.

"Sisi hatutaki mchezo. Tumekuja Tanzania kuwatia hofu na kiwewe. Jibu lako litatusaidia kuua viongozi peke yake kuliko kufagilia mbali umati wa watu na mji mzima wa Arusha. Kipigo tutakachotoa kitasikika mpaka huko ahera. Nyumba hii imejaa silaha za kisasa za kuweza kuuteketeza mji mzima. Sasa sema ama hakika utaumia", F.K. alisema kwa hasira. Willy alifahamu fika kwamba hakuna mtu ambaye angethubutu kumuua, kwani alijuwa wao walitaka kufahamu viongozi wa wapigania uhuru wako wapi. Hilo ndilo jambo muhimu lililokuwa limewaleta.

"Sijui walipo, fanya unavyotaka", Willy alijibu.

"Umeyataka mwenyewe", F.K. alijibu huku akitoa kitu mfano wa saa kutoka kwenye mfuko wa shati na kukiwasha. Mara Willy alijisikia moto unamchoma kutoka kwenye ncha ya kidole mpaka utosini. Alijaribu kuvumilia. Lakini uchungu ulizidi na Willy akaanza kupoteza fahamu. Bila ya kujifahamu Willy alitoa sauti kali.

"Aaaaaa! Nitakuelezeaaa!".

Wakati F.K na George wanamkabiri na kumtesa Willy katika kile chumba cha mateso, Bon na Mike walikuwa wamefika kwenye seng'enge ya jumba la F.K. tayari kwa mapambano makali.

"Tusipite kwa chini maana wanayo televisheni watatuona. Tupite njia ya kawaida ila tujuwe kuwa wanatusubiri", Bon alisema.

"Sawa", Mike alijibu.

"Pande zote mbili, kushoto na kulia zinayo madirisha makubwa. Jambo la kufanya ni kujitahidi kuingia na sisi tuonane huko ndani", Bon alimweleza Mike. Wote waliangaliana ili kupeana moyo.

"Jihadhari sana", Mike alimweleza Bon.

"Na wewe vile vile", Bon alijibu huku akimkumbuka marehemu Rocky aliyekuwa amemuaga kwa namna ile.

"Jambo la kwanza ni kuangalia kama Willy angali hai. Nina wasi wasi juu ya maisha yake", Bon alimnong'oneza Mike huku wakiachana. Mike alimuonyesha ishara ya kumwelewa Bon. Wakiwa wamejificha kwenye vivuli wanaume hao wawili walilisogelea jumba la F.K. kwa tahadhari na hamasa kubwa.

# SURA YA KUMI NA TATU

**MIKE** aliambaa ambaa katika upande wake; mara alisimama kimya na kwa tahadhari alijaribu kusikia kila aina ya jambo ambalo lingetokea. P.G alikuwa upande wa kaskazini wa jumba lile. Mara alimwona Hecke aliyekuwa achunge upande wa kushoto wakati yeye P.G akichunga upande wa kulia.Wakati P.G alipokuwa anaambaa na ukuta wa kulia huku bastola mkononi. Mike naye alishafika kwenye ukuta ule ule akiangalia akiangalia namna ya kufungua dirisha bila kuwashitua watu waliokuwa ndani.

Mara P.G. alisikia jasho jembamba likimtoka. Pale pale alijuwa kuwa alikuwa katika hali ya hatari kwani hali hiyo humtokea mara tu hatari inapobisha hodi. Mike ambaye alikuwa amevaa nguo nyeusi alisogea mbali kidogo kutoka alipokuwa kwani naye alihisi kitu kinatembea karibu na ukuta ule. Alibana chini ya mti huku macho yake yamezoea giza. Mara alikia kitu kama mti kinakatika! Alipoangalia umbali wa mita mbili kutoka chini ya mti alipokuwa amesimama aliona kitu kinatingishika. Alipoangalia vizuri aliona mtu anasogea. Mike alisimama kama mti mkavu. P.G. naye alikuwa ananusa nusa huku na kule kama mbwa wa polisi huku bastola yake tayari kufyatuliwa wakati wowote.

Alipotembea na kufika sehemu ya mita moja kutoka mahali Mike alipokuwa amesimama, naye alisimama. Wakati huo huo Mike aliruka kama risasi. Alimkumba P.G. na wote wawili wakaanguka chini. Bastola ya P.G. ilianguka kando na kuzitema risasi zake. mlio wake haukusikika ndani ya jumba kwa sababu bastola ile ilikuwa na kiwambo cha kuzuia sauti. Walipoinuka, Mike alimtambua P.G. mara moja.

"Ni bahati iliyoje kwangu P.G.? Nilidhani umenikimbia huko Nairobi. Sasa mimi na wewe", Mike alisema na kumshangaza P.G. ambaye hakutarajia kukutana na Mike Arusha.

"Umejileta wewe mwenyewe kwenye kifo chako Mike Maina. Baada ya kukumaliza wewe nitarudi Nairobi. Kisha nitajibadilisha na kuhakikisha vile vikaragosi vyako kwenye ofisi yenu ambao walitaka kuharibu kazi yangu nawafagilia mbali. Kwa kutumia uwezo wangu wa kipesa, nitahakikisha Masoga anakuwa mkuu wa idara yenu..." P.G. alisema. Kisha alikatisha sentesi ili amchukue Mike kwa ghafla ili amtie 'mapigo ya kifo', kama yeye alivyokuwa

anayaita. Lakini P.G. alipotupa mapigo yake hayo Mike aliyazua yote kwa ufundi wa hali ya juu.

"Nilimwahidi Mwaura kwamba nitalipa kisasi chake kwa mikono yangu mwenyewe. Sasa P.G. umekufa", Mike alisema na pale pale aliona sura ya maiti ya Mwaura ilivyokuwa imepigwa risasi. Mori ulimpanda. Alijisikia akipata nguvu zisizo kifani. Mike alimtia pigo la kifuani P.G. ambalo karibu lingemdondosha. Lakini alijitahidi na kurudishia mapigo makali sana. Mike aliteleza mpaka chini. P.G alivuta upanga wake ili ammalize Mike. Upanga ulikuwa umefichwa kiunoni. Huku akiamsha upanga, tayari kumkata Mike P.G. alisema.

"Burian Mike!", wakati huo huo Mike alijiviringisha na upanga ukamkosa, P.G. alijirusha na kujitayarisha tena kumkata Mike. Alimkosa mara ya pili na mara ya tatu. Mike aliruka na kuumpiga teke mkono ule wenye upanga ambao ulianguka chini. Mkono wa P.G. ulikuwa umevunjika. Maumivu yalikuwa makali na Mike alichukua nafasi hiyo. Mike alimtia P.G. kipigo cha mbavu ambazo zilivunjika. P.G. aliamua kujikakamua lakini akawa amezidiwa mbinu.

"P.G. Afrika itashinda na Afrika Kusini itaondokana na udhalimu wa ubaguzi wa rangi na kuwa huru chini ya wazalendo walio wengi. Ukiwa huko ahera utaona kuwa unyama wenu haufui dafu kwa wapigania haki. Hata Mwenyezi Mungu yuko kwenye upande wa wanyonge", Mike alimwambia P.G. ambaye alikuwa anatokwa damu puani na masikioni. Alijua alikuwa amekaribia mwisho wake lakini aliamua kama ni kufa ilibidi afe kiume. Alikusanya nguvu zake zilizobakia na kumrukia Mike. Lakini Mike alikuwa tayari. Hivyo alimpisha P.G. ambaye alijigonga kwenye ukuta na kuanguka chini. Mike alichukua ule upanga wa P.G. na kuutumia kumkata kichwa.

"Malipo ya dhambi ni mauti", Mike alisema huku akiwa ameinua upanga na kuangalia maiti ya P.G. Akiwa bado amepandwa na mori alivunja dirisha kwa kutumia upanga akiwa tayari kwa mapambano makali.

"Leo ni leo. Liwalo na liwe. Sisi na washenzi makaburu ", Mike alisema huku akipanda dirisha ili ajitose ndani.

Baada ya kumtelemsha Willy, Nyaso alielekea New Arusha Hoteli huku akiwa na mawazo mengi sana juu ya Willy. Kitu kimoja kilimshangaza sana na jinsi alivyokuwa ametokea kumpenda kijana huyo. Alikuwa amempenda ghafra kiasi cha kuhatarisha maisha yake wakati alikuwa hamjui sawa sawa kijana huyu.

"Kweli dunia ni msongamano", Nyaso alijisemea huku akiegesha gari karibu na hoteli.

"Mtoto huyo", dereva mmoja wa taksi kati ya wale walioegesha nje ya New Arusha alimnong'oneza mwenzake.

"Sijui mtoto huyo ana nini. Labda F.K. amesafiri kwani namwona anayo njemba moja hivi", dereva mwingine alijibu.

"Ni kweli hata mimi njemba huyo nimemwona. Jamaa mwenyewe mkali na vitu anavyoweka toka chini mpaka juu ni vya ukali tupu", dereva wa tatu alisema.

"Yule ni saizi yake siyo huyo F.K. ambaye anafuja mtoto wa watu bure", dereva wa pili aliongeza huku wakichekelea. Wakati huo Nyaso alishatoka kwenye gari na alikuwa anapotea hotelini. Macho ya watu hao yakimfuata yeye.

"Ama kweli Mungu ana upendeleo angalau kwa kiumbe yule", kijana mmoja wa mapokezi alimnong'oneza mwenzake baada ya Nyaso kuwapita na kusimama akisubiri lifti.

"Huyo msichana mimi simwangalii kwa sababu nikifanya hivyo najisikia msisimko. wakati najuwa fika kwamba hata nishitakie mbingu, siwezi kumpata", mwenzake alijibu.

"Si lazima kupata kila kitu ukipendacho. Hata macho pekee yanatosha kuangalia tu. Mimi ninapoona sura yake humsifia Mungu muumba; halafu kusema kwamba kuna wanaume duniani waliobahatiwa", yule kijana wa kwanza alisema kwa masikitiko.

Bila kujuwa kuwa watu walikuwa wanauguwa roho kutokana na sura yake murua. Nyaso alipanda lifti. Alikuwa na wazo moja tu kwamba kama angekuta akina Bon wamerudi angewataka wamfuate Willy. Alifikiri kwamba kama kweli F.K. amemuua Tondo hata Willy atauawa kama hakujihadhari.

Nyaso alifika kwenye chumba cha Willy. Alibisha hodi lakini hakupata jibu. Alibisha mara ya pili lakini kukabaki kimya. Aligonga tena mara hii kwa nguvu lakini bado hakujibiwa. Mara alitokea kijana mmoja mhudumu katika hoteli alisema huku akitabasamu.

"Samahani dada, nimeona jamaa wanaondoka haraka haraka".

"Wangapi", Nyaso aliuliza.

"Wawili", yule mhudumu alijibu.

"Ahsante", Nyaso aliitikia huku nusu akitembea nusu akikimbia, alielekea kwenye ngazi. Alikuwa na wazo la kuwafuata akina Bon na Mike huko kwa F.K. kwani aliamini Willy alikuwa kwenye hatari. Yule mhudumu alimwangalia Nyaso kwa butwaa.

"Ama kweli duniani kuna wanaume! Mimi nikiwa na miadi na msichana kama huyu siwezi kutoka hata itokee nini. Labda niambiwe mama yangu kafariki", yule mhudumu alijisemea mwenyewe.

Wakati mapambano makali yalipokuwa yanaendelea kati ya Mike na P.G. Bon alikuwa anafanya kazi ya kuingia ndani ya jumba la F.K. Hakupata kipingamizi kikubwa. Alipofika kwenye ile sehemu ya kushoto, aliona maiti ya yule askari aliyeuawa na Willy. Aligundua kuwa Willy alikuwa amepitia njia hiyo. Wakati anaangaza ili kuona Willy alikuwa ameingilia dirisha gani, alimwona yule askari mwingine akija. Bon alibana sawa sawa na ukuta akimwangalia askari anasogea kwa wasiwasi na hofu kubwa. Hofu yake iliweza kumfanya yule askari afike mahali alipokuwa Bon bila kuhisi kitu.

Bon aliyekuwa amebana mithili ya kinyonga afanyavyo kunasa inzi, alisubiri mpaka wote wakawa sambamba. Alimvuta na kumtia kabari kisha akamnyang'anya bastola. Alimpekuwa na kukuta hana kitu. Pale pale akimwamrisha.

"Kama unataka kuishi zaidi, nipeleke alipo Willy Gamba. Najuwa yuko ndani", Bon alibahatisha. Hofu ni kitu kibaya sana. Binadamu anaposhikwa na woga, hupoteza uwezo wa kuamua, hivyo akatenda yale ambayo asingeyafanya katika hali ya kawaida.

"Usiniue, twende nikuonyeshe", Hecke alisema kwa hofu.

Hecke alijua hiyo ndio ilikuwa nafasi yake ya mwisho. Alijuwa angemfikisha Bon kwa George, basi huo ndio ulikuwa mwisho wake hivyo Hecke alimwongoza Bon mpaka kwenye chumba cha mateso.

## FUNGA KAZI

"Hapa", sema sasa nakupa sekunde moja", F.K. alimwambia Willy. Willy ambaye alikuwa amejitahidi kupitisha muda akitafuta njia ya kujiokoa alijuwa kuwa sasa

amepatikana. Mara wazo lilimjia ghafla ... F.K. alikuwa ameshika chombo mkononi. Kazi ya chombo hicho ilikuwa ni kuendesha (kwa mbali), mashine ya umeme ambayo ilikuwa kwenye mti ambao Willy alikuwa amefungwa..... Kama angeweza kukata umeme huo kwa njia yoyote ile, basi mfumo mzima wa chumba kile ungeathirika.

Huku akijifanya kana kwamba alikuwa hajapata fahamu sawa sawa, alichunguza kwa chati ile nguzo alikokuwa amefungiwa. Aligundua kuwa ilikuwa na magurudumu chini. F.K. na George walikuwa hatua moja mbele yake. Hivyo Willy aliamua kutenda jambo ambalo wasingeweza hata kufikiria maisha yao yote. Lakini kwa bahati Willy hakupata nafasi ya kutenda kitendo hicho kwani vitu viwili vilitokea ghafla.

Mlango wa nyuma ulifunguka ghafla na kwa nguvu Bon alimsukumiza ndani Hecke. Hecke alimkumba George na F.K. kutoka kwa nyuma na wote wakaingukia ile nguzo alikofungiwa Willy. Kukatokea kishindo kikubwa.

"Kisanduku hicho hapo juu", Willy alipiga kelele.

Kana kwamba walikuwa wamepanga shambulizi hilo kutoka kushoto. Mike alivunja dirisha kubwa la kioo. Huku akiwa na rungu na upanga mikononi, alitumbukia ndani kupitia dirishani. Alikuwa amekatwa na vipande vya kioo lakini alionekana kutotambua. Vitendo hivyo vilitokea ghafla mno kiasi kwamba George na F.K. walipoteza sekunde mbili ama tatu kabla ya kujua nini kilikuwa kimetokea.

Hapo hapo Bon na Mike walichukua nafasi hiyo kufanya kitendo kimoja kwa haraka. Mike alikata kamba alizokuwa amefungiwa Willy kwa kutumia upanga mkali. Bon alikipiga risasi kile kisanduku kama alivyoelezwa na Willy. Mara chumba kikawa giza. Kisanduku kile ndicho kilikuwa kikitumika kuendesha vyombo vya chumba kizima cha mateso.

Kitu cha kwanza ambacho George na F.K. walifanya ilikuwa kujihami. Kama njiwa, George aliruka na kupitia kwenye diridha ambalo Mike alikuwa ameingilia. Lakini pamoja na vurugu hilo Willy alikuwa amemwona. Alitenda vitendo karibu kwa wakati mmoja. Alifungua kamba na kuruka dirishani akimfuata George.

F.K. alijiviringisha na kumkumba Bon mpaka chini. Halafu alipitiliza mpaka kwenye mlango na kukimbilia ukumbini. Bon aliinuka na kumfuata. Hecke aliliwahi lile rungu aliloingia nalo Mike. Alihamaki na kumpiga Mike akaenda chini. Upanga ulimtoka Mike mkononi.

Hecke aliukimbilia ule upanga, lakini kabla hajaushika Mike alimpiga teke la farasi ambalo lilimpeperusha mpaka akaenda chini. Wakiwa wanaonana vyema kutokana na mwanga uliokuwa unatoka kwenye chumba cha pili. Mike alimrukia tena Hecke na kumtia dhoruba ya kichwa wakati Hecke alipokuwa anajaribu kusimama. Hata hivyo, wote wawili walianguka chini. Dhoruba ya Mike ilimfanya Hecke aone nyota na barabara iendayo ahera. Mike alisimama haraka na kuchukua upanga wake. Kama alivyofanya P.G. aliikata shingo ya Hecke na kichwa chake kikaanguka chini.

"Makaburu wenzako watakaposikia juu ya staili ambayo umechinjwa, bila shaka watagwaya, kamwe hawatathubutu kuichezea Afrika huru", Mike alijisemea kimoyomoyo. Akiwa na upanga wake mkononi. Mike alitoka mbio na kuwafuata wenzake ili afahamu ni kitu gani kilikuwa kikifanyika.

Willy aliporuka na kupitia dirishani, alimkuta George anamsubiri tayari. Alikuwa amewasha taa ambayo swichi yake ilikuwa karibu na dirisha hilo. George alikuwa amesimama. Alimwonyesha Willy ishara ya vita vya maninja. Pale pale Willy aligundua kuwa George alikuwa ninja. Bila kuchelewa Willy alipiga magoti na kuinamisha kichwa. Hiyo ilikuwa ishara na imani yao. Kwa kutumia viganja vyake, Willy 'alisema' sala ya ninja vidole vya mikono yake vinaingiliana na kuachama kama meno ya mamba. George naye alifanya vile vile kama Willy alivyofanya. Kama kawaida sala yao ilichukua kama muda wa dakika kumi. Ndipo vita kali ilipoanza.

F.K. alikimbia na kutoka nje ya nyumba. Alibana karibu na mlango akimsubiri Bon ambaye alikuwa anamfuata. Bon alitokea akikimbia F.K. alimtegea na kumkata ngwara. Bon alianguka chini. F.K. aliruka haraka na kumpiga Bon teke la ubavuni kabla hajasimama na kurudi chini. F.K. alimtupia teke la pili. Alikuwa na nia ya kumpiga kichwani, lakini Bon alikuwa macho. Aliudaka mguu wa F.K. na kumfanya aanguke chini Mara wote waliinuka na kukabiliana.

"Leo ndio mwisho wako F.K", Bon alisema.

"Hee, nyie hamjui nguvu ya Afrika Kusini kijeshi. Hata mkituua sisi haiwezi kuwasaidia. Zaidi ya hayo mtazidisha hasira ya makaburu. Hapo ndipo mtakapokiona cha mtema kuni. Vitendo vyenu vitafuatiwa na mashambulizi ya kutisha. Vitendo hivyo vitazisanya nchi zilizo mstari wa mbele na Afrika huru kwa ujumla kukoma ubishi. Kamwe hamtaichokoza tena serikali imara ya Afrika Kusini", F.K. alijigamba.

"La hasha! Sisi tutawaangamiza nyinyi vibaraka na majasusi wa makaburu. Baada ya hapo. Serikali ya Afrika Kusini itatambua kuwa Afrika sasa ni imara. Zaidi ya hayo, kipigo tutakachotoa kitawatia hamasa wapigania uhuru wa Afrika Kusini. Vile vile vijana mashujaa wa Afrika Kusini watapata moyo wa kuendelea kupambana kwa nguvu zaidi. Na lazima makaburu watasalimu amri.... Na sasa hivi kifo chako kimefika, msaliti wee", Bon alisema.

Mara Bon alimrukia F.K. na kumpa vipigo vinne vya haraka haraka. F.K. alipepesuka huku damu zikimtoka midomoni. Hapo hapo F.K. aligundua kuwa hakuwa na uwezo wa kupambana na Bon Sipele.

F.K. alikuwa anafikiri haraka ni nini cha kufanya. Mara aliona gari lilikuwa njiani kuelekea kwenye nyumba yake. Aliangalia taa zake, akagudua kuwa gari lile lilikuwa aina ya Benzi. Na zaidi ya hayo Benzi hilo lilikuwa la kwake mwenyewe F.K. Katika mawazo yake F.K. alifikiri kwamba Stumke alikuwa ndani ya gari hilo. Alidhani kuwa alikuwa amemtoroka Willy na kuwafuata AICC. Mawazo yake yalimdanganya. Hali hiyo ilitokana na woga mwingi uliokuwa umemwingia F.K. kwa mara yake ya kwanza alifikiria kifo na woga wake ukaongezeka. Kufumba na kufumbua F.K. alitimua mbio kuelekea kwenye gari hilo lililokuwa linakuja kwa mwendo wa kasi. Bon alishangazwa na mbio za F.K. Alianza kumfukuza. Mara alijiwa na mawazo kuwa huenda wale walikuwa adui. Hivyo alisimama na kujiweka tayari kwa mapambano ya ziada.

Wakati ule ule Mike alikuwa ameshika upanga wake mkononi. Alikuwa amemuua Hecke. Baadae alimfuata Bon ili kumuongezea nguvu. Alipotoka nje, alimwona F.K. anatimua mbio huku akifukuzwa na Bon. Hivyo Bon naye aliamua kuwafukuzia. Alipomwona Bon anasimama naye akasimama pembeni. Mike alihisi vile vile wale walikuwa maadui. Gari hilo lilizidi kuja kwa kasi. F.K. alilikimbilia kwa kasi pia. Alikuwa ameinua mikono juu kama ishara ya kutaka lisimame. Bon na Mike walibaki wamesimama kushuhudia tukio hilo. Kitendo kilichofuata, kiliwashangaza. Badala ya gari hilo kupunguza mwendo, lilienda kasi zaidi kuelekea kwa F.K. ambaye alijaribu kulikwepa. Hata hivyo lilimkumba.

"Eeeeh! Nakufa!", F.K. alisema maneno yake ya mwisho. Alipogongwa, alirushwa juu na kuangukia kwenye seng'enge.

Bon na Mike waliona gari hilo likisimama mahali pale lilipokuwa limeegeshwa gari la Mzee Hamisi. Wote wawili walifichama nyuma ya mti. Walishangaa zaidi kuona mtu aliyeshuka kwenye gari hilo alikuwa Nyaso.

"Nyaso", Bon alimwita. Mike akaelekea kule ilipoangukia maiti ya F.K.

"Willy yuko wapi?", Nyaso alihoji huku machozi yakimtoka. Pale pale Bon aliwakumbuka Willy na George. Mambo hayo yalikuwa yemetendeka haraka sana.

"He! He! Hapa... hapa", sauti zilisikika.

"wako huku", Bon alimshika Nyaso mkono wakaenda mbio. Walielekea kule sauti zilikokuwa zimetokea. Hata hivyo Bon alikuwa bado ameshangazwa kitendo cha msichana huyu. Ilikuwa vigumu kwake kuelewa jinsi Nyaso alivyomgonga na kumuua bwana yake halafu asijali. Utafikiri hakuna jambo lililokuwa limetokea; ama kwa Nyaso alikuwa amegonga mbwa!.

"Ni vigumu kuwaelewa wanawake", Bon alijisemea kimoyomoyo.

Walifika sehemu walikokuwa Willy pamoja na George. Ilibidi Bon amshike Nyaso ambaye alikuwa ameshikwa na kiwewe. Sababu ilikuwa ni kwamba vita vya maninja vilikuwa vimeanza.

"Willy! Willy! Ooooh", Nyaso aliita.

"Nyamaza! Hivi ni vita vya maninja. Sikiliza Nyaso. Wote wawili ni maninja. Maana yake ni watu wenye ujuzi wa hali ya juu wa kupigana. Wote wawili wamehitimu mbinu za hali ya juu za mapigano ziitwazo ninja. Sheria yao inasema maninja wawili wakianza kupigana, watu wengine hukaa kando. Mapigano huisha babada ya mmoja wao kuuawa", Bon alimweleza Nyaso kwa haraka

"Hivi unaweza kumwacha Willy auawe ati kwa sababu ya sheria?, mimi nakwenda kumsaidia", Nyaso alisema huku akijaribu kujitoa mikononi mwa Bon

"Kama Willy atauawa mimi nitachukua nafasi yake. Hii ni "sanaa" ya mauaji, nayo ina miiko yake. Hata mimi mwenyewe ni ninja", Bon alisema huku akimwangalia Nyaso usoni. Kwa mara ya kwanza Nyaso aliona macho ya Bon yamegeuka na kuwa kama hayana uhai.

"Mimi sikujuwa kama watu walio hai wanaweza kuwa maninja. Nilidhani ni hadithi tu ama michezo ya sinema. Mpaka sasa siamini", Nyaso alisema huku machozi yakimtoka.

Willy na George walikuwa wametazamana. Bon alimshikilia Nyaso kwa nguvu zaidi. Alipogeuka nyuma alimwona Mike amejiegemeza kwenye ukuta. Alionekana kuwa na wasiwasi. Bon alipomwangalia Mike alitoa ishara kuonyesha kwamba F.K. alikuwa amekufa. Hapo hapo wote waligeuza macho yao kuangalia

mapigano makali yaliyokuwa yameanza. Mbinu zilizotumika zilikuwa za hali ya juu. Hata Bon mwenyewe alikiri. Pamoja na yeye kuwa ninja. Alikuwa hajaona mapigano makali kama hayo.

"George aliruka juu. Kana kwamba alikuwa anatembea hewani, alirusha mateke kumi mfululizo. Willy aliyakwepa yote. Kabla hajatua chini. George alichomoa upanga kutoka mgongoni mwake. Akaanza kumkabiri Willy.

Mike alihamaki akataka kuingia kwenye uwanja wa mapambano. Bon alimpa ishara ya kuzuia. Nyaso aligeuka na kulala kifuani mwa Bon. Alihofia Willy angeuawa wakati wowote. George alirusha upanga wake mara saba. Nia yake ilikuwa ni kumkata Willy. Lakini hakuweza kufanikiwa. Willy alikuwa ni mwepesi kama unyoya. Ghafla George aliruka juu na kumkuta Willy hayuko tayari. Bon na Make walifumba macho. Ilikuwa vigumu kuamini jinsi Willy alivyojipindua. Upanga wa George ulimpita kwenye mkono. Ulichana shati yake na kumkata kidogo.

Damu ilianza kumtoka Willy. Hata George mwenyewe alishangaa jinsi Willy alivyokwepa upanga huo. Willy aliangalia damu yake. Hasira ilimpanda. Alisikia harufu ya damu mpaka ule upanga akauona si kitu kwake. Alichana shati lake na kulitupa. Halafu alimrukia George na kumpiga dhoruba ambayo hakuitarajia. Aliupiga mkono wake wa kulia ambao ulikuwa umeshika upanga. Upanga uliruka na kuanguka karibu na miguu ya Bon. Kishindo cha upanga kilimshitua Nyaso. Aligeuka na kushuhudia jinsi Willy alivyokuwa akimtandika yule kaburu.

"Willy alimpiga George mapigo matano mfululizo, ambayo yalimfanya achanganyikiwe.

"Willy, muuee! muuee", Nyaso alipiga kelele. Lakini George alijibu mapigo. Alimpiga Willy kichwa cha aina ya pekee mpaka wote wawili wakaanguka chini. George aliwahi kuinuka, mara hii alitoa kisu kirefu. Halafu alimrukia Willy ili ammalize. Lakini Willy alikuwa macho. Aliruka kutoka mahali alipokuwa na George akamkosa. Bila kuchelewa Willy akamtupia George teke la tumbo akaanguka chini. Katika kuanguka kisu kilimtoka mkononi. Willy alitumia nafasi hiyo. Alimpiga George pigo la pekee ambalo lilimbomoa kifua. George alijuwa amekwisha.

"Aaaa! Nakufa! Willy, heri ungenikata kichwa ili nife kwa heshima za kininja", George alisema Bon alimtupia Willy upanga. Willy alikata kichwa cha George kwa pigo moja.

Nyaso alikurupuka kutoka mikononi mwa Bon, alimkimbilia Willy na kumkumbatia.

Aaaah. Willy! Siamini", Nyaso alisema kwa sauti kali. Bon na Mike walibaki wameduwaa.

"Haya tutoke hapa haraka, kazi iliyobaki ni ya polisi", Willy aliamrisha. Nyaso alitoa kitambaa na kumfunga mkono Willy. Wote waliingia ndani ya gari la F.K. Ingawa lilikuwa limevunjika taa za upande wa kulia. Willy aliendesha na wote wakarudi mjini.

"Hallo!", sauti ilisikika kwenye simu.

Hallo, mimi naitwa Willy Gamba".

"Ndiyo mzee", Kamanda wa polisi wa mkoa alijibu kwa hofu. Alikuwa amepokea simu kutoka kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kutoka Dar es Salaam. Alikuwa ameambiwa asitoke nyumbani mpaka Willy ampigie simu.

"Haya sikiliza. Rafiki yako F.K. amekufa. Vile vile kuna rafiki zake wamekufa. Mzee Hamisi naye amekufa na maiti yako nyumbani kwake. Tondo pia ni maiti. Yapo nyumbani kwake. Naamini sasa unajuwa cha kufanya", Willy alieleza, wakati wakitelemka kwenye gari, kamanda aliuliza.

"Mzee Hamisi amekufa. Amekufa saa ngapi".

"Kati ya saa tatu na nusu na saa nne", Willy alijibu.

"Hiyo haiwezekani. Mimi nilipata habari kuwa mnamo saa nne na robo Mzee Hamisi alikuwa kwenye jengo la mikutano la AICC", Kamanda alisema.

"Yeye mwenyewe ama gari lake?", Willy aliuliza.

"Eah! Askari wanaolinda huku waliripoti kuonekana gari lake. Halafu waliripoti kuwa chumba kilichotayarishwa kwa ajili ya mkutano kiliwashwa taa. Wao walifikiri Mzee Hamisi alikuwa anaangalia na kuhakikisha usalama, kama kawaida yake", Kamanda alijibu.

"Haya, wewe shughulikia taarifa niliyokupa na kwa heri", Willy alijibu na kukata simu. Mawazo ya Willy yalikuwa yanakwenda haraka haraka.

Willy alipiga simu kutoka hotelini kwake New Arusha Hotel. Alikuwa na wenzake akiwemo Nyaso.

"Anasema nini?", Bon alimuuliza Willy. Willy alimweleza maneno ya Kamanda.

"Kama ni hivyo F.K. na wenzake waliweza kuingia kwenye chumba cha mkutano. Na kama waliingia walifanya nini?", Mike aliuliza.

"Maneno yako ni kweli. Bila shaka walikuwa na sababu", Willy aliitika. Kisha aliinua simu na kupiga namba ya mwandalizi wa mkutano wa wapigania uhuru.

"Hallo".

"Hallo. Willy hapa".

"Lete habari. Nimekaa nikisubiri kwa hamu hata mate hayamezeki. Wazee wana wasiwasi mkubwa. Kwani wanapiga simu kila baada ya dakika kumi. Heri tupate taarifa yako. Vinginevyo, kabla ya asubuhi watakuwa wamekufa kutokana na ugonjwa wa moyo", mwandalizi wa mkutano alisema. Willy alimweleza kwa kirefu yote yaliyokuwa yametokea.

"Hure? Afrika huru imeshinda", alijibu kwa ghafla na furaha kubwa.

"Kwa hiyo mkutano utaendelea kesho kama ulivyopangwa. Waeleze wazee kwamba sasa kazi kwao, kazi yetu sisi vijana wao tumeimaliza", Willy alisema.

"Sijui watawashukru vipi", yule mtu alisema huku akionyesha furaha.

"Hivi si wewe unayeshughulikia maandalizi ya mkutano?", Willy aliuliza.

"Ndiyo".

"Basi, naomba tuonane huko. Sisi tunakwenda huku sasa hivi.

"Oke!".

"Haya sasa twendeni. Tayari nimepata wazo. Wewe Nyaso lala na kupumzika. Hayo uliyoyafanya yanakutosha kwa siku moja". Willy aliwaambia wenzake.

"Nani abaki hapa? tunakwenda wote", Nyaso alijibu huku tayari akiwa amefika mlangoni.

"Tunaomba vitambulisho", askari wa ulinzi kwenye jumba la mkutano, AICC waliwaambia akina Willy. Willy alitoa kitambulisho chake. Mmoja wao alikiangalia na kushituka. Aliwaruhusu haraka huku akiwa kama anataka kupiga saluti. Walipoingia kwenye uwanja walikuta yule mtu wao ameshafika.

Alikuwa amekaa juu ya boneti ya gari akizungumza na askari mlinzi. Willy alimfahamisha kwa wenzake.

"Huyu mtoto umempata wapi?", aliuliza.

"Huyu ni kuruta wetu", Willy alijibu kwa mzaha. Wote walicheka, baadaye waliingia kwenye chumba cha mkutano. Mkutano ungeanza masaa machache kutoka wakati huo. Waliongozwa na yule askari mlinzi. Willy aligusa mlango ukafunguka.

"Mliacha mlango wazi?", Willy aliuliza.

"Nadhani", mwandalizi alijibu huku akiwasha taa. Wote waliangaza huku na huko.

"Kuna kitu chochote kigeni ambacho hamkukiacha humu ndani ama kukipanga?", Willy aliuliza.

Walizunguka kote halafu mwandalizi wa mkutano akasema.

"Naona ni kama vitu vyote viko kama tulivyoviacha".

"Kwani Willy unafikiri vipi", Bon aliuliza.

"Ni dhahiri kwamba iwapo F.K. na wenzake waliingia ndani. Halafu askari walinzi wakafikiri alikuwa ni Mzee Hamisi eti baada ya kuona gari lake. Bila shaka watu hao walikuja kufanya hujuma ndani ya chumba hiki. Ni lazima kuna kitendo wamekifanya. Ni kazi yetu sisi kufahamu kitendo gani. Baada ya hapo kazi yetu itakuwa imekwisha. Vinginevyo kazi yetu haijakamilika kamwe". Willy alisema.

"Maneno yako ni kweli tupu", Mike aliitikia.

Mara nyingine ni vigumu kuelewa jinsi gani mambo fulani hutokea. Kwa muda wote huo Nyaso alikuwa amesimama kimya. Alikuwa mbali kidogo na Willy ambaye wote walikuwa wakimsikiliza. Yeye alikuwa amevutiwa na jambo moja ndani ya chumba hicho. Vyombo vya kuzima moto hapo ukutani vilikuwa vimepangwa kisanii.

Vyombo hivyo vilikuwa vimepangwa juu ya ukuta. Kwa pande zote nne vyombo hivyo viliangaliana kimoja na kingine jumla ya vyombo vilikuwa kumi na nne.

"Willy", Nyaso aliita. Willy alimsogelea.

"Unasemaje mtoto?", Willy aliuliza.

"Yeyote yule aliyepanga hivyo vyombo vya kuzimia moto?", Willy aliuliza.

Yule mtu aliangalia ule mpangilio wa vyombo hivyo. Halafu alimwangalia Willy kwa mshangao. Pale pale wote wakawa wamegundua sababu ya mshangao wake. Pale pale walihisi jibu.

"Hapana, vyombo vyote vilikuwa chini. Na jumla yake vilikuwa vinne tu katika chumba kizima", alijibu kwa kufadhaika.

Wanaume walipanda juu. Mike alikuwa wa kwanza kugundua ni nini kilikuwa ndani ya vyombo hivyo".

"Willy,  ujuzi na uzoefu wako umeisaidia Afrika huru. Majasusi walitega mabomu ndai ya vifaa hivi. Mabomu yenyewe yanaendeshwa na mitambo yenye saa", Mike alisema kwa masikitiko. Nyaso aliyasikiliza yote hayo. Lakini hakuamini masikio yake.

"Heri tumekuja na mtoto huyu. Kuja kwake kumetupa faida; kweli naawambia wanawake wazuri wanayo mashetani yao", Bon alisema kiutani. Lakini Nyaso hakuwa katika hali ya utani bali alibaki ameduwaa. Ungedhani kapigwa dafrao. Mambo yaliyokuwa yametendeka, yalikuwa yamemzidi kimo. Vyombo vyote vilitelemshwa. Nane kati ya kumi na nne vilikuwa na maboni ndani yake. Kwa kutumia ujuzi wao waliyategua kwa uanalifu mkubwa. Willy alimwendea Nyaso na kumbusu.

"Ahsante sana Nyaso. Nikumbushe kesho nikununulie pipi", Willy alisema.

"Ahsante, Nitaisubiri hiyo pipi. Lakini hata hivyo sasa hivi ni asubuhi", Nyaso alijibu. Willy aliangalia saa na kugundua ilikuwa ni karibu saa kumi na moja alfajiri.

"La, twende tukapumzike. Sasa ni saa kumi na moja. Kazi yetu tumeimaliza. Imebaki ya wazee", Willy alishauri.

"Sawa kabisa. Sasa tuseme wewe mwenzetu unakwenda na sisi ama ndio mambo yamekunyookea", Mike alimtania Willy.

"Eti unasemaje mtoto. Maana sasa neno lako kwangu ni sheria. Ukisema nife, nakufa. Ukisema fufuka, nitafufuka", Willy alimwambia Nyaso.

"Tuwarudishe hotelini. Halafu wewe utakuwa mgeni wangu. Unakumbuka kwamba uliniahidi kitu, na mpaka sasa hujatimiza ahadi yako", Nyaso alisema.

"Bwana weee, tulepeleke kwanza sisi halafu uende ukatimize ahadi. Ahadi ni deni", Mike alieleza.

"Ningekuwa na bahati kama ya Willy ya kumpata mtoto kama huyu, mimi nisingepoteza hata dakika, kwanza kabisa mtoto mwenyee siyo wa kawaida", Bon aliongeza.

"Eeh, jamani! Mnanifanya nione aibu", Nyaso alinena.

"Achana na hao. Ndivyo walivyo. Tutawapeleka kwanz halafu twende kula vyetu", Willy alisema.

"Ahsante mwenzetu. Tukebehi tu", Mike alijibu wote waliekea kwenye gari.

"Askari hakikisha hamtoki kwenye chumba cha mkutano", Bon aliwaagiza askari wanaolinda chumba cha mkutano AICC. Ambao walikuwa wanatweta kwa jasho kwani ilikuwa vigumu kwao kuamini kuwa chumba walichokuwa wakilinda kilikuwa na mabomu. Pamoja na hayo, kundi la akina Willy hawakuona ajabu wala kuogopa. Wao walikuwa wanafurahi kana kwamba hakuna jambo la hatari lililotokea. Walikuwa wanataniana kwenye hali ya hatari. Hata hivyo walijitahidi na kujibu.

"Ndio afande", walimwaga yule mwandalizi wa mkutano.

"Tutaonana baadaye. Kesho ni kazi kwenu wazee. Sisi kazi yetu tumemaliza. Tunakwenda kutumia matuna ya uhuru wa Afrika", Willy alisema kwa mzaha.

"Sijui niwashukru vipi, kazi yenu ni ukombozi kwa Afrika nzima, Afrika ina deni kubwa kwenu", alisema mwandaaji wa mkutano huku Willy na wenzake wakimuaga na kupanda gari kuondoka.

Waliingia ndani ya gari. Mwanga wa mapambazuko uliwaongoza vijana hawa shujaa wa Afrikal. Walikuwa tayari wamemfungia kazi kaburu. Walikuwa wameipa hamasa Afrika huru ili kusaidia wapigania uhuru wa Afrika Kusini.

Wakati wananchi walipokuwa wanaamka kutoka usingizini, mashujaa hawa ndio kwanza walikuwa wanakwenda kulala. Walikwenda kuota ndoto za kweli za ushindi dhidi ya utawala wa makaburu, ambaye ni adui namba moja wa Afrika. Makaburu...

NI FUNDISHO

"Hebu jamani, tusikilize taarifa ya habari", msichana mmoja aliwanyamazisha wenzake, Akina Bon na Mike walikuwa wamekaa kwenye bustani ya New Arusha Hoteli. Kipaza sauti kilikuwa kimetundikwa kwenye mti katikati ya bustani.

"Hivi kuna habari gani kwenye taarifa ya habari mpaka watu wote wanasogea kusikiliza. Utafikiri kumezuka vita", Mike aliuliza kwa mshangao.

"Wewe unakaa Yerusalemu ya wapi?. Hata usijue matukio yaliyotokea jana usiku hapa mjini?", msichana mwingine alimuuliza Mike kwa kebehi.

"Mimi sujui", Mike alijibu.

"Sasa tulia usikilize", alisema.

"Haya mtoto", Mike alijibu na taarifa ya habari ikaanza.

"Sasa ni saa moja kamili".

"Ifuatayo ni taarifa ya habari kutoka Radio Tanzania. Dar es Salaam... Arusha. Habari za kuaminika kutoka Arusha zinasema kuwa vijana shupavu wa Afrika wamevunja ngome ya makaburu. Ngome hiyo iliyokuwa chini ya majahili wa jeshi la "KULFUT" ama Gongo la chuma iliyoundwa na makaburu kwa lengo la kuongeza hofu kwa nchi huru za Afrika. Kikiongozwa na tajiri wa mjini humo aitwae Ferozali Kassam ama F.K. Kimeteketezwa kabisa. Vyombo na vifaa vingi vya kisasa kwa ajili ya uimarisha ujasusi vimekamatwa. Nia ya kikundi hicho kuweka ngome mjini Arusha ilikuwa kuhujumu mkutano wa wapigania uhuru ambao hata hivyo umeanza leo mjini humo. Habari za kuteketeza ngome hiyo zimepokelewa kwa shangwe kuu na wakuu wa nchi huru za Arika.

"Hata hivyo kiongozi mmoja wa wapigania amezionya nchi huru za Afrika. Amesema ni lazima kuwa macho kwani aduni sasa ameanza kutangatanga. Kwa sababu maji yamewafika shingoni. Vile vile ameiomba jumuia ya Kimataifa kuzidi kuwabana makaburu kiuchumi ili kuleta mabadiliko ya haraka nchini Afrika Kusini. Kwa lengo la kuutokomeza ubaguzi wa rangi na kuleta utawala wa walio wengi. Amewaonya makaburu kuwa mapambano ya silaha yatazidi ndani ya Afrika Kusini. Hakuna kurudi nyuma.

"Habari zingine kutoka Pretoria. Afrika Kusini zinasema: Baada ya makaburu kupata habari ya kuteketezwa kwa ngome ya 'KULFUT', mapambano mapya na makali yamezuka. Mpaka tunakwenda hewani mapambano makali yalikuwa yanaendelea. Wazalendo katika kitongoji cha Soweto wanapambana vikali na polisi wa makaburu....".

"Mmesikia sasa", yule msichana wa pili aliwauliza.

"Tumesikia mtoto. Lililobaki sasa ni sisi kucheza na kula vyetu huku tukishangilia ushindi. Tutumie vyetu mpaka liamba", Mike alijibu.

"Mwenyezi Mungu akupe nini", yule msichana wa kwanza alisema.

"Napendekeza tuondoke hapa, twende kutumia sehemu nyingine. Maana leo ni leo, asemaye kesho ni muongo", Bon alisema huku akiinuka. Alimshika mkono msichana aliyekuwa karibu naye. Aliondoka taratibu. Mike naye alifuatia huku macho ya watu yakiwafuatlia pia.

"Hebu nikuulize Nyaso. Kwanini uliamua kumuua F.K", Willy alimwuliza Nyaso. Wakati huo alikuwa anajigeuza kifuani. Baadaye alimkumbatia.

"Nisingependa wewe kunikumbusha jambio hilo. Huo ni mzigo wangu. Ni heri niubebe mimi mwenyewe", Nyaso alijibu taratibu

"Oke, mtoto", Willy aliitika taratibu halafu alimbusu.

"Willy".

"Ehe".

"Kazi yako tumeimaliza. Lakini sasa ni mwanzo wa kazi nyingine mpya. Kazi hiyo ni yangu. Unakumbuka wewe mwenyewe uliniahidi", Nyaso alisema kwa sauti nyororo.

Willy alimwangalia Nyaso. Alimgeuza humo ndani ya shuka walilokuwa wamejifunika. Alimbusu tena. Alimwangalia machini kwa mahababa. Mara akamwambia.

"Nikumbushe kesho. Kwa sasa hivi ni kazi tofauuti. KILA KAZI NA WAKATI WAKE".

**MWISHO WA HOFU**